**ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**
**MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA**

| | |
|---|---|
| 1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi | MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais |
| 2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani. |
| 3.Mhe. Omar Yussuf Mzee | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais |
| 4.Mhe. Haji Omar Kheri | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu |
| 5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa |
| 6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa |
| 7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary | MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni. |
| 8.Mhe. Rashid Seif Suleiman | MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani. |
| 9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge |
| 10.Mhe. Juma Duni Haji | MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa |

| | |
|---|---|
| 11.Mhe. Zainab Omar Mohammed | MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa |
| 12.Mhe. Said Ali Mbarouk | MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando |
| 13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban | MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa. |
| 14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga | MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe |
| 15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui | MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni |
| 16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan | MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni |
| 17.Mhe. Haroun Ali Suleiman | MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi |
| 18. Mhe. Shawana Bukheti Hassan | MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/ Jimbo la Dole |
| 19. Mhe. Haji Faki Shaali | MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni |
| 20.Mhe. Machano Othman Said | MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni. |
| 21.Mhe. Othman Masoud Othman | Mwanasheria Mkuu |

| | |
|---|---|
| 22.Mhe. Issa Haji Ussi | Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka |
| 23.Mhe. Zahra Ali Hamad | Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake |
| 24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya | Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais |
| 25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake |
| 26.Mhe. Haji Mwadini Makame | Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi |
| 27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi | Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni |
| 28.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak | Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake |
| 29. Mhe. Mohammed Said Mohammed | Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mpendae |
| 30.Mhe. Abdalla Juma Abdalla | Jimbo la Chonga |
| 31.Mhe. Abdalla Moh'd Ali | Jimbo la Mkoani |
| 32. Mhe. Ali Mzee Ali | Kuteuliwa |
| 33.Mhe. Abdi Mosi Kombo | Jimbo la Matemwe |
| 34.Mhe. Ali Abdalla Ali | Jimbo la Mfenesini |
| 35. Mhe. Ali Salum Haji | Jimbo la Kwahani |
| 36.Mhe. Amina Iddi Mabrouk | Nafasi za Wanawake |

| | |
|---|---|
| 37. Mhe. Asaa Othman Hamad | Jimbo la Wete |
| 38.Mhe. Asha Abdu Haji | Nafasi za Wanawake |
| 39.Mhe. Asha Bakari Makame | Nafasi za Wanawake |
| 40.Mhe. Ashura Sharif Ali | Nafasi za Wanawake |
| 41.Mhe. Bikame Yussuf Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 42.Mhe. Farida Amour Mohammed | Nafasi za Wanawake |
| 43.Mhe. Fatma Mbarouk Said | Jimbo la Amani |
| 44.Mhe. Hamad Masoud Hamad | Jimbo la Ole |
| 45.Mhe. Hamza Hassan Juma | Jimbo la Kwamtipura |
| 46.Mhe. Hassan Hamad Omar | Jimbo la Kojani |
| 47.Mhe. Hija Hassan Hija | Jimbo la Kiwani |
| 48.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu | Jimbo la Bububu |
| 49.Mhe. Ismail Jussa Ladhu | Jimbo la Mji Mkongwe |
| 50.Mhe. Jaku Hashim Ayoub | Jimbo la Muyuni |
| 51.Mhe. Kazija Khamis Kona | Nafasi za Wanawake |
| 52.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa | Jimbo la Kikwajuni |
| 53.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk | Jimbo la Kitope |
| 54.Mhe. Mansoor Yussuf Himid | Jimbo la Kiembesamaki |
| 55.Mhe. Marina Joel Thomas | Kateuliwa na Rais |
| 56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa | Jimbo la Mkwajuni |
| 57.Mhe. Mgeni Hassan Juma | Nafasi za Wanawake |
| 58.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma | Jimbo la Bumbwini |

59.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

61.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

62.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

66.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

67.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

68.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

69.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

70.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

71.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

72.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

74.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir Nafasi za Wanawake

**Ndugu Yahya Khamis Hamad Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

**Kikao cha Kumi na Nne – Tarehe 3 Julai, 2013**

*(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)*

**DUA**

***Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua***

**Mhe. Spika:** Wanawake wanaweza! Waheshimiwa Wajumbe kabla sijamuita Katibu kuanza shughuli zetu leo tunao wageni ambao ni vijana wetu, watoto wetu pamoja na walimu wao. Kwa hiyo wageni wetu wa leo Waheshimiwa Wajumbe ni wanafunzi kutoka Skuli ya Mwanakwerekwe 'F'. Wanafunzi hawa ni watu wenye ulemavu na mahitaji maalum na jumla yao ni vijana 50 pamoja na walimu wao 13. Nawaomba walimu pamoja na wanafunzi hao wasimame ili waonekane na kuwasalimu Waheshimiwa Wajumbe.

Ndugu walimu pamoja na vijana wetu karibuni sana ili muone shughuli zetu ambazo tunazifanya kwa ajili ya wananchi zinakwendaje. Karibuni sana, Waheshimiwa Wajumbe ahsanteni sana.

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

**Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria:** Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka 2013/2014. Naomba kuwasilisha

**Mhe. Ussi Jecha Simai (Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala):** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha hati mezani juu ya Muhtasari wa Hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2013/2014. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MASWALI NA MAJIBU**

**Nam.107**

**Ufanisi wa Polisi katika Kudhibiti Uhalifu**

**Mhe. Saleh Nassor Juma -** Aliuliza:-

Ahsante sana Mhe. Spika, kabla ya kujibiwa swali langu nambari 107 naomba kwanza nikubaliane na wewe Mhe. Spika, wetu mara baada ya hii kauli uliyoitoa baada ya dua ya kwamba wanawake wanaweza. Ni kweli kwamba wanawake wanaweza bila ya kuwezeshwa, kwa kweli nimevutiwa sana na uteuzi wako wa huyu *Sergeant at arms* hivi asubuhi alivyokupeleka kwenye siwa pale na kukurudisha sambamba na huyu mama hapa juu mwalimu aliyekuwa ana-*translate* kutoka lugha ya wasiosikia na kuweka katika lugha ya kuwafanya wafahamu wale vijana wetu hapo juu wamenivutia sana.

Sio hilo tu Mhe. Spika, kwamba wanawake wanaweza, lakini hata Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mwanamke. Spika wa EALA yaani Bunge la Afrika ya Mashariki ni mwanamke. Spika wa Bunge la Uganda ni mwanamke. Mimi nawaomba tu kinamama sasa wasimalizie katika uspika, waende mpaka katika urais. Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima na unyenyekevu wa hali ya juu sana naomba swali langu nambari 107 sasa lijibiwe.

Kwa kuwa katika semina iliyofanywa katika mwezi wa Aprili, 2013 baina ya Jeshi la Polisi na Wawakilishi hapa katika ukumbi wa Baraza la Wawakilishi ilionesha wazi kuwa kuna maboresho makubwa yamefanyika tangu kuanzishwa kwa jeshi hilo hadi leo hii. Hii inaonesha wazi tukiangalia mavazi, walianza na bukta na tunga ambapo sasa wanavaa *uniform* za kifahari na za kisasa.

(a) Kwa kuwa ufanisi wa Jeshi la Polisi hupatikana pale panapokosekana uhalifu (*Criminal case*) ndani ya nchi, na kwa kuwa kesi hizo kwetu bado zipo Je, Jeshi letu limekosa mbinu za kitaalamu katika kushughulikia uhalifu.

(b) Ni lini serikali italipatia jeshi letu vifaa vya kisayansi katika kuchunguza dawa za kulevya pamoja na kuchunguza wale wanaoingia na silaha kwa ajili ya kufanya uhalifu.

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais -** Alijibu:-

Mhe. Spika, nami kabla ya kujibu swali naomba niungane na wewe niwakaribishe vijana wetu waliokuja kutembelea katika ukumbi huu wao pamoja na walimu wao na niwatakie masomo mema na mafanikio makubwa katika maisha yao. Baada ya maelezo hayo mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 107 lenye vifungu 'a' na 'b' kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, ni kweli ukilinganisha na zamani tumepiga hatua kubwa katika kuliimarisha Jeshi la Polisi ikiwemo uweledi, vifaa majengo, mavazi, nidhamu na kadhalika. Na moja katika changamoto kubwa ya Jeshi la Polisi ni kupambana na uhalifu, lakini ifahamike suala la uhalifui ni changamoto sio hapa kwetu tu bali hata nchi nyingi duniani zinapambana na tatizo hili, maana sio rahisi kuondoa uhalifu kwa asilimia mia moja (100%). Hata hivyo, Jeshi la Polisi limefanya kazi kubwa ya kupambana na uhalifu nchini na jitihada za kazi hiyo zinaonekana nchi nzima. Aidha, Vyuo vya Polisi vimeimarishwa ili kutoa taaluma ya juu ya kipolisi katika ngazi mbali mbali ikiwemo shahada ya Chuo Kikuu ya Sayansi ya Polisi iitwayo "*Bachelor in Applied Enforcement"* na licha ya hatua hizo pia tunapeleka askari wetu kwa masomo ya ziada katika nchi za nje zikiwemo: Marekani Misri, India, Botswana, China na kadhalika.

b) Mhe. Spika, serikali hulipatia Jeshi la Polisi vifaa mbali mbali vikiwemo vifaa vya uchunguzi wa dawa za kulevya, vifaa vya uchunguzi wa silaha, pamoja na magari, makaazi, mafunzo na kadhalika kwa kadiri ya bajeti inavyoruhusu.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Ahsante Mhe Spika, kwa kuwa swali langu la msingi niliuliza kwamba ufanisi wa Jeshi la Polisi na hata semina tuliyopewa na *IGP* karibuni ilitueleza hivyo kwamba ufanisi wa Jeshi la Polisi hupatikana pale kunapokuwa na *diffusion of criminal offences.*

(a) Je, kwa sababu hivi sasa Tanzania hizi *Criminal Offences* zimekuwa kubwa, kwa mfano hivi juzi Arusha kumetokea mambo kadhaa mpaka watu kupoteza maisha kule. Na hivi juzi hapa Kamishna wetu Zanzibar alikamata silaha nyingi hapa mjini kama miezi miwili iliyopita, silaha za bunduki, za moto, maninja yale tuliona kwenye Televisheni Zanzibar. Kwa hivyo, kunakuwa na uongezeko mkubwa wa *criminal offences with in both Main Land* na hapa Zanzibar. Je, tuseme kwa *definition* ile ni kwamba Jeshi letu la Polisi kesi hizi za *criminal* zimeongezeka ni kwamba hawana uwezo wa kufanya kazi.

(b) Hivi vifaa mlivyowapatia ili kukabiliana na mambo haya havifanyi kazi vizuri au ni vibovu, au wamenunua vifaa vilivyokuwa sio vya kileo vinavyoendana na ulimwengu huu wa sayansi na teknolojia, ni vile vile vifaa vya *analogue* ambavyo wanashindwa ku-*detect* hizo *criminal offence*.

(c) Kwa kufanya hivyo, ikiwa wamenunua vifaa vya zamani si uharibifu wa fedha za walipa kodi wa nchi hii ambao sisi ni watetezi wake.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Spika, kwanza niseme na napenda nirudie sana kusema hili, kwamba Waheshimiwa wanapotuuliza maswali hasa ya nyongeza wazungumze na spika hii, vyenginevyo inakuwa tabu kuwafahamu na inakuwa si vizuri kila mara kumwambia Mheshimiwa rudia, rudia. Lakini nitajitahidi kadiri nilivyosikia niweze kujibu.

Mhe. Spika, kama nilivyosema katika swali langu la msingi kwamba tatizo la uhalifu ni moja katika changamoto kubwa hapa nchini na sio nchi yetu tu ulimwengu mzima. Na kwa vyovyote vile kwa hali ya ulimwengu wa leo ya utandawazi, sayansi na teknolojia kwa vyovyote itavyokuwa na uhalifu nao unakua kwa kiwango hicho hicho. Vile vile kutokana na idadi ya kuongezeka kwa watu katika nchi yetu na ulimwenguni vile vile inasababisha kuongezeka pia na uhalifu. Kwa hivyo, juu ya jitihada zinazochukuliwa bado uhalifu kweli upo na wakati mwengine uhalifu mwengine unapelekea mpaka kupoteza maisha ya watu.

Lakini Mhe. Spika, na mambo mengine haya yanayopelekea kupoteza maisha ya watu inafaa na sisi viongozi wa siasa kuwa waangalifu sana, maana wakati mwengine tunaimba nyimbo ambazo tunazidi kuchochea mambo hayo yatokee. Kwa hivyo, ni wajibu wetu sote kwa pamoja kuhakikisha kwamba tunahubiri mazuri viongozi wa siasa, viongozi wa dini na wananchi wote.

Mhe. Spika, lakini kubwa zaidi ni kwa wananchi wote kuwa tayari kushirikiana na Jeshi la Polisi kwa kutoa taarifa mbali mbali pale wanapoona ishara ya uhalifu. Ni kweli ulimwengu wa leo unahitaji vifaa vya kisasa zaidi na kutokana na uwezo wetu wa kifedha hatuwezi kununua vifaa vyote kwa wakati mmoja, lakini serikali inachukua jitihada kadiri ya uwezo unaowezekana kununua vifaa hivyo. Bado jeshi letu linahitaji kuwa na vifaa zaidi na ndio maana Jeshi la Polisi limebuni mbinu ya maboresho katika Jeshi la Polisi kwa nia ya kuimarisha uweledi, kwa nia ya kuimarisha vifaa, kwa nia ya kuimarisha makaazi ya askari katika kambi za polisi nchini.

Mhe. Spika, kwa maana hiyo basi, jitihada za ushirikiano sisi viongozi, raia na wananchi wote tuelewe kwamba kazi ya kupambana na uhalifu ni kazi ya kila mmoja wetu, na kadiri tutakavyopunguza kutoa taarifa au kulegeza kamba basi tujue kwamba uhalifu unaweza kuongezeka nchini. Kwa hivyo, kwa pamoja tushirikiane kupambana na uhalifu. Ahsante Mhe. Spika.

**Mhe. Shadya Mohammed Suleiman:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipatia nafasi hii ya kuweza kumuuliza mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Kwa kuwa moja katika nidhamu ya Jeshi la Polisi ni kukaa katika makambi yao.

Je, serikali inachukua juhudi gani za kuwapatia makaazi askari hao.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Spika, katika mpango wa Jeshi la Polisi kwa maboresho katika Jeshi hilo kama nilivyosema wakati nikijibu swali la nyongeza la Mhe. Saleh Nassor kuwa moja katika jitihada ni kuimarisha makaazi ya polisi. Tunaelewa kabisa kwamba kwa askari kukaa uraiani sio jambo la busara, sio nidhamu ya kiuaskari. Lakini ni uwezo wetu wa kifedha

na hali yetu ya kiuchumi ndio inayotusababisha hatuwezi kumudu kwa askari wote kuwa waweze kukaa katika makaazi ya kiaskari katika makambi yao.

Hata hivyo, jitihada zinaanza kuchukuliwa na serikali na zimechukuliwa muda mrefu kidogo kuhakikisha kwamba tunajenga nyumba za askari kwa kadiri ya uwezo wetu unavyotuwezesha. Hatua mbali mbali zimeanza kujengwa katika mikoa mbali mbali ikiwemo ya Tanzania Bara, hapa Unguja pia na Pemba. Jitihada hizo zimepewa msukumo maalum katika Jeshi la Polisi ili kuhakikisha kwamba askari wetu wanaweza kukaa katika makambi yao kila askari asikae tena uraiani.

**Mhe. Salim Abdalla Hamad:** Mhe. Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Mhe. Spika, kwa sababu Zanzibar ni nchi ndogo sana inayozungukwa na bahari ambayo watu wanaingia bila ya kizuizi, wawe Watanzania na waliokuwa si Watanzania, na baada ya kufika hapa hapana utaratibu zaidi ya kuripoti kwa balozi kujua vitu anavyokujanavyo. Na kwa sababu Wazanzibari wote hakuna mmoja anayeruhusiwa kumiliki silaha majumbani.

(a) Hatuoni kuwa kwanba uhalifu huu wa kutumia silaha ni silaha ambazo zinatoka nje ya Zanzibar.
(b) Ili tujilinde zaidi kuliko Mhe. Waziri alivyoelekeza, si bora sasa serikali ikae kwa utaratibu maalum wa kujua watu wanaoingia na wanavyoingia ili kupunguza uhalifu huu.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Spika, ni kweli serikali yetu hairuhusu kwa raia wa kawaida kumiliki silaha na vile vile hairuhusiwi kuingiza silaha nchini. Lakini vile vile kama alivyosema Mheshimiwa kwamba nchi yetu ni visiwa vimezunguukwa na bahari, na yeye akatushauri tuwe na utaratibu maalum wa kuhakikisha watu wanaoingia nchini wanapekuliwa, wanadhibitiwa kwa njia moja au nyengine ili kuhakikisha kwamba watu wote wanaoingia hapa wawe wameingia bila ya silaha.

Mhe. Spika, utaratibu upo wa uingiaji nchini, watu hawaingii kiholela, ijapokuwa kuna ndugu zetu wanaotokea Tanzania Bara wanaruhusiwa

kuingia nchini bila ya *passport* lakini upekuzi wa mizigo mbali mbali unakuwepo katika bandari zetu. Na hasa pale zinapotokea taarifa za awali zinazoonesha kwamba kuna silaha au bidhaa fulani inayoingia nchini kinyume na sheria. Kwa hivyo, uchunguzi huzidishwa, upelelezi huzidishwa kwa nia ya kuwatambua wahalifu.

Lakini Mhe. Spika, kama nilivyosema katika majibu yangu ya awali kuwa ulimwengu wa leo ni wa sayansi na teknolojia na wahalifu nao wanatumia hizo hizo sayansi na teknolojia.

Vile vile kwa kuwa tumezungukwa na bahari *tabaan* mbinu mbali mbali zinaweza kutumika watu kuingiza silaha nchini. Kitu cha msingi nilichokisema Mhe. Spika, ni kwetu sote kushirikiana katika kupambana na masuala mazima ya uhalifu ikiwemo uingiaji wa silaha hizi haramu kwa sababu ni hatari yetu sote.

Naamini Mhe. Spika, kama watu watatoa taarifa kwa sababu hakuna mtu yeyote atayeweza kuingia nchini hapa bila ya kupata muhusika anayemsaidia au kumpokea, hawezi tu mhalifu kutoka pahala popote pale akafanya uhalifu bila ya kuwa na *contact* fulani katika nchi yetu. Kwa msingi huo, narudia tena tutoe taarifa ili kujiepusha na uhalifu ambao unaweza kutuathiri sote wananchi.

**Nam. 143**

**Dawa za Kulevya Uwanja wa Ndege Zanzibar**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub -** Aliuliza:-

Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume unadaiwa kutumia sana kwa kusafirisha na uingizaji wa dawa za kulevya visiwani Zanzibar.

(a) Kwa nini wasafirishaji wa dawa za kulevya wamekuwa wakikamatwa tayari wakiwa katika chumba cha kuondokea baada ya kukaguliwa mzigo na kuruhusiwa.

(b) Kwa nini Askari Polisi wametengwa kushiriki katika ukaguzi wa mizigo kwa kutumia mashine wakati wao ndio wenye ujuzi wa mambo ya ulinzi na usalama.

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais -** Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 143 lenye vifungu 'a' na 'b' kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwa mujibu wa taratibu za Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar hairuhusiwi mtu mwengine ambaye si muhusika wa mamlaka au wa kitengo cha ukaguzi wa mamlaka kufanya upekuzi na ukaguzi wa mizigo na abiria katika viwanja hivyo kwa safari zao. Sababu zinazopelekea kukamatwa watuhumiwa baada ya ukaguzi katika viwanja vya ndege ni hizi zifuatazo:-

Mashine zinazotumiwa na mamlaka hiyo hazina uwezo wa kugundua na kutambua dawa za kulevya ila hugundua vifaa vya hatari kama vile visu, silaha, mabomu na vitu vya aina ya mripuko. Kazi ya kumkamata mtuhumiwa wa dawa za kulevya inahitaji uangalifu na mbinu za hali ya juu sana za kiintelejinsia ambazo zinazingatia na kufuata taratibu na sheria zote za kumkamata ama kumzuia mtuhumiwa.

Katika hatua za awali na kwa mujibu wa taratibu walizojiwekea mamlaka Askari Polisi ambao ndio wataalamu wa ukaguzi na utambuzi wa dawa za kulevya hawaruhusiwi na mamlaka kushiriki katika zoezi la awali la ukaguzi wa mizigo na abiria. Hivyo basi, askari hulazimika kukagua mizigo ambayo imeshaingizwa ndani ya uwanja kwa kutumia mbwa maalum au kwa kumpekuwa mtu ambaye wamepata taarifa za kiintelejinsia za kumtilia mashaka juu ya kusafirisha dawa za kulevya. Hii ndio sababu watuhumiwa hukamatwa wakiwa ndani ya chumba cha kusafiria.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa amekiri kwamba vyombo vinavyotumika vinachunguza mambo ya vyuma vyuma tu, kama bastola, visu na mambo mengine madogo madogo lakini haya mambo yaliyokuwa si ya vyuma haviwezi

kuchunguza. Kwa kuwa sasa suala hili la usafirishaji wa dawa za kulevya limeshamiri na ni *International issue.*

Haoni kwamba sasa kuna haja ya viwanja vyetu vya ndege vya Zanzibar kuleta sheria hapa Barazani tukawaruhusu wataalamu katika masuala haya ya kuweza kupekua na kuchunguza kutoka katika Jeshi letu la Polisi wakashiriki katika hilo. Hamuoni kwamba sasa kuna haja sisi Watanzania kuleta sheria hiyo hapa Barazani kwamba ikiwa sheria hairuhusu askari kupekua basi sasa tulete sheria wapekue kwa sababu lishakuwa tatizo nyeti hapa. Hilo la kwanza.

Pili, ikiwa kuleta sheria hiyo itakuwa ni tatizo anaonaje yeye kwa kushirikiana na Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano wakaweza kupeleka hawa wataalamu hawa vijana wetu wa mawasiliano katika taaluma hii ya intelijensia japo kama si askari, lakini wafundishwe juu ya uchunguzi na upekuzi wa mizigo ili kuweza kupatikana zile *initial information* ya dawa za kulevya. Hamuoni kwamba mkafanya busara hiyo mkawapeleka watu wa mawasiliano kusomea mambo hayo.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:** Mhe. Spika, ni kweli kwa mujibu wa maelezo ambayo nimeyaeleza hapa iko haja inaonekana ya kuwashirikisha Jeshi la Polisi ambao ndio wenye utaalamu wa kuweza kushiriki katika ukaguzi katika hatua za awali.

Kwa kweli Mhe. Spika, Jeshi la Polisi, Ulinzi na Forodha katika uwanja wa ndege wanatakiwa na inapaswa kufanya kazi kwa mashirikiano kama inavyoelezwa katika sheria za usalama wa usafiri wa anga wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 2011 ambayo inaeleza kuwa, ni lazima kuwepo *coordination of activities between organization.*

Mhe. Spika, naomba suala hili tulichukue kwa mazingatio zaidi, kwa sababu sheria tayari ipo inayoeleza kwamba lazima kazi hizi zifanyike kwa *coordination*. Ni wajibu wetu sisi kama serikali kuweza kuzungumza na vyombo vilivyopo hapa ili *coordination* ya pamoja ifanyike hata katika hatua za awali kama tunaweza kuwabaini wahalifu waweze kubainika kabla hawajaingia katika sehemu ya kusafiria.

**Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Nakushukuru sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba niweke sawa kitu kidogo na kuongezea katika lile alilojibu.

Kiukweli kwa uchunguzi wa mwanzo kwa mujibu wa sheria za usafiri wa anga wanatakiwa wawe wafanyakazi wa Uwanja wa Ndege, hio ndio sheria ya kimataifa. Kwa hivyo, suala ni kuwasomesha na kuwapa mafunzo zaidi ambalo hilo linafanyika.

Pili, ushirikiano upo na mambo yote yanayofanyika katika Uwanja wa Ndege vitengo vyote vya usalama wakiwemo Jeshi la Polisi limo hata katika bodi ya uwanja wa ndege wanashirikishwa ili kuona kwamba hali inakwenda katika mashirikiano ya kiusalama. Ahsante sana.

**Mhe. Asha Bakari Makame:** Ahsante sana Mhe. Spika, kabla ya yote nichukue nafasi hii nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha siku hii ya leo kuweko hapa katika hali ya usalama na afya.

Mhe. Spika, kwa kuwa Zanzibar kimaumbile yake ni visiwa ambapo Kisiwa cha Unguja na cha Pemba, na aghlabu visiwa ni mtiririko wa kupita mambo mengi. Je, Mhe. Waziri haoni kwamba kuna haja ya kubadilika ili ile *airport* ya Pemba ikakamilishiwa mambo yote ya kudhibiti uhalifu wa aina yoyote.

Pili, kaeleza hapa kwamba askari hao wanafichua mambo ya mabomu na kadhalika, haoni yeye kwamba dawa za kulevya ni bomu kuliko bomu jengine lolote lile.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:** Mhe. Spika, imeelezwa hapa wakati linajibiwa swali la kwanza na Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwamba Jeshi la Polisi limo katika kufanyiwa marekebisho makubwa na kuwezeshwa kivifaa kuona kwamba linakuwa katika hali ya kuweza kupambana na uhalifu zaidi. Ni imani yangu kwamba gati hiyo ambayo ameizungumzia nayo imo katika mpango wa kuwekewa vifaa na miundombinu ya kuweza kuzingatia uhalifu.

Swali lake la pili Mhe. Mjumbe, Mhe. Spika, mimi nafahamu sana kwamba dawa za kulevya ni hatari na madhara yake katika jamii ni makubwa. Nilichoeleza katika jibu langu mama ni kwamba mashine zilizopo katika uwanja wa ndege hazina uwezo wa kuzitambua na kuzibainisha kama mtu ametia dawa hizo ndani ya mzigo wake.

Hilo ndilo jibu ambalo nimejibu isipokuwa mashine hizo zina uwezo wa kutambua mashine ambavyo vinaonekana sio kwamba dawa hazina madhara au sio kitu kibaya. Lakini mashine yenyewe kwa *nature* yake zilivyo tumeambiwa kwamba hazina uwezo wa kusema kwamba ndani ya mzigo sasa kuna dawa za kulevya.

**Nam. 77**

**Ajira ya Walimu Unguja na Pemba**

**Mhe. Saleh Nassor Juma-** Aliuliza**:-**

Kuna taarifa kuwa Wizara ya Elimu imepata kibali kutoka Utumishi Serikalini cha kuajiri walimu katika skuli zetu za Unguja na Pemba.

(a) Katika zoezi hilo ni walimu wangapi wameajiriwa.

(b) Ni wangapi wameajiriwa Pemba na wangapi wameajiriwa Unguja wakiwa na kiwango gani cha elimu

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali.Alijibu:-**

Mhe. Spika**,** kwa idhini yako, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 77 lenye sehemu (a), na (b).

Ni kweli kuwa Wizara yangu imepata kibali cha kuajiri walimu mbali mbali wa ngazi ya cheti, stashahada na shahada ya ualimu kutoka Tume ya Utumishi Serikalini kwa ajili ya skuli mbali mbali za Unguja na Pemba. Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi kama hivi ifuatavyo:-

a) Katika mwaka 2012/2013, na hapa Mhe. Spika, naomba nifanye marekebisho kwa idhini yako katika *paper*

ambayo unayo wewe ni 338 lakini baada ya ajira tumepata hivi karibuni tu 429.

b) Idadi ya walimu walioajiriwa kwa skuli za Unguja ni 276, kati yao walimu 49 wana shahada ya Sayansi, 61 shahada ya sanaa, 15 stashahada ya sayansi, 128 stashahada ya sanaa na 23 ni walimu wenye cheti cha ualimu.

Kwa upande wa Pemba, idadi ya walimu walioajiriwa Pemba na hapa pia Mhe. Spika, naomba nitoe marekebisho kutoka 108, mpaka 153. Kati ya walimu hao 39 wamehimu stashahada ya ualimu wa Sayansi 22 wana stashahada ya ualimu wa sanaa 29 wana stashahada ya ualimu wa Sayansi na 56 wana stashahada ya ualimu wa sanaa na 6 wana cheti cha ualimu na 1 ana stashahada ya Uzamili. Pia Mhe. Spika, wizara yangu imepata kibali cha kuajiri 150 wa ngazi ya cheti kwa skuli za mikoa 4, nayo ni Mikoa ya Kaskazini na Kusini Unguja na Pemba. Hakuna walimu wa ngazi hii watakaoajiriwa kwa skuli za Mkoa Mjini/Magharibi. Kati ya hao walimu 75 wataajiriwa na kupangiwa kazi katika skuli za Unguja na idadi kama hiyo Pemba. Taratibu za Uajiri wa walimu hao wa cheti zinaendelea na wanatarajiwa wataajiriwa kabla ya kumaliza kwa mwezi wa Julai 2013 nakushukuru Mhe. Spika.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri naomba niulize suali dogo la nyongeza kama ifuatavyo:

Kwa kuwa Mhe. Spika masomo ya Sayansi imekuwa ni kilio cha nchi nzima, na kwa kuwa amesema kwa kiasi fulani kuna walimu wa Sayansi katika ngazi za Digirii na Diploma ambao wameajiriwa miongoni mwa walimu waliajiriwa wa Sayansi kwa kiasi fulani. Sasa suala linakuja hapa Mhe. Spika, Je, ni walimu wangapi wa Sayansi umewagawa katika Mkoa wa Kusini Pemba, Kaskazini Pemba, Kusini Unguja na Kaskazini Unguja pamoja na huu Mkoa wetu wa Mjini Magharibi. Ni mgao wa aina gani uliotoa wa walimu hawa wa Sayansi kwa sababu ni kilio cha kila pembe ya nchi hii.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Spika, kama ambavyo nilizungumza katika swali langu mama. Siwezi kumwambia Wilaya gani imepata ngapi na Wilaya gani imepata ngapi kwa sasa. Lakini idadi hiyo ipo na nitampelekea kwa maandishi. Lakini hawa walimu wa ziada ambazo niliwataja 45 ambao hawako katika *paper* yako wewe. Hii ilikuwa ni hususan kwa Pemba kwa sababu tuliona katika ile ajira ambayo tuliifanya Pemba hawakujitokeza walimu wa Sayansi. Kwa hivyo tukatoa tena kuomba kile kibali tukapewa na Wizara ya Utumishi tukaajiri hawa 45 kwa Skuli za Pemba. Lakini kiidadi ya kila Wilaya ni walimu wangapi ambao wamepata hiyo naomba Mhe. Spika, nitamletea kwa maandishi kwa Unguja na Pemba.

**Mhe. Ali Abdalla Ali:** Ahsante Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza:-

Mhe. Waziri kasema katika majibu yake kwamba Walimu wa vyeti kwa Unguja wamepata fursa 23 tu na Pemba 6 wengi waliochukuliwa ni wa fani ya stashahada.

(a) Anajua kwamba hivi sasa kuna walimu zaidi ya 2000 wa vyeti hawajaajiriwa Je, kwa utaratibu huu wataajiriwa lini ili wamalizike.

(b) Amesema Mkoa wa Mjini hakuna walimu watakaoajiriwa na mimi nina Skuli zangu mbili zina ukosefu wa walimu. Skuli ya Mwache Alale ina upungufu wa walimu 8 na tumeomba na Skuli ya Tasaf Kama walimu 7 na tumeomba. Je, walimu watasomesha vipi na upungufu kama huo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:**

**(a)** Mhe. Spika, nafahamu kama alivyosema kama kuna walimu karibu 2000 wa toka mwaka 2007 ambao hawajaajiriwa wa Cheti, hilo nalifahamu. Mhe. Spika, kwa kufahamu hilo Wizara ya Utumishi hivi karibuni wametupa ajira ya walimu wa cheti tu 150 ambao hawa 150 tumewagawa katika makundi mawili 75 tutapeleka Pemba na 75 tutapeleka Unguja.

(b) Kama katika mgao huu hatutatoa kwa Skuli za Mjini na Mgharibi Mhe. Spika, ni kweli hata katika huu mgao wa walimu 429 ambao tuliajiri basi Mkoa wake yeye walisema hawataki walimu wowote isipokuwa walimu wa cheti na walimu ambao tuliwapelekea kama hao muwaajiri waliwarudisha wakasema wao matatizo yao ni walimu wa cheti tu.

**Mhe. Mwanaidi Kasim Mussa:** Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza:

Kwa vile Zanzibar kuna upungufu mkubwa wa walimu wa Sayansi. Je, hao walimu walioajiriwa kwenye Sayansi wanatosheleza na kama hawatoshelezi. Je, wizara imejipangaje?

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Spika, walimu wa Sayansi ambao tumeajiri hawatoshi na suala hili kama ninavyozungumza siku zote hapa si kwa ajili ya Zanzibar tu. Mhe. Spika, tatizo la walimu wa Sayansi ni kwa Afrika nzima au niseme kwa dunia nzima. Kwa sababu humu ambamo tunakwenda kuhudhuria mikutano viongozi wetu wakuu ambapo wanakwenda Mhe. Rais, Makamu wa Kwanza, Makamu wa Pili kote wanapita huko na kujaribu kutuombea walimu wa Sayansi na pia inakuwa ni kikwazo kuwa walimu wa Sanyansi hawana.

Kwa hivyo, hilo tatizo tusione kwamba ni tatizo la Zanzibar tu ni la dunia kwa jumla. Lakini kama Wizara tumejipanga Mhe. Spika, kusomesha walimu wa Sayansi na hivi sasa SUZA imeanzisha programu maalum ili kusaidia hii ya walimu wa Sayansi wanafunzi pale wanaingia wa Sayansi. Nakushukuru Mhe. Spika.

**Nam: 104**

**Ulipaji wa Leseni kwa Wafanyabiashara ya Daladala**

**Mhe. Saleh Nassor Juma -** Aliuliza:-

Gari za Biashara ya Daladala zimeruhusiwa kufanya kazi kwa muda wa mwaka mmoja na sio kwa kipindi cha miezi sita kama ilivyofikiriwa, na uthibitisho wa hayo yamo katika leseni ya ruhusa ya njia iliyopewa gari husika. Hivyo utaratibu huo wa kulipisha mwaka mzima sio kuwadhulumu wafanyakazi hao katika maeneo mengi ya Zanzibar, hulazimika kufanya kazi kwa zamu kwa maana ya miezi sita badala ya mwaka, na kwa kuwa hutakiwa kulipa leseni ya njia (*road licence*) pamoja na gharama nyengine kwa kipindi cha mwaka mmoja na sio hiyo miezi sita wanayofanyia kazi. Na kwa kuwa wadau wa biashara hiyo wameshaomba sana bila mafanikio kufanyiwa tahafifu.

Je, kuendelea na utaratibu huo wa kuwalipisha mwaka mzima badala ya miezi sita wanayofanyia kazi si kuwadhulumu wafanyabiashara hao.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano –** Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 104 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, gari za biashara ya daladala zimeruhusiwa kufanya kazi kwa muda wa mwaka mmoja na Wizara yangu na sio miezi sita (6) kama inavyofikiriwa. Na uthibitisho wa hayo yamo katika leseni na ruhusa ya njia iliyopewa gari husika, hivyo utaratibu huo wa kuwalipisha mwaka mzima si kuwadhulumu wafanyabiashara hao lakini ni sahihi kulingana na leseni waliyopewa. Hata hivyo ningelipenda ieleweke kwamba, suala la kufanya kazi kwa miezi sita limesababishwa na wamiliki na madereva wenyewe kupanga zamu, Wizara yangu iliziruhusu gari zote kufanya kazi siku zote, lakini kutokana na wingi wa Magari na uhaba wa abiria mapato ya wafanyabiashara hao kwa siku hayakufikia hata robo ya mapato ya siku kwani Magari yalikuwa yanatembea yakiwa hayana abiria wa kutosha wakati gharama za uendeshaji hazipungui na ndio maana Kamati za ruti kuamua kujipangia zamu ili waweze kuongeza mapato na kupunguza gharama za uendeshaji.

Mhe. Spika, Wizara yangu kama mratibu wa hilo na kwa kuzingatia uhalisia wenyewe na kwa kuwa wamiliki wenyewe ndio walioamua

hayo, hatuoni sababu ya kupingana nao zaidi ya kuweka utaratibu huo wa zamu uendelee ili kuongeza tija na mapato kwa wahusika hao.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Mhe. Spika, kwanza napenda nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa jinsi anavyosema maneno sana katika kutujibu masuali yetu haya. Baada ya maelezo hayo naomba nimuulize swali la nyongeza.

Kwa kuwa yeye mwenyewe Mhe. Naibu Waziri amekiri kwamba suala la zamu wamelikubali wizara yake, na kwa kuwa dereva wa daladala Mhe. Spika, anapotoka siku ambapo si zamu yake wanamkamata na kumpeleka polisi na kumfungulia kesi Mahakamani kwamba amekwenda kazini sio siku ya zamu yake. Kwa mnasaba huo ina maana katika siku mia tatu na kidogo za kazi ambao ni mwaka mmoja anafanya siku mia moja na hamsini na wao wameshalikubali hilo.

Sasa Mhe. Spika, kumlipisha dereva wa daladala *road licence* kwa muda wa mwaka mzima kwa sababu anafanya kazi kwa nusu mwaka. Je, huko si kumnyima haki zake za msingi huko. Kwa hivyo, ni lini wizara yako Mhe. Naibu Waziri itaona haja ya kuwatendea haki hawa baada ya kuwalipisha mwaka mzima baada ya kuwalipisha nusu mwaka kwa sababu ndio siku wanazofanya kazi hawa madereva wa daladala.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Spika, nilichokieleza katika majibu mama ni kwamba sisi kama Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ruhusa yetu ya kufanya kazi ni kipindi cha mwaka mzima, wamiliki wa magari pamoja na madereva wao kwa kupitia utaratibu wao wamejiwekea malengo na hali hii inatokana na mapato wanayoyapata. Kwamba kipato wanachokipata ni kidogo mji wetu wa Zanzibar kuna zaidi ya magari 450 yanayofanya biashara ya daladala wao wenyewe wakaona kwamba magari hayo yote ukiyaingiza kwenye soko kwa siku moja tija itakayopatikana ni kidogo. Kwa msingi huo wamekubaliana kwamba ifanye kazi leo kesho itulie keshokutwa inafanya kazi tena.

Na sisi kama ni Serikali hatuna utaratibu wa kuwashtaki. Isipokuwa wao wenyewe kwa mfumo wao na utaratibu wao ndio wamekuwa wakichukuliana hatua zinazostahiki ikiwa pamoja na kuzuiana kutofanya kazi kama vile walivyokubaliana. Malengo yao ni kuongeza tija kwa zile siku ambazo wanafanya kazi. Sisi kama Serikali hatuna kikwazo, na uthibitisho wa hilo ndio zile ruhusa na vibali tunavyovitoa tunavitoa kwa kipindi cha mwaka mzima na hatutoi kibali kwa kipindi cha miezi sita.

**Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Nakushukuru sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri aliyotoa Mhe. Naibu wangu naomba niongezee kidogo nimfahamishe Mhe. Mjumbe.

Gari inapokata leseni inaruhusiwa kuchukua abiria kwa hivyo kuna vyama vya madereva ambavyo vinashughulikia na utaratibu wao na namna ya kuanga zamu hii haihusiani kabisa na ukataji wa leseni. Kama gari itapata kodi haisimamishwi njiani kwamba wewe leo si zamu yako au nini kwa sababu *road licence* yake ni ya mwaka mzima. Kwa hivyo, hakuna njia ya kuizuia gari kwa upande wetu wa wizara kwamba inakwenda kinyume na utaratibu, utaratibu wa zamu ni vyama vya madereva ambao wanaratibiana wao wenyewe kwa wenyewe na wizara haina pingamizi na jambo hilo, usalama wa barabarani unawekwa na hakuna purukushani ya kushindana.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Spika, mimi naomba nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu mazuri, lakini na mimi nina suali moja la nyongeza:

Mhe. Spika utaratibu wa kupata leseni ya njia ilikuwa ni kwenda dereva au kwenda mmiliki wa gari *ZRB* na kukata *road licence* hiyo. Kutokana na mabadiliko ya Serikali kuanzia Julai mosi mwaka huu ili upate *road licence* hiyo itategemea na lita za mafuta ambazo unaingiza kwamba lita moja sasa mmiliki wa gari atachangia shilingi 35 na ili gari itembee kwa mfano daladala imechukua watu ishirini ili ifanye kazi kwa siku maana yake ichukue lita 50. Lita 50 kwa zamu ya mwaka itagharimu laki tatu na kumi na tano elfu suala langu sasa.

Hivi sasa gari hiyo hiyo *road licence* ya njia ni shilingi elfu sabini kwa utaratibu mpya sasa itakuwa ni shilingi laki tatu na kumi na tano elfu.

Je, kwa kuwa bei ya wanafunzi kwa daladala ilikuwa ni shilingi mia mbili kwa hesabu ya sasa wanafunzi wanapaswa kulipa shilingi mia sita, na kwa kuwa wanafunzi leo pale juu wapo watashuhudia Mhe. Waziri atafanya nini ili kuwapunguzia kupitia Bodi ya Usafiri barabarani kudhibiti upandaji wa nauli za wanafunzi zile wasiathirike kama ni Wazanzibari.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Spika, ni kweli kwamba Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imebadilisha mfumo wa ulipaji na matarajio haya ni kuona namna gani Serikali itaweza kuongeza mapato lakini pia kwa kiasi gani Serikali itaweza kudhibiti uvujaji wa mapato. Malengo ya kufanya hivyo hayahusiani moja kwa moja na utaratibu wa upandishaji wa nauli za daladala.

Bado suala la upandishaji wa nauli za daladala utaendelea kuratibiwa na wizara husika Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano na hatuoni kwa kiasi chochote kwamba mfumo huo wa ulipaji *road licence* kwa kupitia mafuta kutaathiri bei za wananchi wanazotumia daladala na kwa sababu tu bei za upandaji wa gari zinazingatiwa kwa mujibu wa vikao vya Bodi na vikoa husika kuweza kuratibu. Nataka nimuhakikishie Mwakilishi kwamba hakutakuwa na athari moja kwa moja kwa vijana hawa na watumiaji wengine wa magari kwa ajili ya kupanda bei na kama kutakuwa na lolote Serikali italizingatia hilo kwa msingi unaostahiki.

**Nam. 12**

**Ulinzi katika vyanzo vya Maji**

**Mhe. Asha Abdu Haji-** Aliuliza:-

Maji ndio uhai wa viumbe vyote na ni nyenzo muhimu kwa maisha ya kila siku pasipokuwa na uangalifu endelevu na wa uhakika basi maji yanaweza kuleta balaa na mauaji kwa watu wetu.

(a) Je, kuna vyanzo vingapi vya maji hapa nchini ambavyo Serikali inavitumia kuwasambazia maji raia zake.

(b) Je, katika vyanzo hivyo, ni vyanzo vingapi vimewekewa walinzi kwa muda wote wa saa 24 za kila siku, ili kuhakikisha kuwa hakuna uharibifu au uchafuzi wa maji hayo.

(c) Je, Wizara inajiridhisha kwa kiwango gani kuwa ulinzi unafanyika kwa muda wote.

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati** - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suali lake nam.12 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Asilimia 87 ya maji safi na salama kwa Zanzibar yanatoka ardhini, ambayo yanapatikana kwa kuchimbwa visima virefu. Hadi kufikia mwishoni mwa mwaka 2012 kuna visima vya uzalishaji Maji *Production Wells* 171 nchini vinavyosimamiwa moja kwa moja na *ZAWA*. Mbali na visima vingine 444 binafsi vilivyosajiliwa rasmi ambavyo hutumiwa na watu binafsi kwa matumizi ya shughuli za kibinaadamu. Ni vigumu kujua idadi ya visivyosajiliwa kwa kuwa huchimbwa bila ya taarifa, karibu kila eneo. Aidha, kupitia kwako Mhe. Spika, nawaomba wale wote ambao bado hawajasili visima vyao wafanye haraka kuvisajili ili kutupa takwimu sahihi. Vianzio vingine ni chemchem na mapango vinavyofikia asilimia 13, vyote vinahitaji kutafitiwa kubaini idadi halisi ya maji iliopo, kabla ya uamuzi wa kuyatumia. Utaalamu uliopo hautoshelezi kuainisha kima halisi cha rasilimali hiyo chini ya ardhi, hali inayolazimu majaribio ya visima baada ya kuchimbwa *pumping test* kujua iwapo wingi wake unakidhi mahitaji. Katika hilo, tunahitaji tuwe na wataalamu ama kutoka nje ya nchi au hapa nchini. Ukosefu wa kubaini kima cha maji husababisha baadhi ya visima hatimaye kutoa maji ya chumvi, hali inayorejesha nyuma juhudi zilizokwishafikiwa katika baadhi ya maeneo.

(b) Mhe. Spika, ili kuhakikisha kuwa hakuna uharibifu au uchafuzi wa maji, Wizara imeweka walinzi wa kawaida

wafanyakazi kwa vituo vidogo vidogo na askari wa vikosi vya SMZ kwa masaa 14 kwa vituo vikubwa vya Mwanyanya, Mtopepo, Saateni matangi ya maji na Welezo matangi ya maji.

(c) Mhe. Spika, Wizara yangu bado haijaridhika na kiwango hicho cha ulinzi, lakini Wizara kupitia Mamlaka ya Maji inaendelea na mazungumzo na vikosi vya SMZ ili kuhakikisha kwamba vituo vyote vinakuwa na ulinzi kwa masaa 24.

**Mhe. Marina Joel Thomas:** Mhe. Spika, kuweka uzio katika vyanzo vya maji ni umuhimu sana unasaidia kuepusha na uvamizi katika maeneo hayo.
Naomba kumuuliza Mhe. Waziri je, vianzio vingapi vya maji vimewekwa uzio kwa hapa Unguja.

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Spika, hadi sasa tumeweka uzio katika visima maeneo makubwa kama Mwanyanya, Mto Pepo pamoja na Welezo na sehemu nyengine tunaendelea na tuko katika progamu hiyo ya kila kisima cha maji kuweka uzio tunapata tatizo na kila tatizo tunalolipata ni kwamba baadhi ya watu ambao wamechimba katika mashamba yao huwa hawataki kutoa nafasi ya kutosha kwa ajili ya uzio. Baada yake husema kisima kibaki hapo hapo shamba langu niendelee kutumia. Kupitia kwako nakuomba Mhe. Spika, na Waheshimiwa Wajumbe waelimishwe watu kwamba usalama wa maji ni wetu sote. Na hakika maji hayo ndio wanayoyatumia na yakichafuka madhara yatakuwa makubwa kama nilivyosema katika swali langu la msingi.

**Mhe. Mohammed Haji Khalid:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kuwa maji yana njia zake mbali mbali na kuna baadhi ya watu ama wanajenga au kulima karibu na vianzio vya maji. Je, wizara yake ina mpango gani kwa kudhibiti jambo hili.

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Spika, nakubali kwamba kuna baadhi ya maeneo watu wanasogea katika visima vya maji kwa ujenzi. Hili si zuri na linapunguza kiwango cha maji katika kile chanzo kilichopo. Ni vizuri wananchi wakajua kwamba kusogea karibu na

chanzo cha maji kunapunguza ile geji ya maji ardhini. Kwa sababu ardhi ile maji yake hata ikinyesha mvua hayaendi chini kwa sababu ile ya kukanyanga kufanya pale maji baada yake yanateremka pwani moja kwa moja na yanakuwa hayapatikani tena.

Tunajitahidi kuwaambia kuwa watu wasijenge na tunagombana nao maana anakwambia nikakae wapi maana mimi sina pa kukaa na mimi masikini nimetafuta pesa zangu nimepata hapa najenga unaniondosha maana yake nini. Hili ndilo tunalokwenda nalo na vile vile tunajitahidi kutoa elimu hata ujumbe wetu wa asubuhi katika redio unaeleza hivyo kwamba usijenge karibu na chanzo cha maji na pia tusikate miti katika maeneo yanayopatikana maji tunatoa taaluma katika redio kila asubuhi ujumbe unasikilikana.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Spika, suala la msingi linasema maji ndio uhai wa viumbe vyote na ni nyezo muhimu kwa maisha ya kila siku. Mhe. Waziri ukizingatia huu mwezi wa Ramadhani unakaribia na wewe jina lako Ramadhan Abdalla Shaaban wananchi wa jimbo la Muyuni hasa Shehia ya Kitogani kuna baadhi wa wananchi hawapati maji, na Shehia ya Pete yote ni jimbo la Muyuni ni lini tutegemee watapata maji kabla ya Ramadhani na mimi niko tayari kushirikiana na yeye kwa hali na mali. Lakini tatizo limekuwa zito na kutokana na Mkurugenzi kutokana na majukumu mengi anayokuwa nayo ya tatizo la maji. Ni lini wananchi hawa ikiwa sasa wananisikia wategemee kupata maji.

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Spika, kuhakikisha kuwa watu wote wanapata maji ni kazi ngumu sana hasa katika mabadiliko nchini petu sasa kwamba watu hawataki kutumia visima baada yake wanatumia maji ya bomba haya tunayoyachimba katika maeneo mbali mbali. Katika maeneo ambayo yapo sugu kama Mheshimiwa tutashirikiana basi japo mara moja moja tutapeleka gari la maji liwasaidie watu katika maeneo hayo.

Hata hivyo tumejitahidi kuanzisha miradi mingi ya maji ili kupunguza kadhia ya maji katika maeneo mbali mbali naomba Mwenyezi Mungu atujaalie tufanikiwe katika miradi hii ili tukifika Septemba mwaka 2014 ili miradi iwe imekamilika na tulimalize kabisa tatizo la maji.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Kwa kuwa juzi Mhe. Spika, wakati Mhe. Waziri wa Afya Mhe. Juma Duni Haji alipokuwa anajibu swali linalohusiana na ghala ya madawa Pemba, niliuliza swali la nyongeza katika swali hilo la msingi, linalohusiana na swali hili la leo nambari 74. Kwa kuwa jibu alilojibu Mhe. Waziri limesibu jibu la swali hili la leo, na kwa kuwa anayetaka kujibu swali hili ni Mhe. Naibu Waziri wake ambaye leo yuko hapa. Kwa heshima kubwa na taadhima ya hali ya juu, namuomba leo Mhe. Naibu Waziri akajitayarishe kwa kujibu swali jengine, hili niliondoshe.

Kwa hivyo, kwa heshima kubwa naliondosha ili kumpa nafasi Dk. Sira Naibu Waziri wa Afya ajitayarishe kwa kujibu swali langu la kesho, ahsante sana Mhe. Spika.

**Nam. 74**

**Kupatiwa Usafiri wa Uhakika kwa Bohari Kuu za Dawa Unguja na Pemba**

*(Mhe. Mjumbe aliyetaka kuuliza swali hilo ameliondoa)*

## HOJA ZA SERIKALI

(*Majadiliano yanaendelea)*

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, tunakusudia kuendelea na majadiliano kwa kuwapa nafasi baadhi ya Waheshimiwa Mawaziri kumsaidia Mhe. Waziri ili hatimaye hoja hii tuimalize leo. Nategemea tutakwenda vizuri na ratiba yetu na hasa kwa kuzingatia kwamba kwa taratibu zetu za kanuni Mwezi wa Ramadhani ambao unakaribia, muda wa shughuli zetu hapa utakuwa unapungua sana na kuna hatari shughuli zetu hizi tukashindwa kuzimaliza katika muda ambao tumepangiwa.

Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe, niwaombe kama vile alivyosema Mhe. Mwenyekiti jana kwamba wale ambao watakuwa wamekosa kuchangia, ambao naomba niwataje majina basi wafanye utaratibu ili michango yao waipeleke kwa Mhe. Waziri kwa maandishi, kwa mujibu wa orodha niliyoipata hapa Waheshimiwa Wajumbe ambao hawatapata nafasi ya kuchangia ni pamoja na;

1. Mhe. Salim Abdalla Hamad
2. Mhe. Abdalla Mohamed Ali
3. Mhe. Subeit Khamis Faki
4. Mhe. Salma Mussa Bilali
5. Mhe. Mgeni Hassan Juma
6. Mhe. Panya Ali Abdalla

Kwa hivyo, majina niliyonayo ili kumsaidia Mhe. Waziri kwa ajili ya kufanya majumuisho ni mawaziri wawili na hatimaye tumalizie na Mhe. Mwanasheria Mkuu. Kwa hivyo, mawaziri ambao wameomba kufanya hivyo ni Mhe. Mohamed Aboud Mohamed Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, karibu

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. Pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa namna ambavyo amewasilisha vizuri

hotuba yake, kaifafanua kwa kina na naamini imeeleweka vizuri na ndio maana Wajumbe wengi walipata fursa ya kuichangia.

Mhe. Spika, mimi nataka niwapongeze Mhe. Waziri na watendaji wake na wafanyakazi wote wa wizara hii kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya katika kuleta mabadiliko makubwa katika nchi yetu.

Mhe. Spika, vile vile niwashukuru Wajumbe wa Baraza hili kwa namna ambavyo wameichangia vizuri sana hotuba ya wizara hii. Mhe. Spika, nianze kwa kuwapongeza Waheshimiwa Wajumbe wote. Kwa namna walivyoichangia hotuba hii na zilizotangulia ni ishara ya wazi ya uwezo mkubwa sana walionao Wajumbe wa Baraza hili tukufu, lakini sio tu uwezo walionao katika kuchangia na uelewa, mbali namna wanavyofanya utafiti wa mambo mbali mbali wa kuhakikisha kwamba serikali ifanye wajibu wake vizuri zaidi wa kutekeleza matakwa yote ambayo yanatakiwa yatekelezwe.

**Mhe. Spika:** Hebu rekebisha hiyo simu inayotuletea tabu.

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Sio hizi zangu. Mhe. Spika, mimi simu zangu nimezifunga zote.

**Mhe. Spika:** Haya endelea.

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: N**a ushahidi huu hapa Mhe. Spika. Mhe. Spika, ni ushahidi wa wazi kwamba Wajumbe wetu hawa wamefanya utafiti mkubwa na wapo hapa kwa ajili ya kutetea maslahi ya umma.

Mara nyingi sana Mhe. Spika, maoni yao na michango yao sisi katika serikali huwa tunaifanyia kazi sana, na ni kinyume kabisa pale tunapoambiwa kuwa sio wasikivu. Nataka nikuhakikishie Mhe. Spika, mambo mengine tunayoyafanya ni kutokana na ushauri, maelekezo na mapendekezo ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu.

Mhe. Spika, katika uendeshaji wa nchi yapo mambo ya kufanywa kwa muda mfupi, yapo yanayofanywa kwa muda wa kati na yapo yanayofanywa kwa muda mrefu, kubwa zaidi ni katika kujenga misingi ili utekelezaji uwe undelevu kwa leo na kesho. Ndio maana

katika serikali tunachukua hatua mbali mbali ya kutengeneza sera na sheria. Ni mashahidi sote hapa Mhe. Spika, tumeleta sera nyingi, tumeleta sheria nyingi katika Baraza hili tukufu.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, vijana wanawaaga wanakwenda kupumzika, wapigieni makofi. Ahsante sana, Mheshimiwa endelea.

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Spika, tumeleta sheria nyingi, msingi wake na chanzo chake kinatokana na maoni ambayo Baraza hili tukufu imeyatoa.

Mhe. Spika, ningependa niseme baadhi ya sheria ambazo tumezitunga hivi karibuni kwa nia na dhana ya kutekeleza utawala bora, kwa nia na dhana ya kupambana na rushwa, kwa nia ya kuweka nidhamu ndani ya serikali na kuwa na utendaji wenye tija na ufanisi. Hivi karibuni Mhe. Spika, tulianzisha sheria ya kupambana na rushwa, tulianzisha sheria ya utumishi wa umma, tumeanzisha rasimu na tumo kwenye mchakato ya maadili ya kitaifa ili viongozi wawe na maadili mazuri. Mhe. Spika, tumefanya jitihada mbali mbali za kuhakikisha kwamba yale mengi ambayo Waheshimiwa Wajumbe wanatuelekeza tuyafanye. Tumechukua hatua ya kutoa mafunzo na midahalo mbali mbali kwa ajili ya suala zima la kupambana na rushwa. Tumeanzisha masuala ya makusudi ya kuhakikisha kwamba watendaji wetu katika sekta ya umma wanafuata maadili na kufuata taratibu na sheria zilizopo.

Lakini tunaanzisha rasimu ya mpango mkakati wa utekelezaji wa sera ya serikali ya mtandao e-*government*. Vile vile tunaimarisha miundombinu ili kutumia vyema mkonga wa mawasiliano, na tayari tumeshafunga mkataba na kampuni ya Zantel ili kuendesha mkonga huo, ili hatua zote ambazo serikali imeahidi iweze kufanya kazi.

Mhe. Spika, katika jitihada zetu hizo, inawezekana wakati mwengine sisi wenyewe tuliomo humu ndani tukashindwa kuona mafanikio makubwa tunayopiga hatua nayo, lakini wenzetu nje wanayaona. Mhe. Spika, ni juzi tu na jana Mhe. Rais wa Marekani Rais Barack Hussein Obama amesifu sana jitihada za Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Zanzibar, katika suala zima la kuimarisha utawala bora na katika suala zima la demokrasia. Haya yote Mhe. Spika, yanatokana na

mashauri ambayo Baraza hili tukufu yanatupa na uwajibikaji wa serikali katika kufanya mambo.

Ningependa niseme tu Mhe. Spika, kwamba hatua hizi zinazofanyika, zinafanyika kwa umakini na kwa utaratibu mzuri, ili yale yote ambayo Waheshimiwa wanayosema basi yaweze kuchukuliwa hatua na yaweze kufanyika vizuri. Hatuwezi kudharau hata kidogo masuala ambayo Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili wanayasema, ni wajibu wetu kuyatekeleza, lakini kutekeleza kwenyewe kunakuwa hatua kwa hatua. Ni lazima ujenge misingi imara itakayoweza kufanya jitihada hizo kuwa endelevu.

Mhe. Spika, nataka niwahakikishie Wajumbe wa Baraza lako tukufu. Misingi hii inayojengwa hakutotokea tena huko mbele watendaji wabadhirifu, wakitokea watakuwa wanaingia katika dema wenyewe moja kwa moja, kwa sababu misingi ipo na sheria zipo. Kwa hivyo, mambo yote haya tunayafanya ili uwazi uwepo na fedha za umma zisiharibiwe.

Mhe. Spika, mimi nataka nichukue nafasi hii kuipongeza sana ofisi ya *CAG*, imeanza kazi vizuri na serikali inaunga mkono sana. Kwa mara ya kwanza kabisa Mhe. Spika, nataka niseme mbele ya Baraza lako tukufu, kwamba wakati *CAG* anawasilisha ripoti zake kwa Mhe. Rais, ni kipindi hiki ambacho hazichukui muda mrefu zinakuja Baraza la Wawakilishi.

Hilo nataka niseme wazi kabisa, kipindi hiki Mhe. Spika, *CAG* anapeleka ripoti yake kwa Mhe. Rais haichukui muda mrefu inaletwa hapa Baraza la Wawakilishi na serikali itaendelea kuchukua kila jitihada kuhakikisha kwamba kazi inayofanywa na *CAG* inafanyiwa kazi vizuri ndani ya serikali. Wale wote ambao wataonekana ni wabadhirifu wamekwenda kinyume na sheria za utendaji wa kazi, serikali haitomvumilia mtu yeyote na itachukua hatua zinazofaa bila ya kumuonea mtu yeyote, haki itabidi itendeke na ndio msimamo wa serikali yetu.

Mhe. Spika, vile vile niwapongeze wenzetu hawa wa Tume ya Utumishi wa Umma. Kulikuwa na malalamiko mengi sana Mhe. Spika, kuhusu utaratibu wa ajira katika nchi yetu. Kwa kiasi kikubwa

sana tume hii imefanya kazi kubwa ya kujenga uadilifu, ya kujenga uwiano, ya kuwa wazi zaidi na taratibu zake ni nzuri zaidi kuliko ilivyokuwa awali. Sasa mwanzo ni mgumu Mhe. Spika, mapungufu ya hapa na pale yanaweza kujitokeza na ni haki yetu Wajumbe kurekebisha pale ambapo ipo kasoro na sisi ndani ya serikali hatukatai hata kidogo, tunapooneshwa makosa yetu na tunaporekebishwa makosa yetu, nia ni kuwatumikia wananchi ili wananchi wa nchi hii waishi katika maisha yaliyokuwa mazuri zaidi.

Kwa hivyo, kadiri tunavyokosolewa tunapokea, lakini tujue tu kwamba na serikali hii hailali usingizi inafanya kazi tena kwa uadilifu wa hali ya juu. Kidogo wao wanatokea kufanya makosa tusitambulikane kwamba samaki akioza mmoja ndio wameoza wote Mhe. Spika. Kwa sababu lugha nyengine ambazo zinatoka hapa ukitizama utaona kama hakuna kinachofanyika ndani ya serikali, lakini haya yote tunayoyafanya tunayafanya kwa ushauri na maelekezo ya Baraza hili.

Kwa hivyo, ni vyema kabisa pale penye makosa tukaambiwa, lakini na pale tunapofanya mema tupewe moyo ili tuzidishe jitihada za kufanya mema na huko ndiko tutakapowaweka vizuri wananchi wetu wakaelewa pia jitihada za serikali yetu.

Kwa hivyo, nataka niwahakikishie Waheshimiwa wa Baraza hili tukufu, kwamba tunashirikiana na wenzetu na haya yote tunayafanya kwa maslahi ya wananchi wetu. Tume ya Utumishi hii imefanya kazi kubwa ya kupanga taratibu nzuri kwa maslahi ya wafanyakazi wetu. Kwa mara ya kwanza katika nchi yetu Mhe. Spika, tumeona mabadiliko makubwa ya mishahara, mabadiliko makubwa ya kupata vyeo katika kazi, kujenga mazingira mazuri ndani ya kazi zetu za utumishi wa umma.

Pia hata katika sekta binafsi mabadiliko yapo na kwa jambo hili Mhe. Spika, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Rais wetu wa Zanzibar Dk. Ali Mohamed Shein, kila wakati anafikiria kuongeza mishahara ya watumishi wa umma, kadiri ya uwezo wa nchi unavyoruhusu na ndio maana tumeanza vizuri na tunaendelea vizuri. Kwa hivyo, naomba kabisa tuelewe jitihada hivi na tuziunge mkono kwa pamoja, kwani mazuri yanayofanyika nayo tuyapongeze, wasitupongeze wenzetu kutoka nje na sisi wenyewe tujipongeze kwa

hatua ambazo tunazifanya na ndio kupeana moyo wa kufanya mazuri Mhe. Spika. Mimi nataka niwahakikishie Mhe. Spika, kwamba kila linalosemwa hapa basi serikali inachukua jitihada ya kulishughulikia kwa maslahi yetu sote.

Mhe. Spika, kuna jambo moja lilijitokeza hapa kuhusu watumishi wa Baraza la Wawakilishi. Mhe. Spika, sote tuliomo humu ndani ni lazima tuwe na imani nao watumishi wetu hawa, wanafanya kazi kubwa, wanafanya kazi nzuri na wanafanya kazi kwa mashirikiano kwa pamoja. Hakuna anayependa hata kidogo itokee watumishi wetu hawa wasipate haki zao zinazostahiki, sio serikali, sio sisi Wajumbe na kila mmoja angependa kuona watumishi wetu hawa wanapata stahiki zao nzuri, ili wafanye wajibu wao vizuri.

Mhe. Spika, katika kulishughulikia tatizo hili bado serikali inasema itachukua kila jitihada kuhakikisha kwamba tatizo hili linapata ufumbuzi uliostahiki, ili watumishi wetu hawa kila kasoro ambayo imejitokeza iweze kuondoka kadiri ya uwezo wa hali ya uwezo wa nchi yetu.

Jambo hili pia lilizungumzwa Mhe. Spika, wakati tunazungumza katika hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, wakati tukijadili na kupitisha kifungu cha Idara ya Uratibu, jambo hili pia lilizungumzwa. Kwa sababu Mhe. Spika, kanuni zetu katika kifungu 91(d) kinaeleza wazi kwamba jambo ambalo limezungumzwa na likapata ufumbuzi wa pamoja, basi sio vyema tuwe tunarudia rudia. Kwa kuwa tumekubaliana kwamba jambo hili liendelee kushughulikiwa na serikali.

Ningependa nirudie tena kulitaarifu Baraza lako tukufu kwamba jambo hili tutalizungumza lipate ufumbuzi muafaka ili watendaji wetu wapate kila haki yao. Lakini tuelewe kwamba mambo yote haya yanakwenda hatua kwa hatua, hakuna jambo ambalo linaweza kumalizika kwa siku moja.

Mimi naamini madamu tumelizungumza na serikali inachukua ahadi mbele yenu Wajumbe kwamba jambo hili litapata ufumbuzi. Kwa hivyo, nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu

tukubaliane na hoja ya serikali kwa sababu jambo hili tumelizungumza na serikali imekubali kulichukua na kulitafutia ufumbuzi wake.

Mhe. Spika, baada ya maelezo haya na mimi niseme naunga mkono hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa asilimia mia moja. Niwaombe na Waheshimiwa Wajumbe wenzangu wote tuunge mkono kwa asilimia mia moja ili tuwawezeshe wizara hii na watendaji wake waweze kufanya wajibu wao vizuri wa kuwahudumia wananchi wetu pamoja na watumishi wetu katika sekta ya umma na sekta binafsi. Baada ya hayo Mhe. Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi).*

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, ilikuwa ni nafasi ya Mhe. Mwanasheria Mkuu lakini simuoni, lakini nafikiri aliyoyazungumza Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ndio mambo ambayo nategemea na Mwanasheria Mkuu angeyazungumza. Sasa kwa kuwa hayupo basi naomba moja kwa moja kumkaribisha Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ili kuja kufanya majumuisho.

Wakati Mhe. Waziri anafanya majumuisho ningewaomba Waheshimiwa Wajumbe wakaingia ndani ili wakasikia kile ambacho Waziri anafanya majumuisho ambayo ni pamoja na yale ambayo Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ameyazungumza hivi punde. Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora karibu sana. *(Makofi).*

Naona makofi mnayapiga kwa woga, mpigieni makofi basi. *(Makofi/Vicheko).*

Enhee. Mhe. Waziri, karibu.

**3/07/2013**

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora:** Mhe. Spika, awali ya yote naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa kunijaalia afya njema na kuwajaaliwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, kwa pamoja kutuwezesha kuwa na afya njema ya kuweza kuwatumikia wananchi wetu wa Zanzibar waliotutuma.

Mhe. Spika, nimuombe Mwenyezi Mungu anizidishie busara, hekima na ujasiri wa kuweza kutoa ufafanuzi. Tafsiri yangu ni ufafanuzi sio majibu, kwa hivyo ufafanuzi mara nyingi sana huwa unaelekea katika kueleza uhalisia wa mambo. Kwa hivyo, nitamuomba Mwenyezi Mungu anizidishie hivyo.

Tokea jana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nikwambie kwamba nilikuwa nikipokea *message* na simu nyingi sana, ambazo zinanitakia kheri kwa Mwenyezi Mungu anijaalie niweze kulimaliza tatizo hili kwa hekima na busara na uaminifu mkubwa. Nawashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Tumbatu kwa mashirikiano yao waliyoyazidisha kuanzia jana mchana mpaka leo asubuhi, nawaahidi kwamba walichonitaka nitakifanya na sitowaangusha, sitochukua jazba ya kuweza kujibu maswali kama vile pengine ilivyotarajiwa nifanye hivyo. Mwenyezi Mungu niwezeshe kufanya hayo.

Mhe. Spika, nichukue nafasi hii kukushukuru pia kwa kunipa nafasi hii ya kuja kufanya ufafanuzi. Lakini nimshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein kwa kuniamini na kuniongoza katika kutekeleza majukumu yangu aliyonikabidhi kwa madhumuni ya kuwatumikia wananchi.

Mhe. Spika, hotuba yangu ya bajeti imechangiwa na wachangiaji 21, wachangiaji 18 wamechangia kwa kusema na wachangiaji 3 wamechangia kwa maandishi. Niwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe kwa kutumia demokrasia yao na kutekeleza majukumu yao ipasavyo, katika kuihoji serikali na kuisimamia serikali juu ya hoja ambayo imesimamiwa mbele yao, niwashukuru sana na wao Mwenyezi Mungu atawapa neema kwa kazi ambayo wanaifanya. *(Makofi).*

Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe wenyewe ni kama hivi ifuatavyo.

1. Mhe. Ussi Jecha Simai, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba Sheria na Utawala.
2. Mhe. Fatma Mbarouk Said, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya (PAC)
3. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
4. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
5. Mhe. Wanu Hafidh Ameir
6. Mhe Asha Abdu Haji
7. Mhe. Mohamed Mbwana Hamad
8. Mhe. Asha Bakari Makame
9. Mhe. Mohamed Haji Khalid
10. Mhe. Marina Joel Thomas
11. Mhe. Salmin Awadh Salmin
12. Mhe. Hija Hassan Hija
13. Mhe. Hamza Hassan Juma
14. Mhe. Bikame Yussuf Hamad
15. Mhe. Mbarouk Wadi Mussa
16. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
17. Mhe. Suleiman Hemed Khamis
18. Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais

Waliochangia kwa maandishi ni;

19. Mhe. Kazija Khamis Kona
20. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman
21. Mhe. Farida Amour Mohamed

Mhe. Spika, nataka hawa wote niwashukuru kwa michango yao ambayo wamechangia jana na wengine kumalizia leo, kwa kutumia fursa ya kuisimamia na kuikosoa serikali ndani ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, mimi naelewa kwamba mimi nawajibika katika Baraza hili kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar, na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wanafanya kazi hiyo kwa kupitia Katiba hii pia. Kwa hivyo, niwapongeze na wala hakuna la ajabu katika utaratibu wa Kimabunge na Mabaraza kupata *challenges* za hoja katika

uendeshaji wa shughuli zetu Mhe. Spika za Kibaraza au Kibunge, yaani kwa mujibu wa taratibu za Mabunge ya Jumuia ya Madola.

Mhe. Spika, nataka nianze na lile ambalo Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais amelizungumza na mutaniwiya radhi sitamtaja Mjumbe mmoja mmoja waliochangia hili. Kwa hivyo, wengi kati ya Wajumbe waliochangia wameligusia hili juu ya suala zima la maslahi ya watumishi wa Baraza la Wawakilishi, lakini hawakuishia hapo pia walizungumzia suala la maslahi ya watumishi wa taasisi nyengine zinazolingana kwa umuhimu wake na kwa kuzingatia ujuzi na umuhimu wa taasisi zenyewe.

Kwa mfano, Ofisi ya *DPP*, Ofisi ya *AG*, Mahakama, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi pamoja na Chuo cha Utawala wa Umma. Lakini hizo ni sehemu tu ya taasisi za serikali ambazo Wajumbe wako Mhe. Spika wameona kwamba kuna umuhimu wa kuzingatia maslahi ya watumishi wake.

Mifano hiyo ikazungumzwa sana na niwaombe Waheshimiwa Wawakilishi kupitia kwako Mhe. Spika, kusema utamaduni tuliojijengea kule kwetu Tumbatu. Kwa mfano, kule kwetu Tumbatu akimtaja mwenzio mtu mzima ukisema mtoto huyu masikini, basi watu walio karibu watakufuata wakwambie usimuombee dua hiyo, lakini ukimuombea mtoto, kwamba Mwenyezi Mungu mtoto huyu awe mfalme, rais, apate elimu ya dunia na akhera, basi wanakuombea dua na wewe kutokana na kumtakia mema yule mtoto.

Mhe. Spika, katika hili imezungumzwa sana Kamisheni ya Utumishi wa Umma na mimi sitaki niingie kabisa kwenye vifungu vya Sheria wala Katiba. Lakini nataka niseme kwamba kilichoandikwa kwenye Katiba ya Zanzibar kinachohusu Tume za Utumishi zote kwa sasa ni nne, na kilichohusu Kamisheni basi chote kimezingatiwa na Sheria yetu Nam. 2 ya mwaka 2011. Kwa hivyo, sitaki niende kwenye vifungu kwa sababu sitaki nichukue muda katika kunukuu vifungu vya katiba na sheria hii.

Kwa maana hiyo, nataka nikubaliane na Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kwamba jambo hili kwenye bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, mwanafunzi wangu Mhe. Hamza Hassan

Juma aliibua *concern* yake pamoja na hoja yake na hatimaye Baraza hili likaiamua hiyo hoja, kwamba Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kushirikiana na Ofisi ya Utumishi wa Umma na Ofisi ya Rais Fedha pamoja na taasisi husika tutakaa kwa ajili ya kulizungumza suala hili la maslahi ya watumishi wa Baraza la Wawakilishi.

Lakini nasema nakupongezeni kwa sababu hamkuwazungumzia tu watumishi wa Baraza la Wawakilishi. Vile vile nataka niseme kwamba ziko hoja nyengine zimetolewa na nafikiri hiyo aliitoa Mhe. Mbarouk Wadi Mussa, kwamba kwa nini serikalini *scheme of service*, kuna tofauti ya miundo ya utumishi na miundo ya taasisi.

Sasa nazungumzia miundo ya utumishi (*scheme of service*). Kwa hivyo, miundo ya utumishi yote iliyoidhinishwa ya wizara 16 za SMZ, imeidhinishwa kwa kuweka daraja za watumishi kwa kuzingatia viwango vyao vya elimu, pahala anapofanyia kazi, mwaka alioingia kazini, *qualifications* zao pamoja na ngazi za mishahara ambayo hivi sasa kwenye *salary structure* iliopo sasa imezingatia vigezo hivyo, hata hizo taasisi zote za serikali.

Kwa nini imefanya hivyo? Imefanya hivyo kwa sababu sheria hii inatambua kuwepo kwa maslahi mazuri kwa taasisi muhimu kama ya Baraza la Wawakilishi na taasisi nyengine za serikali kutegemea viwango na ujuzi wa mtumishi ambaye yupo.

Mhe. Spika, kwenye kifungu cha kuanzia 93, lakini hasa 94 inaitaka Kamisheni wakishapokea mapendekezo ya mishahara kutoka kwenye Tume hizi za Utumishi na Kamisheni ishauriane na Ofisi Kuu ya Utumishi wa Umma, Wizara ya Fedha na Uchumi wakimaliza warudi wayafanyie kazi na hatimaye maamuzi watakayoyafanya Kamisheni wanayapeleka kwa Mhe. Rais na ndipo anapoyatolea uamuzi. Mhe. Spika, wanaomba Waheshimiwa Wajumbe, waangalie kifungu cha 94 cha Sheria ya Utumishi wa Umma.

Sasa mimi nataka niahidi kwamba nitaendelea kufanyia kazi Katiba hii na wala sitathubutu hata siku moja kuvunja yaliyomo katika Katiba, lakini pia yaliyomo kwenye sheria hii. Kwa hivyo, kilichopo Waheshimiwa lile suala la Kamisheni kuamua kuwaambia Tume ya Utumishi ya Baraza kwamba imeidhinisha muundo wa utumishi bila

ya kuzingatia mapendekezo ya mishahara mipya, basi busara yake ni hiyo ambayo ipo kwa mujibu wa sheria na wala sio kuidharau taasisi.

Mhe. Spika, baada ya hapo kama tulivyosema hivi sasa tupo kwenye maandalizi ya marekebisho ya viwango vipya vya mishahara. Kwa hiyo, serikali itahakikisha inayaangalia na kuyatolea maamuzi mema na wala sio mabaya, yale mapendekezo ambayo yameonekana. *(Makofi)*

Kwa hivyo, inawezekana pengine hivi viwango ambavyo viko sasa au vilivyopendekezwa sasa vikawa vidogo zaidi kuliko vile ambavyo Mhe. Rais ataamua kuviidhinisha. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, niwaombe Waheshimiwa Wajumbe kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba haikuwa na maana Kamisheni ilizuia kwa sababu tu ya utashi wao, isipokuwa ni kufuatana na matakwa ya sheria. Mhe. Spika, naomba niwahakikishie na kwa bahati nzuri sheria hii inatambua kuzingatia mazingira maalum ya maeneo kama kuna haja ya kuona kwamba kada hii inahitaji kuekewa kiwango chake kutokana na uzito wa shughuli za chombo chenyewe, basi sheria hii inatambua kuwepo hilo.

Kwa hiyo, niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wenzangu kuhusu hili wasiwe na wasi wasi na serikali inaendelea kulifanyia kazi na hatimaye Mhe. Rais kama nilivyosema siku ya Wizara ya Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwamba Mhe. Rais anawapenda sana watumishi wote wa Zanzibar na mtu unayempenda humtakii mabaya bali unamtakia mema na kutaka afanikishe malengo yake kwa mujibu wa hali ya uwezo uliopo. *(Makofi)*

Katika hili napenda niseme kwamba sisi tunaangalia *scenario* na niliulizwa swali pia kuhusu kima cha chini kwamba bajeti yangu iko *vague* nadhani alikuwa rafiki yangu Mhe. Ismail Jussa Ladhu na Mjumbe mmoja nafikiri akaunga mkono. Kwa kweli hili serikali tumelifanya kwa nia njema kabisa, kwamba si vizuri wala si busara kwa kila wakati unapoamua kutangaza maslahi ya watumishi ukaamua kuyatangaza hadharani yana-*repercussions* zake.

Mhe. Spika, uzoefu unatuonesha kwamba serikali ikishatangaza kima cha chini, basi siku ya pili kila kitu bei juu, ndio busara iliyotumika na wala haikuwa na nia kwamba tusiwe wazi katika hili. Kwa hivyo, kama nilivyosema kwamba serikali itakuwa wazi kwa utaratibu na wenzetu juzi Tanzania Bara wamefanya jambo kama hili na wenzetu nchi nyengine wanafanya jambo kama hili, kwamba nia unaitangaza kwa sababu ya uwezo uliopo.

Vile vile nataka niseme kwamba katika eneo hili la nyongeza ya maslahi ya watumishi kuna bilioni 15.5 kwa ajili ya kazi hii. Sasa mimi nataka Waheshimiwa Wajumbe wajue kwamba hili jambo tunalifanyia kazi na kadri itakavyowezekana, basi tutahakikisha watumishi wa kima cha chini wanafaidika zaidi kuliko watumishi walio juu na hiyo ndio nia ya serikali. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa kuelewa kwamba inawezekana pengine suala la mishahara, lakini sisi kwa safari hii tunawazingatia zaidi watumishi wa kima cha chini kuliko watumishi wa ngazi za juu kuanzia ngazi ya Mkurugenzi na kuendelea. Kwa hivyo, tunafanya hivi makusudi kwa sababu ya kuona umuhimu wa watumishi wetu. Mhe. Spika, niwaombe Waheshimiwa Wajumbe, kwamba niyaeleze hayo na wanielewe na tuko tayari kushauriwa zaidi juu ya jambo hili.

Lakini lile alilolisema ndugu yangu Mhe. Mbarouk Wadi Mussa kwamba kwa nini Tume za Utumishi za Wizara 16 ziliidhinishwa lakini hizi Tume za Idara Maalum, Tume ya Utumishi Baraza la Wawakilishi, Tume ya Utumishi ya Mahakama zenyewe zinaonekana kama zimechelewa miundo yao ya utumishi kuidhinishwa?

Mhe. Spika, ni kweli nataka nikubaliane na Mhe. Mjumbe, lakini hili limetokana na maombi ya tume zenyewe yalivyowasilishwa kwenye Kamisheni ya Utumishi wa Umma na wala haikuwa na nia ya kubagua hizi tume nyengine, tume zote ziko sawa na majukumu yake yako sawa na wala hakuna Tume ya Utumishi ambayo ina mamlaka ya kumsimamia mwenziwe, isipokuwa kwa mujibu wa sheria na Katiba ya Zanzibar na msimamizi wa hizi tume ni Kamisheni ya Utumishi wa Umma, yaani ni *regulatory* wa masuala ya utumishi wa umma hapa Zanzibar.

Sasa haya haiwi sisi kama ni kioja hata nchi za wenzetu hivi karibuni tulisikia Kenya, kwamba muhimili mmoja uliamua kupanga, lakini wananchi wakaandamana wakaenda na vichwa vya nguruwe, ng'ombe. Lakini hatimaye Bunge la Kenya likaona busara kukubaliana na chombo kilichowekwa kilichopewa mamlaka ya kuangalia maslahi ya watumishi wote kwa jumla na Bunge likakubaliana na matakwa ya Tume ya Utumishi wa Umma kule Kenya.

Kwa hivyo, mifano hii ipo lakini haina maana kwamba au ninachotaka kusema ni kuwa Kamisheni haifanyi hivi kwa sababu tu ya kuwa hawaipendi wafanyakazi hapana, isipokuwa kuna hizo taratibu.

Mhe. Spika, eneo jengine ambalo limezungumzwa sana katika Baraza la Wawakilishi ni eneo la utendaji kazi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na hili limechangiwa na wengi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwanza na mimi nichukue nafasi ya kumpongeza sana Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kazi nzuri ambayo ameifanya. *(Makofi)*

Kwanza nataka niungane na Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Kwa kweli ninafanya kazi kwa misingi ya Katiba na Sheria zilizopo, kwa sababu Katiba ndio msingi mama, lakini Katiba haiwezi kumaliza kila kitu kama ni binadamu basi unaweza kusema hichi ni kichwa, halafu kuna *brain* na moyo. Kwa hiyo, Katiba ni kichwa, Sheria ni *brain* na kanuni ni moyo. *(Makofi)*

Kwa hivyo, ukiamua kufanya kazi kwa kupitia Katiba peke yake bila ya kuzingatia sheria nyengine zilizopo basi unaweza usifikie malengo. Mhe. Spika, mimi naelewa madaraka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yaliyoelezwa kuanzia kifungu Nam. 12, ambacho kifungu hichi zaidi kinazungumzia uteuzi wake, na mara nyingi baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe wakinukuu wanakinukuu kifungu hichi kinaelezea uteuzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwenye kifungu kidogo cha 2 mpaka (c) vinaelezea sifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Lakini kifungu cha 3 kinaeleza majukumu yake yanaendelea mpaka kwenye ukurasa wa 76 ya Katiba hii kueleza mambo mengine.

Mhe. Spika, kifungu kidogo cha 3(c) naomba kunukuu kidogo.

Kifungu cha 3(c) cha Katiba, ambacho kinaeleza hivi:-

> "Angalau mara moja kila mwaka kufanya ukaguzi na kutoa taarifa juu ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar …"

Sasa imetoka hoja juu ya Baraza kumuagiza Mdhibiti na Mkaguzi kwamba aende akaangalie *pay roll* ya serikali. Mhe. Spika, nataka niseme chanzo cha kugundua upotevu wa fedha uliotokea katika Kikosi cha KMKM ni ukaguzi uliofanywa na Wizara ya Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora. *(Makofi)*

Kwa kweli walipokwenda watu wetu kule kufanya ukaguzi wa mishahara sisi ndio tukagundua na baada ya kugundua kwa kushirikiana na *CAG*, tukamtilia kwenye *computer* yake *pay roll* ya serikali kwa wakati ule, kwa hiyo yeye anayo *access* ya kuweza kufanya ukaguzi. Lakini ukikiangalia hichi kifungu (c) kwamba mamlaka ya kufanya ukaguzi kwenye *pay roll* ni mamlaka yake kwa mujibu wa kazi zilizooneshwa katika Katiba hii.

Mhe. Spika, tunapomuagiza hapa Baraza la Wawakilishi, nafikiri kwa kumkumbusha inawezekana, lakini kwa mujibu wa kifungu hichi (c) maana yake hilo ni jukumu lake la msingi na wala hahitaji kuagizwa. Kwa hiyo, kuna vifungu vyengine vinasema kwamba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu hatalazimika kufuata na vyote mimi navijua.

Sasa nasema hiki kifungu kinamtaka Mdhibiti afanye hiyo kazi na kazi nyingi zimetajwa pamoja na kuidhinisha matumizi, kwa sababu yale matumizi yanayoidhinishwa hapa hayatumiwi mpaka yeye *authorize* jukumu hilo lake la msingi.

Kwa msingi huo mimi naelewa majukumu ya Mdhibiti na pia naelewa kuwa Mdhibiti anafanya kazi kwa kupitia sheria nyengine ikiwemo Sheria yake ya Ofisi ya Mdhibiti Nam. 11 mwaka 2003 na Sheria ya Fedha, kwa hiyo naelewa na hata siku moja Mwenyezi Mungu asinijaalie kuingilia kazi za Mdhibiti, lakini kwa mujibu wa majukumu

niliyopewa kama waziri basi ninao wajibu wa kusimamia shughuli za kiutawala zinazofanyika katika Ofisi ya Mdhibiti.

Kwa hivyo, msingi wake ni huo Rais ametuea mawaziri na amewapangia majukumu tofauti. Miongoni mwa majukumu ambayo nimepangiwa ni pamoja na kusimamia uendeshaji wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama zilivyo ofisi nyengine. Kwa mfano, leo Rais anaweza kuamua ofisi hii aipeleke kwenye wizara nyengine, waziri huyo atakuwa na majukumu sawa kama nilivyo mimi.

Mhe. Spika, nataka niseme nitathubutu wala sitaingilia na wala uwezo huo wa kuingilia sina, isipokuwa uwezo na majukumu pamoja na wajibu wa kusimamia na kutoa uongozi pale ninapoona mambo hasa yanayohusu mambo ya utawala, na kwenye ripoti huku siruhusiwi na hivyo ndiyo Katiba inavyosema.

Vile vile nataka niungane na Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwamba kama kuna kipindi Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Mashirika zimewasilishwa kwa wakati, basi ni kipindi hichi tokea nimekuwa mimi waziri. *(Makofi)*

*Nataasafu* kusema wakati tunaanza na ile ripoti niliyoiwasilisha mwanzo kwenye *corridor*, labda mengine niyaseme. Kwa hivyo, aliniambia Mheshimiwa nilileta ripoti Ofisi ya Rais mpaka tumemaliza uchaguzi basi ripoti imeshindwa kuwasilishwa Baraza la Wawakishili, kwa maana hiyo ndio ile ripoti ya kwanza niliyoiwasilisha katika Baraza hili na ripoti inapowasilishwa na Mdhibiti haipelekwi kwa waziri, isipokuwa anapelekewa Rais na mimi nalielewa hilo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mara zote tatu tulipopeleka ripoti basi Mhe. Rais alipenda tu niwepo wakati yeye anawasilisha muhtasari na sio kukabidhiwa mimi kitabu, isipokuwa muhtasari wakati alipowasilisha kwa Mhe. Rais ripoti yake. Kwa hivyo, mara zote tatu haijatokea hata siku ripoti ile kuletwa kwangu na halafu mimi ndio nikaiandikia dokezo kupelekwa kwa Mhe. Rais, isipokuwa moja nalifanyia kazi kwa sababu ni wajibu wangu, kwamba Mhe. Rais Mdhibiti yuko tayari

kuwasilisha ripoti kwako, yaani ni wepesi tu wa kutaka kile kitu kifike haraka. *(Makofi)*

Lakini hata hicho cha kuomba *appointment* ikionekana kwamba hakisaidii basi mimi sijui niseme nini, kwa kweli sijawahi na wala sitathubutu na nadhani haitafikia hatua hiyo. Kwa hivyo, amewasilisha Mdhibiti ripoti ya kwanza *State House* ya Mnazi Mmoja na ripoti mbili ameziwasilisha nyumbani kwake Mhe. Rais.

Pia *nataasafu* kusema nakubaliana na Mhe. Mbarouk Wadi Mussa kwamba ripoti ya kipindi hichi haijawasilishwa. Mhe. Spika, mimi nimepokea barua ya kuonesha kuwa ripoti iko tayari, lakini nikaona nakla imepelekwa na wala hakikuja kitabu kwangu, kwa hiyo mimi sizuii Mdhibiti anayo *right* kwa mujibu wa Katiba kupeleka ripoti yake moja kwa moja kwa Mhe. Rais na hatimaye Mhe. Rais ndio anaamua kwamba niiwasilishe ndani ya Baraza hili Mhe. Spika.

Sasa kama imefika kwa Mhe. Rais na kesho akiniambia iwasilishe Barazani, basi nitakuomba Mhe. Spika kama ninavyofanya, kwamba niiwasilishe ripoti hii hapa ndani ya Baraza la Wawakilishi.

Kwa hivyo, naomba nisieleweke hivyo na ninawaambia wananchi wangu wa Jimbo la Tumbatu pamoja na wananchi wa Zanzibar, kwamba sijafanya hivyo na wala sitafanya, kwa sababu naelewa majukumu yangu ya msingi kama waziri, kwani majukumu yangu ni usimamizi na kutoa ushauri pale inapobidi.

Kuhusu kadhia ya rasilimali watu mwanafunzi wangu Mhe. Hamza Hassan Juma. Mhe. Spika, nadhani tutakumbuka kwenye bajeti ya mwaka jana au ripoti ya Mdhibiti na siikumbuki vizuri, lakini katafute *hansard* yako mwenyewe, ulisema kwamba kuna tatizo gani huku kwa Mdhibiti kuhusu matatizo ya rasilimali watu. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, Waheshimiwa Wajumbe ndio munaotutaka sisi mawaziri kwamba maoni munayoyatoa pamoja na ushauri munaotupa tuufanyie kazi na mimi sijasahau. Sasa kwa sababu ya kuheshimu ushauri na maamuzi yanayotolewa Baraza la Wawakilishi, basi mimi niliagiza ofisi yangu na baadaye nikaiagiza bodi na wala sikumuagiza Mdhibiti maana kuna Bodi ya Utumishi. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, nikaiambia kwamba inaonekana lipo tatizo la watumishi tafadhalini lishughulikieni na baadaye munipe taarifa na huo ni wajibu wangu kwa mujibu wa Sheria hii ya Utumishi wa Umma. Mhe. Spika, katika sheria hii kuna kifungu kinamtaka Rais, Waziri na sentensi hiyo inamtaja waziri wake.

Kwa hiyo, Rais maana yake ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Waziri maana yake ni Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora, na waziri wake maana yake ni waziri anayesimamia ile taasisi juu ya uendeshaji wa shughuli zetu za kiutumishi.

Mhe. Spika, kwa usikivu wangu kama ilivyo serikali yetu sikivu, basi kwa usikivu wangu niliyachukua maoni ya mwanafunzi wangu Mhe. Hamza Hassan Juma nikaenda nikayafanyia kazi na niliiagiza Bodi ya Utumishi kwamba walifuatilie jambo hili na hatimaye waniletee taarifa. Kwa kweli nashukuru bodi imefanya wajibu wake, Mamlaka ya Nidhamu imefanya wajibu wake na ripoti iko juu ya meza yangu. Hivi karibuni tu imeletwa, Mamlaka ya nidhamu hatua walizozichukua wamezichukua na sasa hivi watumishi wale wamerudishwa kazini. Nia yangu ilikuwa nini, nia yangu sio kumuingilia Mdhibiti *no*. Nia yangu ilikuwa zifuatwe taratibu na sheria ziliopo. Wafanyakazi wale walipofanya makosa waliletwa Wizarani. Nikasema sio suluhisho, suluhisho ni Mamlaka ya Nidhamu ambaye ni Mkuu wa Taasisi aanze yeye kuwachukulia hatua.

Mamlaka ya nidhamu kama mkuu wa taasisi anayo haki hiyo, lakini kwa chombo ambacho kinasimamiwa na Bodi ya Utumishi baadaye mambo yale yanapelekwa kwenye bodi. Bodi nayo inaingiza, inafanya kazi zake kwa mujibu wa taratibu. Tunafanya hivyo, sheria hii imetambua hilo kwa nini. Imetambua hili kwa sababu tuna mfano mara nyingi serikali inashindwa Mahakamani. Tunapoamua tu kuwachukulia hatua watumishi bila ya kufuata utaratibu tunakwenda Mahakamani tunashindwa. Kwa hivyo mimi nadhani nia yangu ilikuwa ni hiyo ya kutoa uongozi katika kulishughulikia jambo hili wala sio kuingilia kazi za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mimi ni Waziri nina majukumu yangu kikatiba. Msingi huo ni kwamba mimi ndio ninayekuja hapa mkanihoji. Mdhibiti yule pale lakini pale alipo hawezi kusema, msemaji wake hapa Baraza la Wawakilishi ni mimi. Itakuwa ni jambo la ajabu sana kama Mdhibiti atanyanyuliwa na kule na ambiwe hebu eleza. Lakini utaratibu tuliojiwekea kwa mujibu wa Katiba hii na sheria ni huo. Sasa mimi siwezi ku- *criticize* michango ya Wajumbe, pengine wamefanya utafiti, maana maneno yanayosemwa hapa tunatakiwa tuyafanyie utafiti, pengine na wao wameyafanyia utafiti.

Mhe. Spika, mimi nataka niseme kwa dhati ya moyo wangu Wajumbe waendelee kufanya utafiti juu ya kadhia hii mimi niko *free*, nikionekana kama nina makosa si mtakuja kunambia. Kwa hiyo niseme haya kwa sababu *image* iliyojengeka kwa wananchi, maana ki Haji Omar Chenyewe ndio kimimi hapa. Maana labda linaonekana kama hili jitu la ajabu, hapana. Nafikiri *image* hiyo itoke isieleweke hivyo. Mimi ni mtu wa *principle*, nafuata taratibu. Mhe. Naibu Spika, katika eneo hili nilisema niseme hayo.

Mhe. Spika, nije katika maelezo yanayohusiana na michango mbali mbali kama inavyosomeka, na nafikiri haya maelezo nisiyasome huku mwanzo, kwa sababu Wajumbe hawa wamepata hiki kitabu na wameona nini nimekiwasilisha na michango yao nimeipokea. Mengine nimeshauri au serikali imeshauriwa kwamba iende ikaifanyie kazi. Nawahakikishia Waheshimiwa Wajumbe yale yote mliyotushauri tukayafanyie kazi basi tutakwenda kuyafanyia kazi.

Lakini naishukuru sana Kamati ya Katiba na Sheria na Kamati ya PAC ningekuwa mimi ni mtu wa ajabu hata wazo la Mwenyekiti wa PAC. Mhe. Spika, shahidi lilipokuja mimi nikaanza kuliwekea vikwazo. Hee! Jambo hili ndio kwamba linaanza, kwani miye tu. Lakini nikasema kama Sheria ya Fedha kifungu cha 35 kinataka bajeti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu ya Serikali iwasilishwe kwa Waziri na halafu Waziri aiwasilishe PAC. PAC itoe maoni yake ndani ya Baraza na mimi nitoe maoni yangu, kuna tatizo gani. Si *bid'aa* hili ni sheria. Na nashukuru nimeshirikiana na Ofisi ya Mdhibiti, wala sikuongeza changu katika bajeti ile. Nilicholetewa ndicho nilichokiwasilisha. Na nawashukuru Wajumbe mmeweza kuichangia vizuri.

Sasa nikija kwenye hoja kuhusu Idara ya Mipango Sera ya Utafiti, mpango wa malipo ya mishahara bado haujakaa vizuri. Hili lilizungumzwa na Mhe. Mwenyekiti wa Katiba ya Sheria na Utawala. Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Ofisi imepanga kuandaa sera ya malipo ya mishahara. Hata katika kitabu changu nimesema hilo, tunafanya hivyo kwa kuelewa kwamba Wizara hii ina mambo mengi sana hayajakamilika, tunahitaji kuyafanyia kazi ili yakamilike, ili kila kilichopo ndani ya sheria tuweze kukiweka kwa mujibu wa misingi ya sheria, katiba na sera na kanuni.

Mishahara midogo kwa wataalamu wa kada ya Utafiti, nimeshaisema kuwepo kwa kitengo maalum kinachohifadhi tafiti zinazofanywa na watumishi wa umma wanaotokea masomoni.

Namshukuru sana Mhe. Marina kwa ushauri wake na ushauri tunaupokea. Ili hizi tafiti pamoja na kwamba suala la utafiti haliko kwangu moja kwa moja. Lakini wanafunzi au Wazanzibari wanaokwenda masomoni. Sera ya mafunzo ni yetu sisi basi tutashirikiana na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kuhakikisha kwamba hili jambo serikali inalifanyia kazi. Kwa sababu wanafunzi wetu wanafanya tafiti nyingi na tafiti hizi zinaweza zikatusaidia katika maendeleo ya nchi yetu.

Idara ya teknolojia ya habari na mawasiliano kutoa taaluma kwa jamii. Mhe. Mwenyekiti, wa Kamati ya Katiba na Sheria na utawala, Katika Bajeti hii Ofisi imetenga fedha kwa ajili ya mafunzo kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, watendaji wakuu, wananchi na jumuia za kiraia. Tumesema mle tutajenga hata *community center* kwa ajili ya kuhakikisha hili jambo linafanyika. Kwa hivyo ushauri wako Mwenyekiti tunaupokea.

Idara ya Uendeshaji na Utumishi wa Umma. Ufafanuzi wa matumizi ya fedha ya bilioni moja thathini na nne elfu mia tisa sabini na nne na mia tisa yaani inazungumziwa bajeti ile iliyopita. Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba Sheria na Utawala fedha zilizotumiwa hadi Machi 2013 ni kama ifuatavyo, milioni mia saba tisini na moja laki nane sitini elfu mia sita sitini na nane. Matumizi ya kawaida ni shilingi arubaini

na moja milioni laki sita arubaini na nne elfu mia tisa na tatu kwa kazi za maendeleo.

Kuna Mwakilishi mwengine kiwango kilichotengwa ni hichi, je hizi zilizobakia ziko wapi na zimekwenda wapi. Utaratibu wa matumizi serikalini ni kwamba unachopewa ndicho unachotumia na *Inshallah* haya matumizi yalikuwa yamezingatia mpaka mwezi wa Machi, lakini tunayo matumizi ambayo yamekwenda mpaka Juni mwaka huu. Ni si kweli kwamba bilioni moja zote ndio tumezipata zile zilizotengwa. Lakini ni lazima itakuwa kuna fedha ambazo zimebaki hatukuingiziwa na hizo kwa utaratibu wa kawaida zinabakia Hazina, maana unatumia kile unachopewa.

Idara ya Mipango Rasilimali Watu, kuporomoka kwa maadili ya watumishi wa umma. Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala alisema hili na Ofisi itaendelea kutoa mafunzo ya maadili kwa watumishi wote wa umma kama tulivyoanza hivi sasa.

Idara ya miundo ya taasisi na maslahi ya watumishi, utekelezaji wa miundo ya watumishi wa umma haijaonesha mabadiliko makubwa. Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba Sheria na Utawala. Hivi sasa watumishi wote tayari wameshapangwa kwa mujibu wa miundo ya utumishi na mazingatio yanafanywa kwa mwaka wa fedha huu kwa watumishi wa muda mrefu. Kwa hiyo hi ni kazi endelevu si kazi ambayo tutasema hapa ndio tumekoma, hii ni kazi ambayo tutaendelea kufanya, tutafanya itamaliza, tukiona kuna haja ya kuipitia tena, tutafanya hivyo maana sheria ime *provide* hivyo.

Kuwepo kwa wafanyakazi hewa na kukaguliwa kwa mfumo wa malipo *pay roll* ndio lile nililolisema. Mdhibiti kwa mujibu wa majukumu yake anao uwezo huo bila ya kuagizwa na mtu yeyote kwamba majukumu yake yameelezwa, kwa hivyo sisi hatuna tatizo, hata kidogo kwa mujibu wa majukumu yake yanampasa afanye hivyo.

Na ieleweke kwamba ni kweli kwa mujibu wa sheria sisi tunaidhinisha malipo kwenye *pay role*, lakini bado tunaangalia uwezekano serikali huku tunazungumza ili sasa hata ile *management* ya *pay roll* ihamishiwe Ofisi ya Utumishi wa Umma. Kwa sababu haya mambo mengine yanayotokea kwa mfano Katibu Mkuu wa Utumishi

ameshaombwa na taasisi husika, ameshasema kwamba mtu huyu anastahiki kulipwa kiwango hiki cha fedha kwa mujibu wa *qualification* zake. Inachukua muda ndio pale pengine inapoonekana mtu amerudi kusoma lakini muda umechukua mkubwa hajalipwa. Ni kwamba kuna vitu viwili, kuna usimamizi wa *pay roll* na kuna *management* ya *pay role.* Nataka niseme kwamba management ya *pay role* kwa maana ya ile *management* inayoshughulikia *pay roll* bado ipo Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Idara ya Utawala Bora, elimu ya uraia haiwafikii wananchi wa Pemba. Mhe. Bikame na Mhe. Asha Bakari, ni kweli na nawashukuru sana kwa suala hili. Elimu ya uraia inatolewa kwa shehia na taasisi za elimu na kwa upande wa Micheweni tutatumia redio jamii ya Micheweni badala ya kutumia redio ya Shirila la Utangazaji la Zanzibar.

Semina ya mafunzo juu ya serikali ya umoja wa kitaifa ili Wawakilishi wapate elimu hiyo. Wizara yangu imedhamiria kulifanyia kazi jambo hili na tayari kama nilivyoeleza kwenye kitabu changu kwamba tumezungumza na shirika la USA na tumefikia mbali sana, na tumeahidiwa kupata fedha za kutosha za kuweza kuendesha shughuli hii. Mradi huu ni wa miaka mitatu na nina hakika miaka mitatu itatosha katika kutoa elimu ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Lakini si hilo tu lakini na wananchi kuwajengea uwezo wa kujua haki zao na wajibu wao.

Sisi kama Wizara wenye dhamana ndio maana baada ya kuona pengine huku serikalini tunaweza tukawa hatuna uwezo mkubwa ndio maana sisi Wizara ya Utumishi na Utawala Bora tumeamua tufanye, na mazungumzo yamekwenda vizuri na hivi karibuni tunatarajia kutia saini mkataba wa makubaliano na shirika hili ili hii kazi iweze kufanyika. Nasema sio wanasiasa, maana tupo wana siasa ambao hatujaielewa dhana ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa, wako watendaji ambao hawajaelewe lakini wapo wananchi pia ambao hawajaelewa.

Idara ya nyaraka, kutoa elimu kwa Ofisi ya uwekaji wa kumbukumbu katika Idara ya Vizazi na vifo. Ushauri unazingatiwa na kwa sababu tunayo programu hiyo ya kufanya mafunzo kwa taasisi zote za umma. Nadhani kazi hii ni endelevu na hata mwaka uliopita tumefanya kazi

hii na mwaka huu tunatarajia kuiendeleza kama ni jukumu letu la msingi katika idara hii.

Malipo ya tafiti yalipwe Idara ya Nyaraka badala ya Ofisi ya Makamu wa Pili. Mhe. Wanu Hafidh Ameir, ushauri tunaupokea na tutaupeleka serikalini kwa mazingatio. Kwa sababu kama ninavyosema sisi kazi yetu ni kuhifadhi na kuwawezesha wale wanaofanya tafiti waweze kufanya tafiti zao. Lakini vibali vya kufanya utafiti vinasimamiwa na ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Sasa kama ushauri wa Baraza tunauchukua na tutaupeleka serikalini na tutaufanyia kazi.

Kamisheni ya Utumishi wa Umma. Malalamiko ya ucheleweshaji wa Miundo ya Utumishi. Kama nilivyosema kule mwanzo Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala Mhe. Ismail Jussa Ladhu, Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Mbarouk Wadi Mussa, Mhe. Salmin Awadh na wengi wengineo waliochangia hoja hii. Miundo ya Utumishi wa Baraza la Wawakilishi imeshaidhinishwa sio muundo wa Baraza.

Muundo wa Baraza kwa *structure* ya zamani kama sheria inavyosema ipo. Lakini Baraza hili litajaaliwa na kutunga sheria ya Utawala wa Baraza ambayo itaonesha *structure* yake mpya hiyo itazingatiwa wakati huo na hakuna sababu ya kuikataa kama nilivyosema.

Katika kufanya hili sheria ina *provide* hilo lakini unapoandaa *structure* mpya utaratibu wake kama ule wa mishahara mipya, kwamba Tume inapeleka kamisheni na kamisheni inakwenda kwa Mhe. Rais. Najua kuna mawazo mengi lakini ni jambo linalozungumzika. Kwa nini hii nayo aidhinishe Mhe. Rais, yeye ndio kiungo wa Mihimili yote hii mitatu, Lakini ni kweli Mhe. Spika, ndio kiongozi wa muhimili huu wa Baraza la Wawakilishi.

Nataka niseme kwamba Kamisheni hii ina Wajumbe 7 pamoja na Mwenyekiti wake. Lakini Wajumbe sita wametoka katika mihimili yote hii ya dola. Wajumbe wawili amewapendekeza Mhe. Spika, na Mhe. Rais hakupata kigugumizi, akaamua kuwateua. Wajumbe wawili wamependekezwa na Mhe. Jaji Mkuu, na Mhe. Rais aliwateua, na Wajumbe wawili wamependekezwa na Waziri wa Utumishi wa Umma. Kwa sababu Kamisheni hii inasimamia Tume zote za Utumishi

wa Umma, lakini hichi ndicho chombo cha juu kwa mujibu wa Katiba na Sheria yetu ilivyo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sitaki kwenda sana katika suala la mabishano ya kisheria bahati mbaya mimi ni mvuvi. Bahati nzuri mimi mvuvi si mwanasheria lakini nimeingia katika chombo cha kutunga sheria. Wanasheria wenyewe wanaweza wakabishana, wanapobishana wanasheria mimi siwezi kusema kitu, maana si mwanasheria. Lakini natunga sheria na nimejifunza kutunga sheria na nimejifunza vile vile kusoma sheria, lakini si mwana sheria. Kwa hiyo miundo ya utumishi ya Baraza la Wawakilishi isiyoambatana na mishahara mipya imeidhinishwa na Wizara zote zimefanyiwa hivyo. Itakapotoka *salary structure* ya kila taasisi basi nao itarejeshwa kwenye kila Tume ya Utumishi iliyopeleka maombi yake.

Chuo cha Utawala wa Umma kuharakisha suala la malipo ya chuo cha Utawala wa Umma na taasisi nyengine. Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba Sheria na Utawala, suala hili limo katika hatua za mwisho kukamilika. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala bahati nzuri yeye ni Mjumbe wa Baraza la Chuo kwa hiyo haya mengine ni sehemu ya wajibu wake. Imani yangu tutaendelea kushirikiana katika kuona haya yote ambayo yametolewa hapa tunayafanyia kazi kwa pamoja.

Mamlaka ya kuzuia rushwa na uhujumu uchumi Zanzibar, mishahara ilingane na majukumu ya taasisi. Mhe. Mwenyekiti, wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na Waheshimiwa wengine walichangia sana kama nilivyosema mwanzo. Nataka niseme mimi binafsi kama Waziri ninayesimamia hili nishakwenda kujifunza namna ya vyombo hivi vinavyofanya kazi. Bahati mbaya kwamba katika kukutana na watu mbali mbali. Mwezi huu uliokwisha tarehe 22 na tarehe 24 nilialikwa na taasisi za Kuzuia rushwa na uhujumu uchumi duniani kwenda kutoa *paper*, lakini kwa sababu ya kuheshimu mkutano huu wa bajeti nilisamehe kufanya hivyo na niliwajulisha rasmi kwamba kutokana na mazingatio maalum ya bajeti. Maana sisi pengine tukipata nafuu ya kupiga *trip* hizi tunajifunza lakini pia tunapata na kupumzika na pengine *alhamdulillah* ningepata nyongeza ya kuja kuwaona wananchi wangu. Lakini nikasema hapana kuna jambo muhimu la bajeti siwezi kufanya hivyo.

Kwa hivyo nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe kwamba mimi tayari naelewa uzoefu wa nchi nyengine juu ya mafao wanayolipwa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi. Nataka niwaahidi kwamba panapo majaaliwa jambo hili linawezekana kabisa kabisa kwa sababu tutakuwa ni watu wa ajabu sana, kwamba wenzako wanafanya hivi kwa ajili ya kuwalinda hawa watumishi ili na wao wasije wakaingia katika *corruption* halafu na wewe ukawa hukubaliani na hili, utakuwa unafanya mchezo.

Sasa mimi nataka niwaahidi Wajumbe kwamba hili jambo tunalishughulikia na panapo majaaliwa napenda nitoe taarifa kwamba mamlaka hii tumeanzia na vijana 32 kuwaajiri na kuanzia tarehe mosi wapo tayari sasa hivi kwenye mafunzo maalum ambao tumewaalika watalaamu kuja kuwafundisha hapa hapa Zanzibar. Lakini tumewatafutia pahala wanapewa kozi hii nje ya mji. Nia yetu ni kwamba taasisi hii ianze kazi zake rasmi. Kama tunavyoelewa kwamba Mkurugenzi Mkuu amechelewa kuteuliwa na hatimae baada ya kufanya hivyo kama nilivyosema kwenye kitabu changu tumehamisha wafanyakazi 6 na hivi sasa tumeajiri wafanyakazi 32 na wako kwenye mafunzo maalum kwa ajili ya kuja kutekeleza wajibu wao.

Mhe. Spika, yapo mengine ambayo yalizungumzwa na mtu mmoja mmoja lakini mengi yaliyozungumzwa nimeshayatolea ufafanuzi lakini alilolizungumza ndugu yangu kule Mhe. Mtando kwamba nimeshindwa kuwajibika kuhusu suala la kutunga Kanuni. Kwanza nataka niseme kwamba sijashindwa kuwajibika lakini hii sheria ambayo tuliipitisha mwaka 2011 mapema nafikiri ni Mswada wa mwanzo kuupitisha ndio tunaona hivi tunavyozozana. Sasa jambo linalowahusu watu wengi huwezi kukurupuka ukajifanya kwamba wewe umepewa uwezo na sheria halafu ukaamua kutunga kanuni za ajabu ajabu bila ya kufanya *consultation* na bila ya kupata mawazo ya wengi.

Sasa nataka nimuhakikishie Mhe. Mtando kwamba kanuni zipo tayari na hivi karibuni tunatarajia kama nilivyosema mwanzo kwamba hizi kanuni ilibidi washiriki watu wengi isiwe ni Waziri tu kwa sababu nimepewa mamlaka. Ni kweli ninayestahiki kuhojiwa hapa ni mimi

kwa sababu sheria inanitambua na silikatai hili. Lakini mimi nadhani si kanuni hii tu ambayo sheria zake zipo lakini kanuni haijatungwa. Wala hiyo sifanyi kama ni *excuse* kwenu kwamba kwa sababu kuna sheria nyengine hazijatungiwa kanuni hili ndio liwe msamaha kwangu. Ninalolisema kwamba pengine mimi niko *more advanced* kuliko sheria nyengine katika kulitekeleza hili. Nataka muniamini kwamba kanuni zipo tayari tutazichapisha kama tulivyoichapisha sheria hii. Nakuhakikishieni katika kikao kijacho nitahakikisha kila mmoja anapata kitabu chake cha kanuni za Utumishi wa Umma ili tuondokane na huu utata ambao tunao hivi sasa. Mhe. Spika, kupitia kwako nataka niliahidi kabisa Baraza lako Tukufu.

Mhe. Spika, jengine ambalo limezungumziwa na Mhe. Jaku Hashim Ayoub rafiki yangu ni suala la mtumishi wa kituo cha afya Muyuni. Ni kweli tulipokwenda ziara ya Muyuni Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alisomewa risala na Wananchi wa Muyuni na miongoni mwa mambo yaliyojitokeza ni tatizo hili la kumuajiri kwa mkataba mfanyakazi huyu wa kituo cha afya. Sheria yetu inatambua kwamba kila mtumishi ana haki ya kuongeza muda wake kabla hajachukua mafao yake.

Nataka niwahakikishie kwamba mtumishi huyo tayari ameshaongeza muda kwa kipindi cha miaka miwili na akaongeza kwa kipindi cha mwaka mmoja kwa kufuata taratibu ziliopo. Baada ya wananchi wa Muyuni kumuomba Mhe. Rais, Rais akisema kitu inakuwa ni agizo, lakini agizo lile kwanza lazima urudi katika taratibu za sheria katika misingi ya utawala bora, kwamba ni njia gani mtaifanya ili msije mkapata matatizo ya kisheria. Sasa kuna *legal note* ambayo nimeisaini na nimetoa tangazo katika gazeti rasmi la serikali kutangaza kada adimu hasa katika Sekta ya Afya, *legal note* ile inatambua watumishi wenye kiwango cha diploma hatutambui wale ambao wana nafasi za chini.

Nini kinachoweza kufanyika, ama bodi ya madaktari ikae ibadilishe vile viwango na madaraja ya wataalamu, itambue kwamba cheti alichonacho mtumishi wetu yule wa Muyuni kwamba kama tulivyofanya kwa walimu wa Chuo cha Karume wenye vyeti vya PF kama tulivyofanya kwa wale tunatambua kwamba wale sasa wana ngazi ya Diploma.

Kwa hivyo Bodi ya Afya ikikaa ikiidhinisha maana yake huyo *automatic* ataingia katika *legal notice* ambayo nimeitangaza kwa mujibu wa marekebisho ya sheria ya utumishi wa umma ambayo niliileta hapa Barazani. Na tuliileta wakati ule wengi wetu tulikuwa na hofu kwamba tunawanyima vijana ajira na nini lakini tulikuwa tunatambua kuwepo kwa tatizo la wataalamu ndani ya nchi yetu.

Ama mimi Waziri niliyepewa mamlaka nirudi katika *legal notice* yangu nirekebishe kwa mujibu wa mamlaka niliyonayo kisheria. Tukifanya hivyo mfanyakazi yule ataajiriwa. Sasa nitashauriana na Wizara ya Afya wakiona kukaa *board* ni tabu, basi mimi nitarudi nataka nikuhakikishie Mhe. Jaku kwamba nitarekebisha *legal notice* baada ya kupata ushauri wa bodi inayohusika na wataalamu wa afya nirekebishe na hatimaye yule mtaalamu tuweze kumuajiri kwa mujibu wa sheria yetu hii ya utumishi wa umma, kwa mujibu wa vipindi ambavyo ameshapewa mkataba sasa hivi huwezi kumuajiri kwa mkataba bila ya kufanya marekebisho hayo ambayo yanaendana na sheria.

Kwa hivyo Mhe. Jaku ninakushukuru sana kwa kuwatetea wananchi wa Muyuni na wanakuelewa, na mimi nimekuelewa na serikali inakuelewa, na Rais aliwaelewa wananchi wa Muyuni. Lakini akishafanya kitu Rais sisi wasaidizi wake inabidi tufanye kulingana na sheria ziliopo ndio msingi wenyewe tu huo. Natambua kwamba jambo hili limefika kwenye taasisi zinazohusika, Wizara ya Afya wamelipeleka kwetu lakini kuja kuangalia kwamba haliwezekani kulitekeleza bila ya kufanya mambo hayo mawili. Ama mimi nirudi moja kwa moja kwa kushauriana na Wizara ya Afya hasa ile bodi ya madaktari katika kulishughulikia jambo hili.

Walimu wa sayansi Muyuni hawapo, walimu wa sayansi katika maeneo mengi hawapo. Mhe. Jaku nikupe *offer* ukiwa na vijana ambao wameshasoma ualimu wa sayansi Wizara ya Utumishi imewaambia mpaka Wizara ya Elimu kwamba hakuna kikomo cha uajiri wa walimu wa sayansi katika kipindi hiki. Kwa hivyo kama wapo tuleteeni tutafuata taratibu maana sheria inasema lazima nafasi zitangazwe tutafuata taratibu hizo, lakini tukiona kwamba wataalamu wenyewe hakuna sheria pia inatambua kupata kibali maalum bila ya kutangaza kwa ajili ya kuangalia mahitaji ambayo yapo na kuzingatia mazingira

maalum. Kama tulivyofanya kwa walimu katika maeneo yale ambayo yapo *remote area* kama Kidagoni hapa Unguja na Kisiwa Panza kule Pemba, kwamba tunayo nafasi hiyo na sheria inaturuhusu kwamba tukiona kuna eneo liko *remote* na wapo vijana wa pale ambao wana sifa basi Wizara yetu hatutasita. Kwa hivyo Mhe. Jaku tushirikiane ukiwa na watu kama hao nakukaribisha sana tutafuata taratibu na hatimaye tutawaajiri.

Mishahara ya *DPP* kusema waongezwe moja kati ya taasisi sisi kama utumishi wa umma tumezizingatia ni pamoja na Ofisi ya *DPP* na Ofisi nyengine, kwa hivyo hili halina tatizo ni suala la kunini lakini viko viwango tulivyoviidhinisha kwa wataalamu wa *DPP* sheria inaturuhusu kufanya hivyo kwa kuzingatia uzito wa chombo chenyewe.

Mhe. Suleiman Hemed wafanyakazi waliopelekwa nchi mbali mbali je, Pemba wapo? Wapo wafanyakazi kutoka Pemba ambao nao wamepata fursa hii ya kwenda kujifunza nje ya nchi katika mafunzo ya muda mrefu, wa kati na muda mfupi kama ilivyo Zanzibar. Lakini nataka nilirejee hili kusema kwamba nafasi hizi zinatoka pia kutokana na sifa za watumishi wenyewe zilivyo. Na kwa bahati nzuri hata hapa Unguja tunaokwenda masomoni ni watu kutoka visiwa vyote viwili, ila wanafanyia kazi Zanzibar lakini wanatokea Pemba. Lakini kwa maana ya watumishi wanaofanya kazi Pemba wapo ambao wamepata fursa hii Mhe. Hemed.

Ajira za Muungano ni mara ngapi ajira zimefanyika. Katika makubaliano haya mapya ajira hazijafanyika zinaendelea katika utaratibu ule wa zamani kwa misingi kwamba baada ya makubaliano tuliyokubaliana kati ya sekta husika Wizara ya Utumishi wa Umma na Wizara ya *management* ya Utumishi wa Umma Tanzania hubidi kupeleka kwenye kamati ya mambo ya Muungano. Hatua hizo zimekamilika na baada kukamilika hubidi vile vile kupelekwa kwenye Baraza la Mawaziri na Baraza la Mawaziri la Zanzibar. Hatua hizo zote zimeshakamilika. Na ndio maana tumeripoti kwamba Wizara zote zile zinazohusu masuala ya muungano zimeshapewa taarifa kwa maana ya toleo maalum kwamba sasa utaratibu wa kutoa ajira katika taasisi za muungano ni huu. Kwa hivyo Wizara hii *East Africa* ikiamua

kuajiri watu 20 basi asilimia 21 ni ya Zanzibar na asilimia 79 ni ya Tanzania Bara.

Na tunachofanya kwamba zile asilimia 21 ndio maana tumesema tumeipatia ofisi ya sekretarieti ya ajira ya Jamhuri ya Muungano Ofisi kwenye Ofisi ya Makamo wa Rais ili nafasi zile zitangazwe kwa wazanzibari. Kwa hivyo tutaanza kwenye bajeti hii kwa sababu kwenye kikao chetu cha muungano na sisi tuliarifiwa kwamba rasmi tayari jambo hili taasisi zinazohusika za muungano zote zimeshapewa taarifa kwamba jambo hili litaanza. Na kwa sababu sisi tunafanya kazi kwa karibu zaidi na hii sekretarieti ya ajira tunazijua hata nafasi zilizokubaliwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hivyo sisi ni kuangalia Wizara gani kulingana na uwezo wa fedha wa SMT wanatoa ajira sisi kutaka asilimia 21 yetu ambayo itatolewa kwa wazanzibari.

Lakini kwenye nafasi nyengine zile zisizokuwa za muungano tumepewa fursa pia wazanzibari wajitokeze kuomba nafasi. Kwa mfano nafasi za ualimu na nafasi nyengine za ajira. Kwa hivyo nikupongeze kwa kuliona hilo na napenda nitoe taarifa hiyo.

Upo utafiti wowote uliofanyika kuhusu raslimali watu. Upo na sasa hivi tunakamilisha taratibu za kuwaweka katika *data base* yetu watumishi wote wa umma na kila kitu chao, kwa hivyo utafiti upo Mhe. Suleiman.

Kuhusu ripoti ya *CAG* Mhe. Mbarouk Wadi kutowasilishwa. Kwanza natambua kwamba PAC ripoti ya *CAG* nikisha kui-*table* Barazani tunawakabidhi *PAC*. Kwa hivyo ripoti hii madhali nimearifiwa iko tayari na *CAG* atatafuta muda wa kuipeleka kwa Rais mwenyewe maana halazimiki kufuatana na mimi wala kufanya jambo jengine. Nataka niwahakikishie Rais akiniagiza tu kui-*table* Barazani nitaomba nafasi kwako Mhe. Spika, uniruhusu nii-*table* katika Baraza hili la Wawakilishi.

Maslahi ya wafanyakazi ni madogo. Mhe. Mtando Ofisi ya *CAG* kama nilivyokwisha kutoa maelezo kwamba ipo *room* ya kuzingatia kada maalum na maeneo maalum kulingana na umuhimu wa chombo

chenyewe. Kwa hivyo hilo nitalifanya kwa kushauriana au kwa kushirikiana na vyombo vinavyohusika.

Kuhusu kifungu 105 sheria ya Utumishi wa Umma kuhusu muundo wa Baraza la Wawakilishi. Nimeshatoa ufafanuzi nadhani Wahemishimiwa Wajumbe mridhike tu na hayo niliyoyasema kwamba nia ni moja. Majukumu ya Tume za Utumishi, majukumu ya Kamisheni. Majukumu ya Tume za Utumishi yameelezwa wazi katika sheria na majukumu ya Kamisheni yameelezwa waziwazi. Kwa hivyo nalo hili nataka lieleweke kwamba lipo kwa mujibu wa sheria. Ndugu yangu ulinambia unazuia mshahara wangu kwa sababu sijatunga kanuni. Mheshimiwa uruhusu mshahara wangu nikuombe uruhusu mshahara wangu, maelezo niliyoyatoa kuhusu kanuni kwamba kanuni tayari, kwamba sababu ya kutaka jambo hili liwe na washiriki wengi zaidi isiwe mimi mfalme ndio maana limechelewa kidogo lakini kanuni ziko tayari.

Kwa hivyo mshahara wangu ndugu yangu uruhusu, mshahara huu unawasaidia wananchi na bahati nzuri mimi jirani yako kule, tuna huduma za jamii tuna-*share* mimi na wewe, tuna skuli tuna-*share* mimi na wewe mmoja asipopata nafasi mmoja hulazimika kutekeleza. Sasa ukizuia ndugu yangu hayo nitashindwa kuweza kuyafanya maana nategemea huu huu.

Kwa hivyo Mhe. Mbarouk nakuomba uridhike na maelezo niliyoyasema. Bahati nzuri kwa sababu ya ujirani wetu na undugu wetu kama nilivyosema mimi Mtumbatu wa Kisiwani wewe Mtumbatu wa juu. Wapiga kura hao hao wako wewe mimi ndugu zangu na wapiga kura hao hao wangu mimi wewe ndugu zako. Kwa hivyo hakuna sababu ya kufikishana hapa ndugu yangu nikuombe tu kwamba uunge mkono hoja ili na mimi niweze kutekeleza majukumu yangu. Na ulisema unamuunga mkono Mhe. Mnadhimu wa CCM, na unasema kwa sababu amesema Mhe. Mnadhimu na sisi tuna tabia ya kiongozi akisema wafuasi tunafuata. Inategemea kasema nini, huwezi kufuata kila kitu, ndugu yangu labda nikupe ushauri huo wa bure inategemea kasema nini. Sasa sina mamlaka ya kuingilia mawazo yako lakini nikushauri tu kwamba isiwe kila kitu anachosema mkubwa wako basi ukiunge mkono. Lazima upime alichokisema na hatimaye ufanye maamuzi.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad, ninakushukuru sana umechangia kuhusu Idara ya Mafunzo na ukasema iwepo mikataba maalum ya watumishi wanaokwenda masomoni. Nataka nikuhakikishie kwamba Wizara yangu tayari imeshatengeneza mikataba hiyo na imeshapitishwa rasmi na imeshasambazwa kwenye taasisi zote za serikali, na hivi sasa watumishi walioko masomoni wote tunawatambua. Na mikataba na masharti kati ya wao na serikali ipo katika mikataba hiyo na mikataba hiyo Mhe. Bikame naomba nikuarifu kwamba ipo tayari kwa kupitia Baraza lako tukufu kama nilivyosema kwenye hotuba yangu.

Wizara ya Afya watumishi hawatoi huduma vizuri sana. Mimi ninakushukuru kwamba umeelewa dhana ya haki na wajibu ni watoto pacha, na katika kulifanya hili basi mimi napokea ushauri wako tutafuatilia. Na napenda nilihakikikishie au niliarifu kwamba sasa kuanzia mwaka huu wa bajeti Mawaziri wenzangu na watendaji serikalini mtakapoona nafanya ziara ya kuzungumza na watumishi msione ninawaingilieni kazi ni wajibu wangu. Kwa sababu na mimi nitakuwa ninajiridhisha katika kuona hayo ambayo tumekubaliana yanapatikana. Saa nyengine tunaweza tukapachikwa majina ya ajabu ajabu kwamba mimi kama Waziri nataka kuangalia mwenendo wa namna ya watumishi hata katika Idara yangu nakwenda kuangalia mwenendo huo pengine mtumishi akaniona ni mtu wa ajabu. Sasa haya inatokana na mazoea tuliyojijengea kwamba wanahisi watu wengine hawawezi kukaguliwa wala kuguswa. Mhe. Bikame ninakushukuru sana.

Mhe. Hamza Hassan Juma mwanafunzi wangu mengi umehitimu vizuri moja tu sikukufundisha lile la kusema kwa ukali sana sikukufundisha, lakini hili linatokana na *nature* ya mwalimu na mwanafunzi, kwamba saa nyengine mwanafunzi anahitimu mengine ambayo mwalimu hana.

Ni jambo la kawaida kwa hivyo wala sikulaumu kwa hii, lakini niliona Mheshimiwa mwanafunzi wangu kadri ulivyokuwa basi ilikuwa sauti inapanda. Matokeo yake hata lile suala la mikataba ya meli zilizosajiliwa sijui linaingia wapi katika Wizara hii nikaona umelizungumza, kwa hivyo ninafikiri ulikuwa ukimuagiza CAG. Kwa hivyo nikuombe Mhe. Hamza kwamba yale yote niliyokufundisha mema endelea kuyafuata na yataendelea kukusaidia katika kutenda

kazi zako na mafanikio ambayo umeyapata mimi nakupongeza sana, umepata mafanikio makubwa mengine umeyaiga kwangu mengine lakini umeyabuni mwenyewe mimi ni shahidi kabisa.

Juzi juzi umepokea kontena la vifaa vya hospitali, kwa hivyo mwanafunzi umeanza kupokea mimi *inshaallah* mwezi ujao na mimi napokea kontena la vifaa. Sasa ungefuata yale tu niliyokufundisha mimi mengine usingeweza kuyafanya. Nakupongeza na ninakushukuru na uendelee na kufuata mafunzo uliyoyapata lakini na yale mafunzo mengine ulokuwa nayo. Umejifunza sana namna gani unachangia ndani ya Baraza ninakushukuru sana nchi mbali mbali umekwenda lakini na mimi ziko fani nimejifunza.

Mimi ni mtu wa *strategy* kwa hivyo ninajua mikakati. Ukitaka nifanye tathmini nitafanya baadae sitaki kufanya leo, lakini mimi pia nimejifunza mambo ya *strategy* na kwa bahati nzuri kazi ambazo nimefanya kwa kutumia ujuzi huo ninafikiri si zaidi ya asilimia tano ndio nimefeli. Kwa hivyo kila mmoja na fani yake na ujuzi wake na namna alivyojifunza.

Kwa hivyo *strategy* najua sana naelewa hiki kinatokana na *strategy*, hiki kinatokana na nini naelewa kwa sababu na mimi nimebahatika kujifunza eneo hilo kidogo. Mhe. Hamza ninakushukuru kwa mchango wako umesema utazuia fungu 47 mimi bado nikuombeni tu kwamba haya mafungu muendelee kuyaruhusu kwa sababu mkiyazuia na hayo mengine yanayohusu mambo mengine hayatafanyika. Mimi ni maridhia sana mimi ni mpole sana. Kama kuna mambo yalitakiwa nitoe ufafanuzi nimejitahidi kwa mujibu wa uwezo wangu lakini kwa kufuata misingi ya sheria na kanuni ziliopo, sikutoa kwa sababu ya utashi wangu.

Lile la *pay roll* nimeshalisema *CAG* kwa mujibu wa Katiba kazi hiyo ni yake ya msingi hahitaji kuagizwa kukumbushwa ni wajibu wake na mimi niko tayari *pay roll* iende ikafanyiwe ukaguzi. Na katika hili serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haitamvumilia muovu yoyote, mimi sitaki nitumie neno la ufisadi. Mimi nataka nitumie neno la mwizi yoyote, kitumbatu mwivi yoyote achukuliwe hatua kwa mujibu wa taratibu na sheria ziliopo. Kama kuna Wakurugenzi wa Ofisi ya *CAG* walihusika wabainishwe makosa yao na wafikishwe kwenye vyombo

vya sheria. Hakuna mkubwa sisi tunapata tabu, tunahangaika tunatafuta pesa, tunagombana wenyewe kwa wenyewe tumuongeze huyu mshahara, tumpunguzie huyu mshahara lakini kama kuna watu pesa hizi wanazitafuna kama ilivyosemwa kila mwenye ushahidi wa mtu anayetafuna pesa hakuna Rais atakayemlinda, hakuna Waziri atakayemlinda wala hakuna mtendaji yeyote yule atakayemlinda.

Kwa hivyo mimi nadhani Mhe. Hamza nikushukuru sana kwa uoni wako huu na mimi utaratibu wa ripoti hizi kuwasilishwa hapa ndani ya Baraza hatimaye tunaikabidhi kamati ya *PAC* inazifanyia kazi. Na hatuishii hapo tunachukua ripoti ile tunai-*submit* kwenye Baraza la Mapinduzi mawaziri wote wanakuwepo. Ni imani yangu kwamba kamati za Baraza la Wawakilishi ni kamati za kisekta tunao sisi wajibu kukaa na mawaziri na mawaziri kuchukua hatua kama itakuwa imebainika ubadhirifu kwa mtendaji yoyote yule. Kwa hivyo mimi siwi sehemu ya kulinda uovu. Maana adhabu zinapotokea unaweza hakimu au Jaji akakuhukumu kukufunga, akakuhukumu kutoa faini, na anaweza akakuhukumu kutumikia adhabu zote ambazo yeye ameamua azifanye.

Sasa moja kati ya adhabu ambayo ninaiogopa ni kuambiwa lipa, tumeshuhudia watu wamekufa vihoro, kwa sababu wamejihusisha na mambo wakajiingiza na hatimaye anafika pahala anaambiwa alipe kibanda chake kinauzwa mashaka yanabaki kwa warithi na hatimaye hakuna faida inayokuwa imepatikana. Kwa hivyo nitoe wito kwa watumishi wa umma wote wawe kwa *CAG*, wawe Ofisi ya Rais Utumishi, wawe Wizara ya Elimu wawe popote wafuate maadili ya uaminifu ili wasinyakue nyakue fedha za umma, na kwa yule ambaye atabainika sheria ichukue mkondo wake. Hakuna mtu ambaye anaweza akamkinga mtu kwa maovu, nalisema hapa mchana kuzimu hakuna nyota.

Mhe. Hamza ninakushukuru kwa kukumbusha hilo na kama nilivyosema mwanzo kuna mwahala mwengine kuna unuko, kule kwetu Tumbatu kuna *grade* ya huu unuko, likitoka kwenye unuko kuna uvundo. Sasa mimi nithibitishe kwamba sitakaribisha uvundo licha ya unuko, uvundo pia sitoukaribisha, kwa hivyo mimi nadhani nimekusikia sana. Mhe. Hamza ninakushukuru.

*Website* ya SMZ haipo kwa sababu ya Baraza hutakiwi useme kitu ambacho huna uhakika nacho. Mimi hili naomba nili-*reserve* na nikuletee kwa maandishi baada ya kufanya utafiti. Nikiri kusema kwamba hili sijalifanyia utafiti. Lakini nia na madhumuni ya kuwepo *E-Government* ni yale ambayo niliyaeleza kwenye hotuba yangu. Wajumbe wamezungumza kwa hisia kali sana na kutaka iundwe Tume Teule ya kuchunguza jambo hili.

Kama mwaka jana mtaangalia *hansard* zangu wakati linaulizwa swali hili, nilisema mimi sioni tatizo la kupewa *break down* ya matumizi ya jambo hili. Lakini kwa sababu jambo hili halikuratibiwa na Wizara yangu ijapokuwa mawaziri tunawajibika kwa pamoja ndani ya Baraza natambua wajibu huo, mimi nisingependa nikatoa kauli ya kukubali kuunda Tume. Kwa sababu fedha hizi hazikusimamiwa chini ya Wizara yangu, *actually* fedha hizi ni za mradi wa *E-Government* kwa maana ya kutandika mkonga pamoja na ku-*install* mashine pale kwenye kituo chetu.

Kwa hivyo mimi nadhani pahala pa kuweza kulihoji hili Mhe. Ismail ambapo Wajumbe walikuunga mkono na Mhe. Salmin kama aliliunga mkono na yeye kama Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha bahati nzuri Wizara hii iko chini ya Kamati yake. Sasa maamuzi mimi hili nitashindwa kulitolea kauli lile la kwamba iundwe Kamati Teule lakini itapokuja Wizara inayohusika na hili lihojini mtapata majibu. Mwaka jana nilisema hivyo na leo nataka nirejee hilo, mkitaka mimi nitoe kauli ya kuunda Tume wakati hili jambo sikulisimamia mimi nimepewa kuendesha *system* ya *E-Government* ndio kazi ambayo nimepewa mimi.

Sasa masuala ya matumizi na ghasia wala simrushii mwenzangu paka wa uso katika hili hapana, tumegawana majukumu, na kama tumegawana majukumu basi kila hoja ipelekwe kwenye taasisi inayohusika. Nikilisemea mimi hili nitakosea sana na sitawatendea vizuri wenzangu.

Niiombe sana Mhe. Hamza hili na wale wengine wote waliolichangia walipeleke kwenye Wizara inayohusika. Mimi ninahusika na uendeshaji wa serikali mtandao, mwenzangu miundombinu anaendesha na anasimamia uangalizi wa mtandao wenyewe

tumegawana majukumu, na Mratibu aliyeshughulikia hili na aliyesimamia yupo, kwa hivyo mimi nadhani tuelekee huko *nataasaf* kusema hili Mhe. Hamza na Waheshimiwa wengine na Mhe. Jussa, ambaye ndio umelianza hili.

Niombe radhi sana rafikri yangu kwamba hili nisilitolee maelezo mimi ninaweza nikalikosea, kwa sababu sina taarifa sahihi juu ya jambo hili. Ukiniuliza ni kwa nini bilioni moja na bilioni mia nne hatukukusanya ni sababu kwamba mkataba kati ya Serikali na *Zantel* ulichelewa kusainiwa na lazima tujue kwamba mikataba hii inayohusu masuala ya fedha inaratibiwa na kusimamia na Wizara ya Fedha.

Mimi nilikuwa ni kama sekta nilopewa jukumu la kukusanya, lakini kabla ya kukusanya kulikuwa na makubaliano kwanza yafanyike kati ya Serikali na *Zantel* ambao kwa mujibu wa mkataba uliosaniwa wanahusika na mambo ya uunganishaji wa Taasisi zote za Serikali katika kukamilisha mawasiliano ndani ya Serikali. Kwa hiyo hili Mhe. Hamza ulilizungumza na Waheshimiwa wengine walilichangia naomba majibu yangu yawe hayo.

Mhe. Spika, madereva nao wapewe maposho wanakaa mpaka saa 7 ya usiku. Kwanza maposho wamepewa madereva wote wa Mawaziri na juzi ilipokuja hoja kwenye kifungu cha Baraza la Mapinduzi hata kile chakula sisi tukila mle ndani na wao wanakula. Kwa sababu nitoe hadithi moja kuna mkubwa mmoja zamani palikuwa na dhifa pale *People's Palace* wakapata mambo pale vinono na nini, lakini madereva wako nje, yule dereva tokea asubuhi mpaka saa hizo walizotoka usiku dereva hajala, kwa hivyo wakashauriana pale wakaamua kufanya uhuni. Akachomoa mpira wa petroli akahakikisha mafuta yale yaliomo kwenye ile *system* yatamfikisha angalau V.I.Lenin, wakati ule V.I. Lenin lakini sasa hivi Mnazi Mmoja Hospitali. Lakini mafuta yale yalimuwezesha kutoka *People's Palace* mpaka Posta ya zamani, pale gari ikaanza kuzima zima, sasa nini kilichotokea, bosi akalazimika kusukuma gari mpaka Gofu yule dereva yumo ndani, sasa kufika pale Gofu yule mkubwa bahati nzuri alikuwa na nafasi kwenye vijana wetu hawa, sasa wakashughulika wakaona yule karoa amenyeshewa mvua ya masika, wakatoka vijana waliopo Gofu pale wakaamua kumsaidia, yule akawa anahema tu, mpaka kufika kwenye Msikiti ule pale Gofu akawaambia wale wenzake, jamani mimi nimefanya hivi kwa sababu

mimi binaadamu tokea asubuhi sijawaona wanangu, sijamuona mke wangu, lakini ile chai sijapewa na watu kule wamekwenda kula lakini sisi hatukupewa.

Mhe. Spika, kwa hiyo sisi Serikali hatuwezi tukawadharau madereva, kwa hiyo kwa upande wa maslahi kule kidogo kipindi kilichopita tuliwaangalia. Sasa suala jengine aloliongeza ambalo ni jema la kuhakikishwa kwamba kila dereva anapata Vespa hilo naomba nilichukue na twende tukalizungumze Serikalini ili tuone kama uwezo ukiruhusu tunayo haki ya kuwafanyia madereva wetu wema.

Na mimi ninathamini sana kazi ya dereva, nataka nitoe *challenge* mtizame dereva wangu ukitokea ghafla kati ya Waziri na dereva huwezi kumjua nani. Tunatakiwa tukae nao watumishi wetu sio watumwa wala watwana, ni mgawanyo tu wa kazi kwamba yeye amekuwa dereva mimi nimekuwa Waziri. Na mimi vile vile kwa kuyaelewa haya dereva wangu akifika nyumbani hatoki na gari ya Waziri lakini anatoka na gari yangu, ikiwa hujasifiwa jisifu mwenyewe. Nnachokula mimi chakula na yeye anakula, sio mimi nakula basmati yeye anakula mapembe, huo ndio uungwana nakushukuru sana Mhe. Hamza kwa kutukumbusha hilo.

Mhe. Spika, Mhe. Hija Hassan Hija, ndugu yangu Mtumbatu mwenzangu, nakushukuru kwa maoni yako sana uliyoyatoa kuonesha kukerwa kwako na matatizo, umeunga mkono suala la kuunda tume ya *E - Government* maelezo nimeshayatoa.

Ofisi ya Kadhi ifanye uchunguzi wa *pay roll* nimesharuhusu lakini katiba bila ya kuambiwa na mtu yeyote inamtaka afanye hivi. Huungi mkono fungu 47 na mimi nitumie busara za kukuomba uliruhusu fungu 47. Tumemuomba Kadhi huo ndio uungwana, ukimkosea mwenzio lazima kama ni muungwana umumuombe radhi na huo ndio uungwana wa Kitumbatu. Mimi kama kuna mtu nitamkosea sichukui sekunde moja nitamuomba radhi, lakini kama na mtu atatokea amenikosea busara zinaonesha na yeye aniombe radhi.

Kwa hivyo mimi nakushukuru sana ndugu yangu kwa kumuomba radhi kwa sababu umejua kwamba ulivyokuwa ukimfanyia Kadhi haikuwa vizuri, sasa mtu kujifunza ndio ubinaadamu ulivyo, na

tukitoka hapa tusirudi nyuma twende mbele tujenge misingi ya kuaminiana na hatimae tufike pahala pazuri.

Mhe. Spika, tumezungumzia pia maslahi ya watumishi wa ofisi muhimu chungu nzima, umeungana na wenzio, nikushukuru sana kwa hilo nishalitolea ufafanuzi kwamba Serikali itahakikisha ofisi hizo muhimu kulingana na hali ya uwezo wa Serikali utakavyokuwa.

Mhe. Spika, ofisi zinapigwa vita, hakuna ofisi inayopigwa vita. Ofisi zilizo chini ya Wizara yangu mimi natoa *challenge* muende mkafanye utafiti wa kutosha juu ya yale ambayo umeyazungumza jana nitajua kama wanapigwa vita au kuna mgongano tu wa mawazo wa kutoelewa majukumu yepi ni ya nani na majukumu yepi ni ya nani, tukishafikia hapo hatuwezi kuwa na lugha hizi.

Na mimi kama nilivyosema asubuhi Mhe. Spika, ulivyoniruhusu namuomba Mwenyezi Mungu anizidishie busara na hekima na naelekea kibla, na kama mimi nimewahi kufanya hilo nakwenda *minbar* Mungu anihukumu, maana huko mnaweza mkenda Mahakamani ukawa na wakili mzuri hata kama umefanya kosa ukashinda kesi, inategemea uhodari wa wakili wako, lakini *minbar*! Na mimi nataka nikwambieni hata nafasi hii niliyonayo nilikabidhiwa na wazee wa Tumbatu juu ya Msikiti kwamba tunakutaka ututumikie, nathamini sana imani waliyonipa wazee wale na hatimae wananchi kwa jumla wanaendelea kuniamini katika kipindi cha 4, kwa sababu ya *Allah* tu si jambo jengine.

Mhe. Spika, kuna rafiki yangu mmoja wakati wa uchaguzi alioneshwa pete na mgombea mwenziwe, unajuwa kuna pete hizi zinakuwa na vito, sasa yule mwenzangu kumbe alikuwa mwoga alivyoonyeshwa ile pete akaona sasa hapa siwezi kwenda kugombea. Nataka niwahakikishie kwamba mimi sina pete za mikono wala miguu ninamtegemea *Allah Subhana Wataalla*, na imani niliyopewa na wananchi wangu na wazee wangu wa Tumbatu na huko waliko wananisikia. Wamefadhaishwa sana na jinsi nilivyokuwa naonekana nafanya mambo kinyume na makubaliano niliyokubaliana nayo. Naomba kwa hili niishie hapo kwa sababu nahisi kama sikutendewa haki katika hili, lakini ni vizuri sisi kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tukisema jambo tulifanyie utafiti wa kina, mimi niko

huru, kamati hizi ndio zinazotusimamia na kutuchunguza iende ikaangalie, kama kuna chembe ya kuingilia isipokuwa kutekeleza wajibu wangu na majukumu yangu niliyakabidhiwa kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Spika, mengine yanajirejea rejea na Mhe. Salmin, Mnadhimu wangu na yeye alianza kwa kutoiunga mkono. Mhe. Salmin Awadh Salmin, siwezi kusema ni jambo la ajabu kwa Mnadhimu wa *CCM* ambaye Chama chake kinaongoza nchi akaanza akawa ndio wa mwanzo kutoiunga mkono hoja, alikuwa na sababu zake na hisia zake na demokrasia katika uendeshaji wa chombo hichi. Nakupongeza sana Mhe. Mnadhimu kwa kazi nzuri ambayo umeifanya ya kuonesha nia ya kuwatumikia wananchi wa Jimbo lako na wananchi wa Zanzibar. Nakuomba uendelee na moyo huo utusimamie, utukosoe na hatimae na sisi tunaokosolewa kama yapo makosa tukubali kwamba tumekosea na huo ndio uungwana, huo ndio uungwana niliofundishwa mimi na nafikiri uungwana wa kitumbatu na wa kimakunduchi haupishani wala hauhitilafiani.

Mhe. Spika, ilinukuliwa hotuba ya Mhe. Rais, kuhusu namna Kamisheni inavyokwenda *against* na maelezo ya Mhe. Rais, alipolizindua Baraza lako tukufu. Mimi nataka niseme Mhe. Spika, wewe shahidi, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais wewe shahidi, namna Mhe. Rais, anavyoendelea na kutaka kutekeleza azma na madhumuni yake na malengo yale yaliyotokana na utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi, ahadi zake alizozitoa wakati wa kampeni zake za uchaguzi kwa kuzingatia mipango ya kitaifa katika kutekeleza *MKUZA II* na mipango ya *millenium* na kuridhia mikataba ya kikanda na kimataifa, na kwa kunukuu sisi sote mimi nataka nikuhakikishie Mhe. Salmin, nilioingia kama Waziri, watendaji hebu simameni huko (Makofi). Kila mtendaji nilimkabidhi ilani ya uchaguzi, katiba ya nchi, sheria na hotuba za Mhe. Rais, hotuba ya mwanzo aliyoitoa Baraza la Wawakilishi na naomba niseme kwamba watendaji wangu nawapenda sana na wananipenda sana, wamekuwa wakiniliwaza Mheshimiwa pole, nawaambia ndio kazi ilivyo, ndio *challenge* na nikawaambia ndio mjue sasa ninapowekwa kikaangoni kule nyie hamuwezi kusema nasema mimi.

Mhe. Spika, nataka nimuhakikishie Mhe. Salmin kwamba watendaji wangu wanajua hilo, kwa sababu hotuba ile ya mwanzo ya Baraza la Wawakilishi na hotuba ya Sherehe za Mapinduzi ya mwaka 2011 zote niliwakabidhi watendaji wangu wote pamoja na maandiko mengine. Kwa hivyo ulipokuwa unanukuu nikasema *alhamdullillahi* ananikumbusha mbali. Kwa hiyo nakushukuru kwa kunukuu na watendaji wamesikia kwamba tunatakiwa ulichonambia wewe tunachujua kukifanya ni yale ambayo Dkt. Shein, ameyasema na kuwaahidi wananchi na ukasema utaondosha shilingi mia. Mnadhimu wangu nirejeshee, (makofi) sijamaliza mchango wako wa Chama wiki hii, nataka kumaliza mchango kwa hii shilingi mia, ukiitoa itanipa dhiki katika kukamilisha mchango wa kukijenga Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Spika, Mhe. Marina nakushukuru mchango wako zaidi ulikuwa kushauri na mengine nimeshayatolea ufafanuzi.

Mhe. Mohammed Haji Khalid kwa sababu ya muda na mimi vile vile nasema mchango umenisaidia sana katika kunikumbusha, pongezi kwa watendaji nazipokea na mambo mengi mliyoyasema yanajirejea, lakini ulisema enzi zako ulipokuwa mwalimu ulikuwa unajua ngazi na vigezo ulikuwa unajua anayekufuata chini anajua mwaka gani ndio maana ya *scheme of service*. Hayo unayoyakumbuka wewe ambayo katika kipindi kirefu yalikuwa hayafanyiki, sasa ndio hayo tuliyokuja nayo. Kwa hiyo ni imani yangu kwamba tutaendelea kufanya kazi hizo kwa mujibu wa taratibu na sheria.

Jengine ambalo ni suala la wafanyakazi kuwazingatia kwa mujibu wa kada zao nimeshalisema na *scheme of service* kuzingatia nishasema, maslahi ya watumishi hili lilisemwa na wengi vile vile.

Mhe. Asha Bakari kuhusu ujenzi wa jengo, mimi nilipoingia Wizara hii ya Utumishi kwa kuelewa umuhimu wa pande zote mbili za Zanzibar nilipeleka mapendekezo ya kutaja kununua jengo la ofisi kule Chake Chake Pemba, Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala wanakumbuka, bila ya kujali kwamba hapa sina ofisi lakini nilijua pia kwamba na kule ninahitaji kuwa na ofisi.

Kilichonisitisha kwamba kwa sababu Serikali ina mpango wa kujenga majengo yake mapya tukakubaliana kwamba tusijiingize katika kununua majengo na twende na mpango huu wa kujenga majengo ya ofisi za Serikali.

Kwa hiyo nataka nikuhakikishie kwamba Serikali imeanza na mimi nilihakikishie Baraza lako tukufu kwa Unguja na Pemba utaratibu ni ule wa Wizara mbili mpaka tatu zinakaa kwenye jengo moja, mpango huu ni endelevu Mwanasheria Mkuu karibu jengo lake litamaliza, ZRB lishamaliza, Katiba na Sheria karibu wanamaliza na sisi Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi mwaka huu wa bajeti tutaanza ujenzi wetu hapa na kule Pemba mipango inaendelea.

Mhe. Spika, hii tunaifanya kwa makusudi kwa sababu pale *State House* tunataka tumuache Rais na *private office* yake, tuliobakia sote tutoke tufanye kazi zetu nje ya ofisi. Kwa hivyo Mhe. Asha nakuhakikishia kwamba tutakavyofanya shughuli hizi tutafanya sambamba na Pemba na kwa mpango ule Serikali utakuwa umeuamua na huo wa kujenga jengo moja kukaliwa na ofisi zaidi moja.

Mhe. Spika, ilitoka hoja kwamba ajira zinatolewa na Mawaziri, haidhuru vifungu vilivyotolewa Mhe. Spika, lakini aliyetoa hoja hayupo, na ikatolewa hapa mfano kwamba na sisi tupewe, utaratibu unatukataza wa kugawana nafasi kwa mujibu wa sheria, lakini bahati mbaya kilizungumzwa kifungu cha Idara ya Uendeshaji na Utumishi ambacho kinazungumzia uajiri wa Wizara, lakini ule uajiri wa nafasi nyengine zote kwenye utumishi wa Baraza ni Tume ya Baraza inahusika. Utumishi wa Mahakama Tume ya Mahakama inahusika, utumishi Serikalini Tume ya Utumishi Serikalini inahusika, Idara Maalumu Tume ya Utumishi Idara Maalum inahusika. Kwa sababu sikupata uchambuzi na ufafanuzi wa kina juu ya Tume gani inazungumzwa napenda niseme kwamba hili nimeshindwa kuweza kujua hasa ukweli wa jambo lenyewe ukoje.

Mhe.Spika, nafasi za ajira na hili pia lilizungumzwa na Mhe. Jussa, na akatoa hoja yake kuhusu kijana ambaye nimepata, nakubaliana naye na mimi nimuombe Mhe. Jussa tuijue hiyo taasisi aliyokwenda kufanya *interview* na Tume aliyofanyiwa *interview* na ilikuwa Wizara gani,

kwa sababu maadili pia yanakataza kumwambia mtu wewe nambari *one*, sasa hatumuhukumu lakini tutafuatilia kama kweli sifa alizofanyia *interview* ya *oral* na *writing* alipata *first class*, basi sheria yetu inasema ikitokezea jambo kama hili basi malalamiko yanatakiwa yapelekwe kwenye taasisi zinazohusika na kabla ya miezi mitatu baada ya kufanyika hilo jambo uajiri wote inabidi usimamishwe tuanze *process* ya uajiri mpya. Kwa hiyo usimtaje hadharani umefanya vizuri sana kwa sababu ya kutaka kumchonganisha, lakini niletee tufuatilie kwa pamoja halafu tutapata *result*, nikuombe sana Mhe. Ismail.

Mhe. Spika, kwa lile ambalo lilizungumzwa na Mhe. Mshimba nataka nihakikishe mimi sijawahi kupokea orodha nikaipeleka kwenye Tume yoyote ile kwamba hawa waajirini. Sasa Mawaziri hawajawahi kuniletea orodha hizo, sasa kama wamepeleka moja kwa moja hilo inabidi nalo nilifanyie utafiti ili niweze kujiridhisha na suala hili.

Mhe. Spika, baada ya hayo siwezi kuyasema machache ni mengi mno, lakini nimetumia muda mwingi kutoa ufafanuzi, na kama utaona watu wachache waliochangia lakini mchango wao ulikuwa mzito sana. Mchango wao ulikuwa mzito na ulikuwa wa maana wenye lengo la kuweza kutusaidia, kutukosoa na kutuelekeza na kutushauri. Nataka niwahakikishie wale wote ambao sikupata nafasi ya kutoa ufafanuzi wa hoja zao na bila ya kusahau wale waliochangia kwa maandishi kwa haraka haraka, imezungumziwa masuala ya ripoti ya mdhibiti, ripoti ya haki za binaadamu na ripoti ya utawala bora.

Mhe. Spika, nataka nithibitishe kwamba ripoti ya utawala bora tayari nimeshawapelekea viongozi wetu wakuu wa kitaifa kwa kuiona na nitaomba nafasi kama utanipa katika mkutano huu baadae nije kuwasilisha ripoti ya haki za binaadamu na vile vile ripoti ya utawala bora ya mwaka nitaomba nafasi kama utaniridhia nitaiwasilisha katika kikao hichi sambamba na ripoti ya Kadhi kwamba kama iko tayari mimi sina tatizo ripoti hizo nitaziwasilisha iwapo Mhe. Spika, utanipa ridhaa ya kuwasilisha kwenye mkutano huu.

Baada ya kwishasema hayo naomba Wajumbe muikubali bajeti yangu ya Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ili yale mliyoyachangia na mengineyo nipate wasaa wa kuweza kuyatekeleza. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

**Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko**: Mhe. Spika, naafiki.

**Mhe. Spika**: Tunakushukuru sana Mhe. Waziri, kwa majumuisho hayo ilikuwa muda mrefu sana pengine tafauti na hotuba nyengine zote huko nyuma, na hii ni kwa sababu nilikuwa nafuatilia mjadala huu kwa karibu sana na hayo uliyosema mazito yalikuwepo na mimi niliyakuta na mengine tumekuwa tunayafanyia kazi hapa jana saa 5 za usiku.

Na mimi niliingia kazini vile vile, ili kuona kwamba mambo yanakwenda vizuri, kwa sababu nia ni kuwa mambo yetu yaende vizuri sana. Kwa hiyo nakushukuru sana kwa majumuisho hayo ambayo umeyatoa na sasa Waheshimiwa Wajumbe niwahoji basi, wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri ya makadirio ya mapato na matumizi kwa Wizara hii ya Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka 2013/14 wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda (Makofi).

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Spika**, Waheshimiwa Wajumbe kuna nusu saa na kazi mliyofanya leo ni kubwa sana, nafikiri tukapumzike. Unajua hata kama kazi kubwa zaidi aliyoifanya sasa hivi Mhe. Waziri, lakini mapumziko haya yamjumuishe na yeye Mhe. Waziri, kwa hivyo niombe rasmi nimuombe Mhe. Waziri, atuwekee utaratibu ili tuje jioni saa 11 kwa ajili ya kuendelea na kupitisha vifungu vya makadirio ya Wizara hii.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora, amemaliza kufanya majumuisho ya Wizara yake, na kwa kuwa kutakuwa na kazi ya kamati ya mapato na matumizi kwa ajili ya kupitisha mafungu, na kwa kuwa muda tulionao hautoshi kufanya kazi hiyo kwa usahihi na kwa busara, kwa hiyo niliombe Baraza lako tukufu tuweke kanuni ya muda kando kwa nia ya kuliakhirisha Baraza lako tukufu hivi asubuhi na likutane tena jioni hii saa 11 kwa kufanya kazi zilizomo katika *order paper* ya leo.

**Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko**: Mhe. Naafiki

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe niwahoji wanaokubaliana na hoja wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Saa 6.30 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni leo)*

*(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)*

*(Majadiliano yanaendelea)*

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora:** Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza lako limejadili na kukubali hotuba ya bajeti ya Wizara ya Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora, sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kuvipitisha vifungu vya matumizi vya wizara yangu. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

## KAMATI YA MATUMIZI

## KUAHIRISHWA BARAZA KUTOKANA NA KUTOTIMIA *QUORUM*

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe nadhani turejeshe Baraza kidogo naona idadi ya Wajumbe waliopo humu ndani ya ukumbi haituwezeshi kupitisha matumizi haya. Hebu tuhesabu tuone kama kuna *quorum* tufanyie kazi, kama kuna Wajumbe nje hebu waingie haraka.

Waheshimiwa Wajumbe inaonekana idadi ya Wajumbe waliomo ukumbini haikutimia ili kuweza kufanya maamuzi ya shughuli zetu jambo ambalo ni muhimu sana. Kabla ya kuahirisha kikao kwa muda nataka nitoe maelezo yafuatayo:-

Waheshimiwa Wajumbe sote tunaelewa tuna shughuli nyingi sana, lakini inapofika wakati wa vikao tunapaswa kabisa kuzingatia

umuhimu wa vikao vyetu, si utaratibu, haielekei, si vyema, ni aibu mbele ya wananchi kwamba Wawakilishi waliotumwa na wananchi kuja kufanya kazi kwa ajili yao ionekane mapengo matupu namna hii, kiasi cha kufika pahala tuwe tunaahirisha kikao kwa ajili ya kuwasubiri wajumbe, huu si utaratibu.

Tunajitahidi sisi tunaokaa hapa juu ya meza pamoja na watendaji wetu haijatokezea hata siku moja kufika pahala tukachelewa hata kwa dakika moja, utamkuta Spika na watendaji wapo, nastaajabu leo Wajumbe mnaowakilisha wananchi mnakuwa mnachelewa ovyo ovyo namna hii. Huu si utaratibu na naomba nichukue nafasi hii kukemea sana kabisa juu ya utovu wa nidhamu wa aina hii kwa kutohudhuria vikao kwa wakati. Vikao vyetu tunaelewa vinaanza saa tatu asubuhi hadi saa saba na kuanzia saa kumi na moja jioni hadi saa mbili kasorobo usiku, ndio maana inapofika wakati kwamba shughuli zetu hazijesha huwa hoja maalum inatolewa ili kuhakikisha tunaweka nidhamu ya utaratibu wa kanuni, inapofika hivi kwa kweli inatufikisha pahala pazito, pagumu na mbele ya macho ya wananchi haioneshi ile tunayoitaja wakati wote *seriousness* ya vikao vyetu.

Waheshimiwa Wajumbe nakuombeni sana nitakuwa nachukua hatua kwa mujibu wa kanuni wale wanaochelewa tuchukue hatua za kinidhamu kwa mujibu wa kanuni zetu. Jambo hili ndilo linatufelisha katika shughuli zetu nyingi kwa sababu imekuwa hatuna nidhamu ya kuhudhuria vikao kwa wakati wake.

Makatibu, watendaji mpige kengele kwa muda kama kanuni inavyoelekeza wa dakika tano na basi nichukue nafasi hii kuahirisha kikao hiki kwa muda ili kuwasubiri Wajumbe wasiokuwa na nidhamu waingie.

*(Saa 11:07 Baraza liliahirishwa kutokana kutotimia quorum)*

*(Saa 11:13 Baraza lilirudia)*

## KAMATI YA MATUMIZI

## FUNGU 11 – OFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZANZIBAR

Kifungu 0201 Utawala Unguja 15,000,000/-

**Jumla ya Fungu**

**15,000,000/-**

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitisha na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

## FUNGU 11 – OFISI YA MDHIBITI NAMKAGUZI MKUU WA HESABU ZANZIBAR

Kifungu 0201

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Mwenyekiti, *Bismillahi Rahmani Rahym* nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa hoja niliyoileta na kufanyiwa kazi na wale niliowasema kuwa wamesimamishwa kazi wamerejeshwa na nashukuru kwa hilo. Sikupiga buti kwa dhana ya kumkomoa ila nimepiga buti kumpongeza na lakini kilichobakia ni yale mafao yao naomba wasaidiwe wale watu kama walivyorejeshwa kazini.

Mhe. Mwenyekiti, nishukuru kwa hilo kwa utendaji mzuri. Ahsante sana.

Kifungu 0201 Utawala Unguja 1,339,477,000/-
Kifungu 0301 Ofisi Kuu Pemba 571,523,000/-

**Jumla ya Fungu**

**1,911,000,000/-**

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitisha na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

## FUNGU 44 – OFISI YA RAIS UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA

Kifungu 0101 Idara ya Utawala Bora 216,504,000/-
Kifungu 0111

**Mhe. Ismail Jussa Ladhu:** Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu nilizungumzia suala zima ambalo limo katika hotuba ya waziri ukurasa wa 68 maendeleo na maslahi ya wafanyakazi.

Katika mchango wangu nilizungumzia suala la kwamba wakati akiwasilisha bajeti kuu ya Serikali Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo alitwambia kwamba serikali imekusudia kuongeza maslahi ya wafanyakazi na kwamba maelezo yake kwa undani tungeyapata katika bajeti ya Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu nilisema kwamba nilisikitika kuwa katika sehemu hiyo niliyoitaja ya hotuba yake bado maelezo yaliyokuwepo ni ya jumla. Katika kujibu hoja Mhe. Waziri nimemsikiliza kajibu hoja yetu moja kimsingi sina tatizo nalo sana, ingawa pia napingana naye katika taratibu fulani aliposema kwamba imeonekana si vizuri kutangaza kiwango cha nyongeza kwa sababu mara nyingi inapelekea katika muda mfupi gharama za maisha hupanda kwa kuongezeka bei za bidhaa.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, mimi ninavyodhani ni kwamba ni utaratibu uliojengeka dunia nzima kwamba kima cha chini huwa kinaeleweka, takriban nchi zote zina kawaida ya kutangaza kitu kinachoitwa kima cha chini. Hata mwaka juzi yalipokuja marekebisho ilifanyika hivyo. Sasa Mheshimiwa mara hii tunapata shida sisi kama wapitishaji masuala haya kwamba hatukupata hata mwelekeo wa jumla, na ninaliuliza hili Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu moja ile ambayo baadhi ya wajumbe pia waliizungumza kwamba katika bajeti ya Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ukurasa wa 112 wa kitabu hiki hiki tunachokizungumza, hapo kuna fungu la marekebisho ya mishahara ambalo limekuwa ni kawaida, kila alipotaja pana marekebisho kwamba kwa mwaka huu kumetengwa bilioni 17 na 500 milioni.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nasema kwamba angalau hata vile viwango vyengine havitajwi kima cha chini tungetajiwa kitapangwa kiasi gani, lakini na baadae ile *formula* au utaratibu utakaotumika kuongeza maslahi kwa wengine tukaujua. Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu katwambia na mimi katika hilo nampongeza kwa sababu katika

mchango wangu nilisema kwamba nadhani kwa huku juu tena kwa sasa inatosha. Lakini alisema hayatawahusu kuanzia Wakurugenzi lakini zaidi yatawahusu kuanzia chini ya Wakurugenzi mpaka kufikia kima cha chini. Sasa nilikuwa nasema angalau atusaidie basi wakati tunapitisha fungu hili atuongoze kwamba nini yatakuwa msingi wa *formula* ambayo italenga katika kuboresha maslahi ya wafanyakazi wetu, naomba sana Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nimpongeze sana Mhe. Ismail Jussa, ni kweli wakati alipochangia ali-*raise* hoja hiyo na mimi wakati wa kufanya majumuisho nilisema ni kwa nini. Lakini *formula* gani tunayotaka kuitumia kama nilivyosema kwenye hotuba yangu ya bajeti kwamba kwanza tutazingatia vigezo vilivyotokana na *scheme of service* ambavyo vinazingatia elimu, uzoefu.

Kama watakumbuka Waheshimiwa Wajumbe kwenye marekebisho tuliyoyafanya mwaka 2011 Oktoba hatukuwazingatia sana hawa ambao elimu zao ni ndogo, lakini wana uzoefu mkubwa sana na wametumikia sana nchi hii, na wanaendelea kutusaidia sana. Kwa hivyo, *formula* tutakayotumia ni zile *scheme of services* na vigezo vitakuwa vya elimu, vitazingatia kada maalum lakini pia vitazingatia watu wenye uzoefu.

Lakini jengine ndio maana nilisema kwamba serikali inataka ihakikishe kima cha chini cha safari hii kisiwe kidogo kama kile tulichotoa mwaka 2011. Kwa msingi huo, mimi najua kwa kuzingatia kada na uzito wa taasisi, zipo taasisi kima cha chini cha kuanzia ni shilingi 125,000; zipo taasisi kima cha chini kwa kuanzia shilingi 135,000; ziko taasisi kwa kuanzia shilingi 155,000. Ninachotaka kusema viwango vyote hivyo tutahakikisha tunavipita ili watumishi wetu waweze kufaidika. Tulipo si pabaya na ndio maana pale tulipopata wazo la kuona kwamba hebu tuangalie, tukijiondoshea sisi, kwa maana ya serikalini naomba nieleweke hivyo, nieleweke vizuri kabisa, hivyo hatuwezi kuwasaidia watumishi wetu wa kima chini katika kunyanyua hali zao. Zoezi linaonesha tunaweza tukawasaidia na wakafurahi zaidi kuliko walivyofurahi mwaka 2011.

Kwa hivyo, Mhe. Ismail Jussa naomba uniruhusu kwamba naielewa *concern* yako kwamba lazima tuwe na cha kuanzia. Lakini katika kuzingatia yote hayo ya kujiondoshea sisi vinono tukawaangalia watu wa chini kile ambacho tunajiondoshea sisi pengine kinaweza kikaongezeka maradufu zaidi ya kile ambacho tulichokuwa tumekiona baada ya kufanya mahesabu yetu.

Hivyo ningemuomba Mhe. Ismail atuachie tuendelee kulifanyia kazi jambo hili na wafanyakazi wetu hasa wa kima cha chini waendelee kufaidika na zoezi ambalo tutalifanya. Ahsante sana.

**Mhe. Ismail Jussa Ladhu:** Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa maelezo ya Mhe. Waziri na pamoja na hayo aliyoyaeleza naomba aniruhusu ninukuu sentensi moja tu katika hiyo sehemu anayoizungumzia ya ukurasa wa 69.

Inasema kwamba, "Aidha, kada ukiondoa ile ya wafanyakazi wenye uzoefu waliotumikia kwa muda mrefu", lakini pia inasema "Aidha, kada adimu zitapewa uzito unaostahiki, wataalamu wa kada hizo waweze kupata moyo wa kufanya kazi katika taasisi hizo na kujiendeleza zaidi na kama nilivyotangulia kueleza marekebisho hayo itakuwa katika toleo maalum litakalokuwa na muongozo wa marekebisho".

Sasa Mhe. Mwenyekiti, katika ufafanuzi wake ni bahati mbaya sana kwa sababu kawaida katika vifungu hatupaswi kuingia katika haya, lakini kwa sababu hotuba yake haikuwa wazi inabidi tutake maelezo ili tujiridhishe kabla hatujapitisha mafungu hayo. Kagusia hayo nilikuwa nataka pia tuweze kufahamu kwa sababu katika mchango wangu katika mfano mmoja nilioutoa nilizungumzia madaktari. Tunazo taarifa kwamba madaktari walifika kutishia kugoma na Waziri wa Afya baada ya kupeleka miundo yake akawahi kusema kwamba atagoma nao kwa sababu hapewi ufumbuzi kutoka katika Kamisheni ya Utumishi wa Umma sijui ama wizara. Sasa mimi nataka nisaidiwe hili.

Mhe. Mwenyekiti, zaidi anihakikishie tu basi kwa sababu sitaki niweke mjadala anihakikishie tu kwa sababu sasa hivi inakuwa ngumu kupitisha *formula* ambayo hatuijui, Baraza linaambiwa itakuja baadae

katika muongozo kwamba yale makosa yaliyojitokeza mwaka juzi hatutayaona mara hii.

Mhe. Mwenyekiti, mwaka juzi watu walilalamika sana kwa sababu ufahamu wa watu walipoambiwa kwamba mishahara inaongezwa kwa kiwango cha asilimia 25 kwa kima cha chini na kutokakana kwa uwiano ambao unalingana na maslahi yao, wengine walifika wakasema wameongezewa shilingi mia mbili, wengine shilingi mia tano, wengine shilingi elfu moja na wengine hawakuongezewa kabisa na wengine wakasema baada ya hayo marekebisho kuzingatia viwango vya elimu walikuja wakapunguziwa. Sasa hapa malalamiko yalikuwa mengi huko nje. Sasa nataka anihakikishie hayo kwa sabahbu chombo hiki kinachosimamia serikali kinapaswa kijiridhishe na hayo ili kiruhusu fungu hili la matumizi liendelee.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, ni matumaini yangu kwa sababu tulitoa wito na akaukubali alipokuwa anafanya majumuisho kwamba kuna tatizo zima la *pay role* na akasema kwamba hana tatizo kama waziri kumruhusu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa sababu ni wakati wa kazi zake za kikatiba kwenda kufanya ukaguzi wa *pay role* yote, kwamba hizi shilingi 17 bilioni na 500 milioni zilizotengwa zitakwenda kutumika kwa kazi ambayo imekusudiwa. Nilikuwa naomba maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, lile la mkaguzi naliacha kwa sababu kalikubali lakini haya ya *formula*, hebu atuwekee wazi kwamba katika hivyo vigezo alivyoviweka vya mwaka juzi hayatojirejea, lakini pili atuhakikishie kwamba kada maalum wakiwemo madaktari, walimu watazingatiwa katika marekebisho hayo. Mhe. Mwenyekiti, naomba maelezo.

**Mhe. Spika:** Mhe. Waziri maelezo zaidi na nilimsikia akitaja shilingi 17.5 bilioni na nilikusikia ukitaja shilingi 15 bilioni, hebu na hapo pia paweke sawa.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora:** Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na nimshukuru tena Mhe. Ismail kwa hoja zake. Nataka niseme kwamba kilichotokea mwaka 2011 ilikuwa ni makosa kuacha baadhi ya watumishi. Kwa sababu tulisema *program*

yetu ilizingatia kigezo cha kupandisha kima cha chini kutoka shilingi laki moja mpaka laki moja ishirini na tano. Lakini ika-*happen* kwamba kulikuwa na taasisi nyengine kima hicho kilikuwa tayari wameshakipita wao kama kima cha chini. Kwa hivyo, kompyuta ile *program* ikawa haikuwazingatia wale ikawa inawaweka kwenye kima kile kile ambacho kinatengenezwa kwenye *program*. Sasa hilo lilikuwa ni kosa la kiufundi kwa sababu sisi pale Utumishi wa Umma tulikuwa wapya hatukujua kwamba huko nyuma kulikuwa na taasisi ambazo hiki kima cha chini cha shilingi 125,000/- kwamba tayari walishazipita, lakini baadae baada ya kuwasiliana na taasisi husika tatizo hilo liliondoka, lilisawazika na kila mtumishi alipata haki yake kwa mujibu wa maamuzi.

Wajumbe wamezungumzia sana juu ya sheria inayozungumzia maamuzi ya nyuma, ilibidi turejee katika maamuzi ya nyuma kwa sababu vyombo vilivyotoa vilikuwa ni vyombo halali na vinatambuliwa na sheria yetu Nam. 2 ya mwaka 2011 sheria yetu ya utumishi.

Kimsingi hilo lilisawazika, tunachotaka kusema kwamba jambo hilo sasa hivi tumejiandaa vya kutosha kama nilivyosema, tunayo *program*, tunao wataalamu wa kutosha wenye uelewa wa mambo haya ya kimtandao, tumeajiri na sasa hivi wanafanya kazi hiyo. Taaban tutakapofika pahala sasa tunataka kulitekeleza kila kitu kitakuwa safi kabisa na mwanana na kitakuwa shwari.

Ninachotaka kusema kuhusu suala la kada adimu ni kweli nimetaja na moja kati ya mambo ambayo tutayazingatia ni hilo suala la kada adimu. Katika hotuba yangu pia nimesema hivi karibuni tumeidhinisha maposho mbali mbali kwa ajili ya kada hii adimu fani kama hospitali madaktari, *orderly* na walimu pia tumeidhinisha na wengi wengineo.

Katika marekebisho hayo na wataalamu wengine zile *rare professions* zote tutajitahidi sana tuzingatie katika kuona tunaweka maslahi yao mazuri ili kuwavutia na kuwa na moyo wa kuweza kufanya kazi katika nchi yao na badala ya kwenda kufanya kazi nchi za nje na kukimbia. Kwa hivyo, nataka nimhakikishie Mhe. Jussa na Baraza lako tukufu kwamba hilo tumelizingatia na tutalipa kipaumbele na watu wa maeneo hayo watafaidika katika marekebisho hayo.

Jengine la ile 17.5 bilioni au 15.5. ni kwamba fungu lote lile linajumuisha mishahara au marekebisho ya mishahara ambayo yatafanyika katika kipindi hiki cha mwaka 2013/2014. Kwa hivyo, kuna fungu litazingatia kada fulani na eneo fulani na kuna fungu litazingatia maeneo fulani. Lakini lote kwa jumla kasma ile ni kasma ya mishahara ambayo ipo kwenye fungu moja itaingia katika utaratibu mmoja wa kuweza kuwagawia wale wanaostahiki keki au kisheti kitakachokuwepo. Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

**Mhe. Spika:** Unajua nimebabaika kuona hesabu mbili tofauti, hii 17.5 au 15.5. nimebabaika kuhusu hesabu hizo 17.5 ameitaja yeye lakini wewe nilikuwa nakusikia wakati unatoa majumuisho kwamba kuna 15.5. Sasa *figure* ipi ni sahihi.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora:** Mhe. Mwenyekiti, unapata tabu katika 17.5 na 15.5. Mimi nadhani Mhe. Mwenyekiti, unikubalie tu kwamba matumizi haya yanahusu watumishi.

**Mhe. Spika:** *Figure* ipi iliyo sahihi? 17.5 au 15.5?

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora:** Mhe. Mwenyekiti, ni 17.5.

**Mhe. Ismail Jussa Ladhu:** Mhe. Mwenyekiti, nashukuru na niendelee kukupongeza mwenyekiti wetu kwamba katika masuala haya na wewe mwenyewe ni makini kuhakikisha kuwa tunafuata taratibu sahihi, kwa sababu hili niliseme sio tatizo langu lakini nalisema kutahadharisha tu, serikali iweze kujipanga vizuri. Unajua tatizo linalokuja kwamba tunapitisha suala la sera katika wizara hii lakini fungu la utekelezaji liko katika Wizara ya Fedha ndio ikafika wakati utaambiwa aah, kwa nini unazitaja zile kwa sababu ziko katika Wizara ya Fedha lakini utekelezaji wake unamhusu Mhe. Waziri wa Utumishi wa Umma, lakini kule kumetajwa 17.5.

Sasa baada ya maelekezo hayo kama alivyoeleza Mhe. Waziri na nikitegemea kwamba kama ulivyosema kuwa marekebisho yale mengine yatazingatiwa na matumizi haya ya hizi shilingi 17.5 pia

zitatizamwa vizuri hasa kwa sababu *CAG* atakwenda kufanya *proper auditing* ya *pay role*. Mhe. Mwenyekiti, nasema baada ya maelezo hayo mimi nashukuru tuendelee ahsante sana.

| | |
|---|---|
| Kifungu 0111 Idara ya Miundo ya Taasisi Utumishi na Maslahi ya Watumishi | 163,834,000 |
| Kifungu 0301 Ofisi Kuu Pemba | 434,448,000 |
| Kifungu 0401 | |

**Mhe. Mbarouk Wadi Mussa:**Mhe. Mwenyekiti nakushukuru, nilipokuwa nachangia nilieleza kutokuridhishwa kwangu na utendaji wa Mhe. Waziri wa kutokuandaa kanuni za ile sheria ya Utumishi wa Umma. Nilieleza azma yangu ya kuondosha shilingi katika mshahara wake. Pamoja na maelezo ambayo ameyatoa Mhe. Waziri lakini Mhe. Mwenyekiti, bado sijaridhika na zile sababu ambazo zimemfanya hadi hii leo kanuni ile haijawa tayari.

Mhe. Mwenyekiti, ile kanuni kama ndio muongozo wa ile sheria yenyewe au kina Maalim Abdalla wao wanasema inatia '*sherhe',* katika vitabu yaani inasherehesha ile sheria yenyewe. Sasa Mhe. Mwenyekiti, kuna miaka miwili tangu sheria ile imekuwa sheria, maana baada ya kusainiwa na Mhe. Rais tarehe moja Juni kama sikosei mwaka juzi 2011 hadi hii leo kanuni haijawa tayari. Sasa ukiangalia Mhe. Mwenyekiti, sheria hii utekelezaji wake unakuwa mgumu kweli, maana ina mambo humu yameelekezwa kwamba yatapatikana kwenye kanuni, yaani kanuni ndio itafafanua utekelezaji wa hii sheria yenyewe. Lakini miaka miwili Mhe. Mwenyekiti, kanuni haijawa tayari. Sasa nilimtaka Mhe. Waziri atueleze sababu za msingi kwa sababu ambazo alizizungumza mimi sikubaliani nazo kwamba wadau ni wengi awashirikishe, hii mimi sikukubaliana nayo. Lakini ametoa ahadi kwamba hivi karibuni itakuwa tayari, hata mwaka jana alisema hivyo hivyo kwamba hivi karibuni itakuwa tayari lakini mwaka umekatika.

Sasa azma yangu ya kulizuia fungu hili Mhe. Mwenyekiti, iko pale pale na ninaendelea kulizuwia fungu hili mpaka nitakapopata majibu ya kuridhisha.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikubaliane na fatwa ile ya Mhe. Mbarouk Wadi Mussa. Naona na yeye anamkaribia kidogo swahibu wangu Mwanasheria mkubwa. Sasa sijui yeye ile *concern* yake kwamba zile kanuni za utumishi chini ya sheria ile kusema kweli ni muhimu na zinasherehesha ile sheria yenyewe au zinaifanya iwe rahisi. Kusema kweli hicho anachosema ni cha msingi kabisa lakini naomba nilihakikishie Baraza hili kwamba kwanza Mhe. Waziri alitimiza wajibu wake, nao ni kufanya ule mchakato wa kuziandaa zile kanuni. Katika kuandaa kanuni hizi bahati mbaya mpaka ziwe kanuni hazimhusu yeye peke yake kuna na wengi.

Sisi tulipoletewa ushauri mmoja tuliotoa tulisema kwamba kwa sababu huku nyuma kulikuwa na kanuni mbali mbali pamoja na *GO,* na tumekuwa na matatizo katika usimamizi wa mambo mbali mbali chini ya sheria hii, si vizuri waziri akajifungia wakaandaa hizi kanuni halafu tena tukazitoa kwenye Gazeti Rasmi. Ni vizuri zingefuata kwa sababu hili ni jambo kubwa na tumekuwa na mazoea tofauti huko nyuma, ni vizuri likafuata utaratibu kama vile tunataka kupitisha sheria kutokana na umuhimu wa kanuni hizi. Maana yake ukitizama hata kwenye sera inaambiwa itoke *Public Service Hand Book*, yaani sio iwe tu kama kanuni lakini iwe kama ni muongozo.

Kwa hivyo, tukashauri sisi kwamba ni vizuri zifuate utaratibu, zipite kamati ya Makatibu Wakuu watoe maoni yao na ni vizuri hata zikaletwa Baraza la Mapinduzi kila mtu kwanza akazifahamu. Kama kuna mapungufu basi pia yakaongezwa tukasawazisha ili zitakapotoka ziwe ni kanuni ambazo zinaweza zikatusaidia badala ya kuharakisha tukapata kitu ambacho hakitotusaidia. Ni vizuri tukafanya utaratibu na tukawashauri hata zile tume za utumishi, ni vizuri na wao wakapewa fursa wakatoa maoni yao. Tume najua zilipewa na nyengine zilitoa maoni katika hili.

Ni kweli limechelewa lakini si kwa makosa ya waziri, ni kwa makosa au niseme ni kwa sababu za msingi kabisa za umuhimu wa kanuni zenyewe na ule mchakato umeshauriwa kwamba uende katika utaratibu ambao utakuja kutusaidia badala ya kuwa katika utaratibu ambao tutakuwa tu, tumetimiza wajibu lakini wajibu ule utakuwa haujatusaidia sana.

**Mhe. Mbarouk Wadi Mussa:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, pamoja na maelezo ambayo ameyatoa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, lakini mimi sijakubaliana na utendaji wa namna hii. Haiwezekani kutunga kanuni tuchukue miaka miwili. Huu ni udhaifu kwa sababu hii sheria imetungwa na Rais ametia saini kwamba sasa itumike, ina maana wanaizuia sheria hii kufanya kazi zake kwa muda wa miaka miwili sasa, maana yake kufanya kazi zake ni kupata ile tafsiri ya ile sheria yenyewe Mhe. Mwenyekiti. Sasa kama ile tafsiri haipatikani sheria hii itakuwa inatekelezwa nusu nusu. Kuna nusu ambayo vile vifungu vilivyokuwa wazi maana yake vitatekelezwa, vile ambavyo vinahitaji kanuni maana yake havitekelezeki.

Leo hii Mhe. Mwenyekiti, ukimwambia mfanyakazi kakawia kwa kutumia kanuni ipo, maana *GO* nayo imefutwa katika ile sheria, ilifuta vitu vyote. Sasa *GO* ilikuwa inaelekeza kule saa ngapi wataingia kazini, saa ngapi watatoka, labda likizo litaanza lini, mzazi atapata likizo la uzazi litakuwaje, hizo ni kanuni zinavyofafanua mle. Sasa ile sheria itakuwa ipo tu lakini haiwezi kufanya kazi zake. Mhe. Mwenyekiti, mimi naona bado kuna udhaifu wa utendaji. Sasa katika hili Mhe. Mwanasheria Mkuu anasema si suala la waziri, hapana.
Waziri ndiye aliyetajwa katika hii sheria kuwa ndiye dhamana, anaambiwa yeye akazitunge hizo kanuni, yeye ndio atakayemjua nani amkusanye na nani ampitie ili iweze kupatikana hiyo kanuni. Ina maana waziri hakuweza kufanya wajibu wake sawa sawa, maana yake angefanya wajibu wake sawa sawa sifikirii kama tungechukua miaka miwili.

Hiyo ndio hoja yangu Mhe. Mwenyekiti, hatuwezi kuchukua miaka miwili katika kutunga kanuni tu ikiwa kanuni hii moja inatuchukua miaka miwili, haya tungekuwa tuna tatu ingekuwaje. Baada ya miaka mitano au sita ndio kanuni zitakuja hapa. Sasa zile sheria tunazozitunga za kazi gani Mhe. Mwenyekiti, tumetunga sheria ziweze kutumika.

Utumikaji wa sheria unakuwa mgumu kama hakuna kanuni. Mimi Mhe. Mwenyekiti, nataka niendelee na hoja yangu niisimamie pale pale kwamba Mhe. Waziri ameshindwa kuwajibika amepewa majukumu lakini ameshindwa kuwajibika. Kwa hivyo, naendelea

kuzuia shilingi ya mshahara wake kwamba mpaka anihakikishie ni vipi atakuwa amewajibika.

Mwaka jana alitueleza hapa akasema sheria hizi lakini tulipoipitisha ile sheria, kwanza ile ya mwaka juzi atafanya mchakato haraka haraka ili kanuni ziwe tayari. Mwaka jana akasema haraka iwezekanavyo atazileta. Lakini mwaka huu bado anatwambia kuwa kikao kijacho ndio atazileta katika majumuisho yake alisema kikao kijacho ndio itakuja ile kanuni.

Mhe. Mwenyekiti, naona Waziri amekuwa na majibu ya kubabaisha, hakuwa na majibu sahihi. Sasa kwa hili nilikuwa labda nimuombe kwa heshima kabisa yupo hapa Mkuu wa shughuli za Serikali katika Baraza, atupe msimamo wa hii kanuni lini hasa itakuwa tayari sasa ili serikali yenyewe sasa iwajibike kwamba tunahakisha kipindi hichi kanuni hii itakuwa tayari ili sheria iweze kutekelezeka Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

**Mhe. Mwenyekiti:** Kabla ya kiongozi wa shughuli za Serikali ndani ya Baraza, tumsikilize tena Mhe. Mwanasheria Mkuu.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kusema kwamba hoja anayosema Mhe. Mbarouk Wadi Mussa ya umuhimu wa kanuni, mimi ninaiafiki na naamini kila mmoja atakubaliana naye kwamba hizi kanuni ni muhimu. Kama ambavyo kanuni katika sheria zote tunazozipitisha ni muhimu.

Lakini kwanza naomba nimtoe wasi wasi kwamba hii sheria haikufuta kanuni zote zilizofanywa kwenye sheria zilizokuja kwa mujibu wa sheria namba 7 ya mwaka 1984 isipokuwa labda kanuni zimefutwa wazi wazi kwenye ile sheria yenyewe. Lakini kanuni zilizotungwa katika sheria ilizopita kabla ya sheria ile kufutwa zinaendelea mpaka itakapotungwa kanuni nyengine mpya ndio utaratibu wa sheria. Kwa hivyo, sijui kama kuna mtu kamfuata Mhe. Mbarouk Wadi Mussa kwamba hakwenda likizo, kwa sababu tu kanuni haijawa tayari sina hakika, inawezekana yupo lakini inawezekana huyo aliyemfuata naye hafahamu au huyo aliyemnyima likizo kwa sababu hakuna kanuni itakuwa na yeye pia hafahamu.

Kwa mujibu wa sheria ni kwamba kanuni zilizokuwepo zinaendelea mpaka zitakapokutwa na kanuni nyengine ambazo zitatungwa chini ya sheria hii. Ni kweli zikiwepo kutakuwa na ufanisi mzuri zaidi lakini sasa hivi sio kama sheria haitekelezeki moja kwa moja, na kwa sababu masharti mengi ya sheria hii yanasomeka na sheria ya ajira ambayo ina masharti mengi kuhusiana na haki za wafanyakazi zinasomeka na sheria ya *labour relation* ambayo inaonesha haki za wafanayakazi katika mambo mengine. Lakini pia na kanuni zilizopo za utumishi ambazo hazijafutwa pindi kanuni hizi zitakapoanza kazi.

Mimi ninachomwambia Mhe. Waziri katimiza wajibu wake kwa sababu yeye anacholeta ile dhana ya utungaji wa zile kanuni. Tunapitisha sheria nyingi na Waheshimiwa Mawaziri wengi wanaandaa kanuni na ukenda leo ofisi kwangu utakuta rundo la kanuni ambazo wizara mbali mbali wameleta ziangaliwe na taasisi mbali mbali za Serikali, ofisi ile ambayo inatakiwa iziweke sawa mtu hasa aliyekuwa anasimamia usimamizi wa hizi kanuni, *actual* watu wawili au mmoja, yuko kwenye Tume ya Katiba na mwengine yupo.

Lakini kubwa tulisema kwamba kwa umuhimu wa hili nipate maoni zaidi ya wadau. Kwa hivyo, kama anasema waziri hakuwajibika siwezi kumtoa katika hilo, maana hawa ni majirani ni Mtumbatu wa juu na Mtumbatu wa kisiwani. Sasa hatujui huko wamefanya nini lakini ninavyofahamu kwamba huu mchakato unaendelea na naweze kumwambia kwamba hautofika mwezi wa kumi hizi kanuni zitakuwa tayari.

**Mhe. Mwenyekiti:** Kwa maneno mafupi ambayo Mhe. Waziri ameeleza Mhe. Mwanasheria Mkuu ameshaeleza mara mbili. Anasema kukawia kote huko ni kwa ajili ya kanuni hizo ziwe bora zaidi na ziondowe kwa kiasi kikubwa yale matatizo ya mambo ya kiutumishi ambayo yamekuwa yana matatizo kwa muda mrefu.
Madhumuni yake kukawia kote huko ni kuzifanya kanuni hizo ziwe bora. Katika hilo Mhe. Mbarouk Wadi Mussa unasemaje kabla hatujapiga kura?

**Mhe. Mbarouk Wadi Mussa:** Mhe. Mwenyekiti, kabla hatujapiga kura nataka na mimi nitoe ufafanuzi kidogo ambapo Mhe. Mwanasheria Mkuu amezungumzia. Tukiangalia katika ile sheria

yenyewe ya Utumishi wa Umma kwenye kifungu cha 103 kinasema masharti ya Kanuni kuwa, Waziri atatunga kanuni kueleza usimamizi wa huduma, nidhamu, mashauri ya kinidhamu na kutoa masharti ya watumishi wa utumishi wa umma. Ina maana haya hayatotekelezeka kama kanuni hazijatungwa.

Mhe. Mwenyekiti, hiyo ilikuwa ni 1 ukenda ya 2 pale inasema waziri anaweza katika kutekeleza uwezo chini ya kijifungu cha kwanza cha kifungu hichi kutunga kanuni

(a) Kueleza jambo lolote ambalo chini ya sheria hii linaweza kuwekewa kanuni achana na zile za zamani, yaani katika hii sheria mpya kuna mambo ambayo yamejitokeza ina maana yatungiwe kanuni kuyatolea ufafanuzi.

(b) Kueleza kanuni za maadili za utendaji kazi kwa watumishi wa umma ndio yanayomtaka afanye hayo, kuweka usimamizi wa utumishi wa umma na nidhamu na uimarishaji wa masharti na maelekezo ya utumishi wa umma kwa watumishi wa umma.

(c) Kuweka masharti ya viwango na fidia zitakazolipwa kwa athari za mwili au vitu, chini ya kifungu cha 79 cha sheria hii yako mengi hayo.

Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu kwamba miaka miwili kanuni hazijatungwa haya hayatekelezeki na hii ni sheria, haya ni matakwa ya sheria. Ina maana ilikuwa yeye waziri afanye bidii hawa wadau wote wako hapa hapa, *just* kuwaita akakaa nao akapata hayo mashari. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu iko hapa hapa ni kukaa nao akaweka utaratibu. Miaka miwili Mhe.Mwenyekiti, tunasubiri kanuni ili matakwa ya sheria yaweze kutekelezwa. Maana kuna hii sheria nimesema inatekelezeka lakini kuna sehemu lazima tupate ufafanuzi na ufafanuzi unafafanuliwa na hizo kanuni. Basi Mhe. Mwenyekiti, juu ya kwamba tunataka ije hiyo kanuni iwe barabara inafanana na sheria miaka miwili au zinatoka Uingereza. Kama tunatunga hapa hapa basi Mhe. Waziri inaonekana hakuweza kuwajibika ipasavyo maana Mhe. Rais baada ya kupelekewa ile sheria yeye alishaisaini tangu tarehe 1 Julai 2011.

Waziri anachukua miaka miwili wakati Mhe. Rais ameshaisaini kuwa sheria, bado Mhe. Mwenyekiti, tuseme kwamba yuko katika utelekezaji mzuri. Mimi hili kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, siwezi kukubaliana nalo, hapa panaonekana kuna udhaifu wa utendaji hilo ndilo ninalolisema mimi. Sasa nikamuomba tu Mhe. Waziri kwa heshima kabisa ili tusiendelee sana nimuombe sana Mkuu wa shughuli za Serikali atupe ahadi katika hili. Maana Mwanasheria Mkuu amesema kwamba haitofika mwezi wa kumi, haifiki mwisho wa mwaka huu kuwa itakuwa tayari. Lakini yeye ni Mwanasheria Mkuu pengine hiyo shughuli kwake imeshakaa siku chungu nzima pengine yeye ndiye aliyeikawilisha.

Sasa mimi namuomba Mkuu wa Shughuli za Serikali katika chombo hichi atupe ahadi basi mimi sina tatizo Mhe. Mwenyekiti, nadhali hiyo ahadi itakuwa imetolewa na kiongozi wa juu wa Serikali, maana yake sasa na yeye atamsimamia huyu waziri wake kwamba hatofanya hivi, yeye ndiye ameahidi hapa, hilo ndilo ninalolitaka na atupe muda ahsante.

**Mhe. Mwenyekiti:** Nataka nikumbushe jambo moja dogo sana kabla sijamuomba kiongozi wa shughuli za Serikali. Mwanasheria Mkuu katoa ahadi kwamba kabla ya Oktoba, sijui kama nimesikia ndivyo. Haya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais na Mkuu wa Shughuli za Serikali Barazani. (*Makofi*).

**Mhe. Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniruhusu kumsaidia Mhe. Mbarouk Wadi Mussa rafiki yangu wa siku nyingi. Lakini leo naona mimi amependa asikie sauti yangu humu ndani leo.

Mhe. Mwenyekiti, namshukuru Mhe. Mwanasheria wa Serikali kwa ufafanuzi alioutoa. Mimi niahidi kwamba nitafuatilia suala hili kama alivyosema Mhe. Mwanasheria nitahakikisha kwamba kanuni hizi zitakuwa tayari kabla ya mwisho wa mwaka.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Mbarouk Wadi Mussa ile sauti uliyokuwa unataka uisikie imeshatoka.

**Mhe. Mbarouk Wadi Mussa:**Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa kutoa ahadi katika Baraza hili. Si kwamba nilikuwa nataka kusikia sauti yake lakini nilikuwa nataka ahadi ya Serikali. Kwa sababu yeye Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ndio Mkuu wa Shughuli za Serikali katika chombo hichi lakini yeye ndiye anayewasimamia hawa mawaziri.

Sasa nilikuwa nataka kumuona kwamba anamsimamia yule Mhe. Waziri ipasavyo ili hii kanuni iweze kuletwa kutumika kwa sababu bila ya kuwepo ile kanuni Mhe. Mwenyekiti, bado tutakuwa tunapiga dane dane. Kwa hivyo, yeye anamsimamia waziri wake na nafikiria sasa waziri atawajibika. Lakini nataka kumwabia Mhe. Makamu wa Pili awaone baadhi ya mawaziri wake namna ambavyo utendaji wao haupo sawa sawa. Ahsante Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*).

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Mwenyekiti, na mimi nakushukuru kunipa nafasi hii nikataka ufafanuzi wa ziada, lakini kabla ya hapo nataka nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa ufafanuzi wake ambao aliutoa asubuhi.

Mimi nataka nimuhakikishie tu kwamba hii sauti ni sauti ya Ki-Bunge, sizungumzi kwa ukali na mimi ni mdau sana wa Mabunge. Mimi nilikuwa nafuatilia sana mijadala ya Bunge la Uingereza kama atamuona Waziri Mkuu wa Uingereza wa sasa hivi David Cameroon alipokuwa *back bencher, style* yake ya kuzungumza na mimi ndio ninayoiga hapa Barazani.(*Makofi*).
Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo nilikuwa nakuja katika hoja yangu. Kwanza Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri alipokuwa akitoa ufafanuzi kuna mambo mengine aliyazungumza ambayo sikuyazungumza katika mchango wangu, nilikuwa nataka nimuhakikishie alizungumza kwamba kuna mikakati.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa nataka nimuhakikishie Mhe. Waziri na Mawaziri wote mimi sina mkakati wowote kwa mtu yeyote. Mimi ninafanyakazi kwa mujibu wa Kanuni na Katiba inavyoturuhusu, kuiuliza maswali Serikali, kuishauri Serikali na ndio maana sichagui wizara kila hoja ambayo nahisi ya msingi ndio naizungumza.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nataka nimuhakikishie Mhe. Waziri mimi kwanza hanikuti katika baraza aina yoyote, mimi kwangu sina baraza. Kwa hivyo, mkakati sijui nitaupanga wapi. Hili tu rafiki yangu na mwalimu wangu nilikuwa nataka kumuweka sawa.

Sasa hoja yangu Mhe. Mwenyekiti, katika hoja aliyonambia atanijibu kwa maandishi. Suala la *Web-Site* ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, mimi kidogo Mhe. Waziri sikuridhika na jawabu yake. Kwa sababu hii ni hoja ndogo sana, hoja niliyosema kwamba *Web Site* ya Serikali sasa hivi imefungwa haionekani. *Web site* ile tuliizindua kwa vigelegele na Mhe. Rais wa Zanzibar nakumbuka aliizindua na pale Wazanzibari na watu wote wa ulimwengu wakitaka taarifa za Serikali wanafungua wanaangalia wakatutajia mpaka ile ufunguo wake, yaani *www. Zanzibar.go.tz.* **S**asa hivi iko *blank,why?*

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilitegemea kwa sababu hapa pamoja na kwamba tunamuuliza Mhe. Waziri lakini kuna *bench* la mawaziri mbele basi hata wao hawatembelei *Web Site* yetu ina maana hii *Web Site* tulimfungulia nani aangalie. Mimi nadhani hapa Mhe. Mwenyekiti, hapa pana uzembe kidogo. Ninafikiri Mhe. Waziri alikuwa anaona labda asiizungumze. Sasa hebu atueleze tu kwamba hii *Web Site* ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuna sababu gani iliyofungwa mpaka sasa hivi tumeshindwa kulipa au imeharibika, hebu anisaidie jawabu. Mimi naamini kwa sababu yeye anapojibu kuna jopo lake la wataalamu kule basi hili pia wameshindwa kuliangalia na wakaleta jawabu, ghafla moja Mhe. Mwenyekiti, labda akinisaidia maelezo nitaendelea huko mbele, kama alivyosema fungu 47 kama kawaida ahsante.

**Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora:** Mhe. Mwenyekikti, namshukuru sana Mhe. Hamza Hassan Juma, mwanafunzi wangu na hiyo *terminology* aliyonambia ya sauti ya Kibunge naikubali.

Lakini nataka nimwambie kilichonisikitisha mimi kutokumwambia *Web Site* ya Serikali ambayo iko chini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kama inafanyakazi au haifanyi kazi, ni ile ile kulinda heshima ya

Baraza la Wawakilishi kwamba usiseme kitu ambacho huna hakika nacho.

Ndio maana nikamwambia kwamba kwa sababu hili jana unajua tumetoka usiku na bahati nzuri usiku mwigi nimefanyakazi ya kufanya majumuisho sikuwahi kuwasiliana na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, sikupata uhakika kama inafanyakazi au haifanyikazi. Lakini *Web Site* ipo chini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais nayo ni *www.Zanzibar.go.tz* na *Web Site* hii kama inafanyakazi au haifanyikazi bahati nzuri Waziri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais yupo. Lakini *Web Site* ya Wizara ya Utumishi wa Umma inafanyakazi hiyo nina uhakika nayo na ndio maana hata kwenye kitabu changu nimeiweka kwa sababu shughuli zetu zote sasa hivi tunatumia *Web Site* hiyo. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, kilichonisikitisha mimi kufanya hivi kusema kitu ambacho sina uhakika nacho na katika Baraza hili hutakiwi useme kitu ambacho huna hakika nacho. Lakini baadae wataalamu wangu wamenithibitishia kwamba *Web Site* nambari yake ni hiyo, lakini inafanyakazi au haifanyi kazi, hilo siwezi kulithibitisha kwa sababu wenyewe wizara hapa wapo.

Nirejee kauli yangu ya asubuhi sina nia ya kuwarushia paka wa uso wenzangu hapana. Lakini mimi sina hakika kama inafanyakazi au haifanyikazi. *Web Site* ya Wizara Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora inafanyakazi.

Mhe. Mwenyekikti naomba Mhe. Hamza Hassan Juma anielewe hivyo kwamba jina la *Web Site* ni hii. Ile *Web Site* ya Serikali inafanyakazi au haifanyikazi nitamuomba mwenzangu hapa asaidie hilo lakini *Web Site* ya Wizara ya Utumishi wa Umma ijapokuwa hakuitaka hiyo nina uhakika nayo inafanyakazi.

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:**Mhe. Mwenyekiti, *Web Site* ya Serikali inafanyakazi na sasa hivi tumeweza kumtuma mtendaji wetu kwenda kufungua akaona kwamba iko kazini hata hiyo rasimu ya Katiba tutaipata kwenye *Web Site* hiyo.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Mwenyekiti, nilipokwenda China juzi nilikuja na chombo hiki hapa. Chombo hiki unaweza kuona mitandao yote, sio simu huu ni mtandao naweza kuiangalia dunia

nzima, rasimu ya Katiba, Prof. Shivji hapa nikifungua tu naona ule mdahalo alioutoa juzi pale Dar -es Salamu, ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar iko *black*.
Sasa nilikuwa naomba tu Mhe. Mwenyekiti, kwamba ile ndio sura ya nchi tena ule ni utawala bora kabisa, nilikuwa naomba suala hili waliokabidhiwa dhamana hii basi wajitahidi kila wakati wawe wanaiangalia na iweko *live*. Mhe. Mwenyekiti, naomba tuendelee.

**Mhe. Ismail Jussa Ladhu:** Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya pili katika utaratibu wa vifungu.
Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nilizungumzia suala la e-*Government* na nikahoji kwamba inasikitisha sana kwamba mradi huu umekuwa ukipigwa dana dana.

Mhe. Mwenyekiti, msingi wa hoja yangu ulikuwa unatokana na maelezo ambayo yako ukurasa wa 11 kwa hotuba ya Mhe. Waziri pale aliposema, "Kutokana na kuchelewa kuanza kwa matumizi ya huduma za mkonga wa mawasiliano ya *ICT,* hakuna makusanyo yaliyopatikana na kwa sasa ukusanyaji wa mapato hayo umehamishiwa Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo Zanzibar". Mwisho wa kunukuu.

Mhe. Mwenyekiti, nilipochangia nilihoji kwamba mradi huu ambao tuliombwa na tukaidhinisha humu ndani jumla ya fedha za dola za Kimarekani milioni 19 ambapo ungeweka mkonga wa taifa na ukaambatana na huo mfumo wa *e-Government*. Sasa mwaka juzi ulipoletwa Mhe. Mwenyekiti, nilihoji suala moja na nafikiri utakumbuka kwamba mradi ule ulikuwa unaonekana kama vile unagombaniwa.

Ulikuja ukatajwa katika hotuba za Wizara nne humu ndani. Nikauliza hasa mwenyewe nani? Tukavurugana mwisho ikawa Wizara ya Mawasiliano, mwisho nikamtaka Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha atuhakikishie na yeye akasema kwamba mradi huu mwenyewe ni Wizara ya Mawasiliano.

Katika yale mambo ambayo Mhe. Mwenyekiti, analalakimika kwamba kupewa halafu hatekelezi ni kwamba haukurejeshwa Wizara ya

Mawasiliano kinyume na ahadi zetu za serikali ndani ya Baraza hili. Tukanyamaza tukasema kama tunakwenda mbele sawa.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, mwaka jana tuliambiwa mradi huu umekamilika na hivyo tukaomba fedha sasa sio tena mradi wa maendeleo ya kusaidia utekelezaji wa shughuli ile na tukaambiwa matokeo yake gharama za uendeshaji na matumizi ya mambo ya *internet* kuwa Serikali na taasisi za watu binafsi na kwa raia wa kawaida zitashuka.

Lakini mwaka huu tunaambiwa hakuna mapato yaliopatikana kwa sababu haya mambo yameelezwa ndani ya hotuba. Mimi nilitoa hoja katika mchango wangu bahati mbaya ulikuwa hupo katika kiti, lakini kiti kipo. Nilitoa hoja kwamba iundwe kamati teule kwenda kuchunguza mradi ule na Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu hiyo nashukuru iliungwa mkono na Mhe. Salmin Awadh, Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Hija Hassan Hija, Mhe. Mbaouk Wadi Mussa na Mhe. Jaku Hashim Ayoub na wengine.

Nimesikitika kidogo kwa upotoshaji tunaambiwa leo katika redio ya *Zenj Fm* saa 11 imetangazwa kwamba Serikali imekataa uundwaji wa kamati teule. Mimi nikastaajabu nikasema Serikali haina mamlaka ya kukataa, wenye uwezo wa kuunda kamati ni Baraza hili.

Sasa nimesimama hapa Mhe. Mwenyekiti, kusimamia hoja yangu hiyo waziri maelezo yake na ndio maana nachukua muda, waziri katika maelezo kajibu sahihi na katika hili nitakuwa shahidi hapa hata mbele ya Mwenyezi Mungu kwamba upande wake yeye mimi nathibitisha kwamba alitoa ahadi kama alivyosema ndani ya kamati wakati huo nilikuwa ni mjumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwamba yeye hana tatizo tupewa *break down* na hii ilitokana tulipotembelea kama Kamati ya Katiba na Sheria wakati huo mie niko Mjumbe, tuliomba mchanganuo wa gharama zake akasema tupewe hatukupewa tukaambiwa tuandike Wizara ya Fedha Mhe. Mwenyekiti, ninayo barua hii hapa ambayo Mwenyekiti wangu wakati ule Mhe. Naibu Spika wako yuko hapa Mhe. Ali Abdalla Ali alitia saini barua tuliyopeleka tarehe 16/5/2012 zaidi ya mwaka mmoja uliopita kuomba mchanganuo, mpaka leo barua hii haikujibiwa na Serikali.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, ni wazi kwamba hapa pana matatizo, hapa fedha zimeliwa. Mimi nina kila sababu ya kuamini hivyo kwa sababu kama nilivyosema ushauri wa kitaalamu niliopewa ni kwamba hata nusu ya gharama zilizotajwa milioni 19 dola zisingefikia. Lakini zaidi tuna taarifa kwamba tulipotembelea katika kamati yangu mpya uliyoniweka Mhe. Mwenyekiti, ya Mawasiliano na Ujenzi kwamba kazi yenyewe imefanyika chini ya kiwango, zile mita tatu kuzikwa kwenda chini, kwenda ardhini kazikufikiwa hata pale palipozikwa pamezikwa kama alivyosema Mhe Salmin Awadh Salmin katika mabega ya barabara. Kwa hivyo kwa kifupi kuna madudu makubwa katika mradi ule.

Sasa naomba kwa mujibu wa kanuni zetu ya 120 (2) kwamba kamati teule itapendekezwa kwa njia ya hoja itakayotolewa na mjumbe na kuamuliwa na Baraza, taarifa ya hoja hiyo haijajadiliwa. Mimi naomba sana Mhe. Mwenyekiti, sasa kamati hii utoe tamko rasmi kwamba tuunde kamati teule ili kwenda kuuchunguza mradi huu wote tujue nini kimefanyika na nini hakijafanyika na baadae tulete ripoti katika Baraza lako. Mhe. Mwenyekiti, naomba sana.

**Mhe. Mwenyekiti:** Kabla ya kuamua hoja kuna maelezo Mhe. Waziri.

**Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora:** Mhe. Mwenyekiti, ni kweli alitoa hoja hii na aliungwa mkono na baadhi ya Waheshimiwa wengi katika kutaka iundwe kamati teule na mimi majibu yangu yalikuwa *very clear,* kwamba tatizo ni kukubali mimi kuundwa kamati teule, hili fungu la uratibu wa mradi wa *e-Government* halikusimamiwa na wizara yangu. Haidhuru kama nilivyosema mawaziri sisi tunawajibika kwa pamoja hapa ndani ya Baraza la Wawakilishi kwa mujibu wa Katiba.

Lakini kuingia katika jambo ambalo hukulisimamia linaweza kuleta matatizo, nimuombe sana kwa heshima kubwa sana Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwamba hili jambo angesubiri kwenye sekta husika akaja akali-*raise,* namuomba sana pengine ama wanaweza wakampa maelezo na pengine akaondokana na hoja yake ama pengine wao sasa wameona namna ya kuweza kulitolea kauli juu ya jambo hilo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kama Ofisi ya Utumishi wa Umma kazi yangu ni kuendesha ile *system* ya *e-Government* na suala la utaratibu wa mradi huu na matumizi yake yako Wizara ya Fedha. Sasa mimi nimuombe sana Mhe. Ismail Jussa Ladhu akubaliane na mimi pengine hoja aihamishe asubiri siku ya fungu la Wizara ya Fedha ili hili jambo lije kupata maelezo ya kina kabisa katika utekelezaji wake. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Ismail Jussa Ladhu mradi hauko chini ya wizara yake uko chini ya Wizara ya Fedha.

**Mhe. Ismail Jussa Ladhu:** Mhe. Mwenyekiti kwa utaratibu hata nisingelazimika kusimama tena. Lakini kwa sababu katoa maelezo Mhe. Waziri nadhani ni vizuri hoja zake zikasikilikana na halafu utuongoze tufanye maamuzi kama kanuni zetu zinavyotaka.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ushahihi kabisa Mhe. Waziri kasema kwamba Serikali inawajibika kwa pamoja katika chombo hiki. Na ibara 43.5 naomba nisome Mhe. Mwenyekiti, Katiba ya Zanzibar inasema kwamba:-

Ibara 43.5 "Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya mamlaka ya Rais ndio itakuwa na uwezo wa kufanya maamuzi juu ya Sera za Serikali kwa ujumla na mawaziri chini ya uongozi wa Makamu wa Pili wa Rais, watawajibika kwa pamoja katika Baraza la Wawakilishi kuhusu utekelezaji wa shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kama maelezo hayo yangekuwepo basi tungepatiwa hapa kwa sababu serikali iko hapa yote na Makamu wa Pili wa Rais yupo, lakini zaidi hapa hoja ni ya kuundwa Kamati Teule ambayo kwa kawaida haitaki mjadala wala haina msingi kwamba hoja ya kuundwa Kamati Teule umeiibua katika eneo gani. Nimeiibua hapa kwa sababu kama nilivyosema baada ya kukamilika mradi tumeambiwa umeanza kupelekwa kwake na katika kitabu cha hotuba yake kaja katuripotia. Lakini zaidi Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema katika Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ambayo ulikuwa umeniteuwa katika kipindi kilichopita tukiwa tunaisimamia wizara hii, wizara yake ndio iliyotupeleka kwenda kukagua mradi wa *e-government* hapo Mazizini.

Kwa hivyo, ninachosema sio suala la kwamba iko wapi, yeye ndiye aliyeripoti na hapa ndio pahala pale, kwa sababu mradi huu haujaripotiwa pahala pengine popote Mhe. Mwenyekiti. Hata tutakapofika katika fungu la maendeleo bado kuna kifungu cha *e-government*, hata katika mfumo wowote ambacho kinahusu wizara yake. Sasa naona mheshimiwa aje katika hili asijizonge, asijaribu kuona labda tunamuhukumu yeye, tunaihukumu serikali na tumetaka iundwe Kamati Teule, hiyo nilitaka ku-*clear* kabisa, nimesema nimeweka katika kumbukumbu ya *Hansard* kwamba yeye tangu wakati nilikuwa mjumbe alishajieleza kwa muonekano wake hana shaka na hili.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kukusaidia tu na kulisaidia Baraza lako kwa sababu sio vizuri kuliongoza Baraza kufanya maamuzi makubwa kama haya, kwamba ikadhaniwa labda kuna hoja tu ya juu juu. Mhe. Mwenyekiti, nasema kuna matatizo katika suala la mradi wa *e-government*. Mbali ya gharama anazozizungumza za mradi wenyewe, kama alivyosema kuna milioni 19 dola hizo Mhe. Mwenyekiti, katika fedha za Tanzania ni takriban kama si zaidi ya shilingi bilioni 30 hizi ni fedha nyingi sana, zingeweza kufanya mambo mengi sana na zingeweza kutatua matatizo mengi sana ya wananchi wetu.

Pia Mhe. Mwenyekiti, tunaambiwa katika suala hilo mpaka leo katika ofisi ya *e-government* hakuna *tender board*, ununuzi wa mitambo hauna maelezo yanayoeleweka, kuna ujenzi wa jengo lenyewe lile namna lilivyojengwa, kuna mambo mengi yana mapengo katika mahesabu, kuna suala la kumbukumbu za matumizi yake hayako sawa. Lakini Mhe. Mwenyekiti, tunazo taarifa kwamba serikali imefika kuingia hasara ya kulipa leseni kwa kampuni ya *Microsoft* kuhudumia mradi wa *e-government* ambao baadae hautumiki mpaka leo. Sasa hizi ni fedha za maskini Mhe. Mwenyekiti.

Kwa hivyo, mimi nilikuwa naomba Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima na nimalizie nukta yangu moja tu. Mhe. Mwenyekiti, katika kitabu cha bajeti kuu, katika ukurasa wa 16 palikuwa na deni la taifa ambalo limeongezeka kutoka shilingi bilioni 209 hadi bilioni 252. Mhe. Mwenyekiti, hizi ni fedha ambazo zinaongezeka kutokana na mikopo kama hii inayochukuliwa ambayo baadae inafaidisha matumbo

ya watu badala ya kuwafaidisha wananchi wa Zanzibar. Sasa Mhe. Mwenyekiti, sisi kama wasimamizi nadhani uturuhusu.

Mhe. Mwenyekiti, nikumbushe jambo moja, naomba nitumie fursa hii. Nimegundua katika *Public Finance Act*, sheria ya matumizi ya umma. Katika kifungu cha 23 kuna jambo ambalo serikali haitufanyii Baraza hili katika miradi ya maendeleo. Kwa heshima yako hili tunafanya maamuzi magumu, naomba nikisome kinasema hivi;

Kifungu cha 23 *Public Finance Act;*

*"Where for the purposes of any development project which has been approved by the House of Representatives by resolution or otherwise a contract for the supply of goods or services is entered into on behalf of the Revolutionary Government of Zanzibar which provides that any payment (other than a payment charged on the Consolidated Fund by virtue of the provision of this or any other Act) is to be made on or after the first day of the next accounting period, the Minister shall as soon as possible after the making of such contract give notice thereof to the House of Representatives and every such notice shall specify:-*

*a) The names of contracting parties;*

*b) The nature of the goods or services to be supplied;*

*c) The total amount payable by the Revolutionary Government of Zanzibar in respect of such goods or services and the date or dates on which payment is to be made, the development project to which such contract is referable".*

Mhe. Mwenyekiti, kifungu hiki nime-*notes* kwamba kimekuwa hakitekelezwi, kinahusu miradi yote ya maendeleo, lakini hatujawahi kupewa taarifa hizi. Sasa mengine tutaamua siku za mbele. Kwa mradi huu mimi naomba tuanze kutengeneza kifungu hiki na taarifa hizi zilizotajwa tutaweza kuzipata sio tena kutegemea serikali kuja kutujibu, serikali tumeipa nafasi. Kama nilivyosema tumeliibua mwaka juzi, tumeliibua mwaka jana na tumeandika barua hii hapa Mhe. Mwenyekiti, yote inaonesha dharau ya serikali kwamba watu wa Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo wanadhani wana haki ya kutafuna fedha za umma kadri wanavyotaka hakuna mtu wa kuwahoji.

Mhe. Mwenyekiti, naomba hoja yangu ambayo imeungwa mkono na wajumbe wengi wa Baraza hili tuiamue tuunde Kamati Teule tukachunguze suala hili. Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja, ahsante *(Makofi).*

**Mhe. Mwenyekiti:** Mmemaliza. Tuwe na utaratibu kabla ya kuamua hoja hii nilitaka tupate ufafanuzi, nina hakika ndio Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria anataka kutoa lakini ufafanuzi dhamana hii iko katika wizara gani. Sijapinga suala la kwamba Kamati Teule iwepo au isiwepo, lakini je tunaunda Kamati Teule chini ya wizara ambayo sio yenye dhamana hii. Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, karibu.

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru ndugu yangu Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwa maelezo yake yote. Mhe. Mwenyekiti, mjadala huu uko chini ya Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo na mradi huu ulianza zamani kidogo, kabla awamu ya saba kuingia madarakani. Lakini hata hivyo serikali ni endelevu na kwa msingi huo Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ingeweza kutoa ufafanuzi wa kina kuhusu mradi huu na kwa kuwa Wizara ya Fedha itakuja hapa kuwasilisha bajeti yake, naamini kama alivyosema Mhe. Waziri hapa itakuwa na ufafanuzi wa kutosha. Maana mradi huu una mambo mengi, una suala zima la kulaza mkonga wenyewe, una suala zima la kusambaza miundombinu na kadhalika.

Mhe. Mwenyekiti, wizara hii kazi yake baada ya kukamilika kote ndio itakabidhiwa kwa sababu ya kusimamia maendeleo. Kwa hivyo, kwa vyovyote vile ikiwa kuna upotevu wowote wa fedha, basi wahusika wa mradi wanakuwa ni Wizara ya Fedha. Ni vyema Mhe. Mwakilishi akavuta subra na kungojea Wizara ya Fedha itakapowasilisha bajeti yake, na naamini watalieleza jambo hili kwa kina. Kwa vyovyote vile kama alivyosema Mhe. Waziri kulipeleka jambo hili kuundiwa kwenye Kamati Teule kwenye wizara yake litakuwa lina uzito fulani. Sote hapa Mhe. Mwenyekiti, tunapinga kwa njia yoyote ile ubadhirifu au matumizi mabaya ya fedha za serikali. Kwa hivyo, siku zote tutakuwa tuko tayari kusikia kwa namna yoyote ile tutakayohakikisha kwamba matumizi mabaya ya serikali hayana nafasi katika serikali hii. Lakini na utaratibu Mhe. Mwenyekiti, ni lazima tufuate ili mambo

haya yaende katika njia nzuri, ufumbuzi mzuri upatikane na yote haya yataelezwa kwa kina wakati Wizara ya Fedha itakapowasilisha bajeti yake.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Mwakilishi azidi kuvuta subra, angojee wakati ukifika maelezo atayapata, naamini pengine ataridhika kabla hata ya kufikia uamuzi huu ambao leo ameutaja. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria ulitaka kusema kitu, hebu tupe maelezo, kabla sijatoa maamuzi.

**Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria:** Mhe. Mwenyekiti, hapa kuna njia mbili. Kwanza ni kuunda Kamati Teule na pili ni suala la kwamba aidha Kamati Teule iundwe wakati wa wizara hii ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora au katika Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Kwa uzoefu mdogo niliokuwa nao, utaona kanuni ya Baraza la Wawakilishi, nafikiri kifungu cha 120. Kinasema kwamba Baraza linaweza likaunda Kamati Teule kwa *issue* yoyote itakayotokea.

Hii Mhe. Mwenyekiti, haina maana kwamba ile Kamati Teule haiwezi kuundwa kama kuna wizara inayozungumza, lakini ikatokea *issue* katika mazungumzo yale, unapounda Kamati Teule haina maana kwamba unachunguza ile wizara. Inapoundwa Kamati Teule unaunda kwa kuchunguza *issue* ambayo imekuwa *arise*. Sasa hapa *issue* iliyokuwa *arise* ni suala la mkonge na unapounda Kamati Teule hu-*reflect* kwamba lazima uende katika Wizara ya Utawala Bora kwa sababu ndio ilipokuwa *recite.* Kamati Teule ina-*general terms* inaweza ikaenda pahala popote katika kutafuta taarifa kuhusiana na hilo.

Sasa kwa kifungu cha 120 cha kanuni tunaweza tukaunda Kamati Teule wakati wowote hata hivi sasa. Halafu Kamati Teule ile inaweza ikenda katika wizara nyengine zozote zinazohusika, kwa sababu wale wanakwenda kutafuta taarifa hiyo ambayo italetwa pengine hata haihusiani na Wizara ya Utawala Bora. Kwa maana hiyo Mhe. Mwenyekiti, inategemea Baraza litaamua vipi, kama litaamua kuunda Kamati Teule tunaweza tukaamua hivyo na tukaendelea halafu *issue* hiyo ya Kamati Teule wakatizama wao katika sehemu zote

zinazohusika, kama ni Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, kama ni Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano au kama ni Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Sasa huo ndio utaratibu wa Kamati Teule inavyofanywa chini ya kifungu cha 120, kwa sababu hapa haikusema kwamba lazima iwe katika wizara ile.

Kwa hivyo, mimi Mhe. Mwenyekiti, naomba tuamue suala hili ili tuweze kumpitishia vifungu vyake Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora, nakushukuru Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe, sipingani na hoja iliyotolewa, ningeweza kuiamua kama maelezo aliyotoa Waziri Mhe. Abubakar Khamis Bakary. Lakini kimsingi unaamua hoja baada ya kwamba hakuna maelezo sahihi, kama kuna maelezo ambayo wajumbe mnaweza ikawa mmeridhika basi haja ya kuunda Kamati Teule itakuwa haipo.

Sasa maelezo yangeweza kutolewa na waziri yeyote lakini waziri hasa ambaye mradi huu hayupo kwa shughuli za kikazi. Mimi nimuombe na hii iwe ndio *ruling* ninayoitoa. Nimuombe Mhe. Ismail Jussa Ladhu tu-*suspend* hoja hii ili tusubiri wizara inayohusika. Kama kutatoka maelezo yaliyo mazuri na wajumbe wakaridhika nayo pamoja na yeye mtoa hoja, basi wakati huo tunaweza tukaamua kwamba Kamati Teule iundwe au laa. Lakini napata tabu kidogo kuiamua hoja hii wakati maelezo sahihi ya kina hayakuweza kutolewa kwa sababu ya waziri anayehusika hayupo.

Niwaombe Waheshimiwa Wajumbe tukubali kwamba hoja hii tui-*suspend* mpaka wizara inayohusika iingie, ili waziri anayehusika na dhamana ya jambo hili apate nafasi ya kutoa maelezo, tuone kama maelezo haya yanaridhisha au laa na hoja hii inaweza ika-*take on board*.

**Mhe. Ismail Jussa Ladhu:** Mhe. Mwenyekiti, kimsingi mimi sina pingamizi kwa sababu najua maelekezo yako unayotupa na umesema ni *ruling* na kama ni *ruling* hatupaswi kuihoji, kwa sababu wewe ndio mwenyekiti hapa. Kwa hivyo, mimi kwa kuheshimu kawaida siku zote taratibu za Baraza hili na ni mlinzi wake mmoja mkubwa

nitaliheshimu hili, lakini nachukulia kwamba *ruling* yako maana yake ni kwamba itakapofika wizara inayohusika ambayo kwa sasa umeamua kuwa ni Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, kwa maelezo ya serikali yenyewe kwamba wanasimamia madeni wao, kuwa wakifika hapa hawatokuja kuruka, maana hatuna haja tena ya kuja kuibua hoja. Ni kwamba hoja umei-*suspend* tu hujaizika.

Kwa hivyo, ikifika hapo kama yapo maelezo na sijui, kwa sababu kama nilivyosema kuna barua hii na sijui kama kwenye hotuba ya bajeti utakuja kutupa maelezo ya mradi mpaka turidhike, kwa sababu kuna mambo mengi ambayo yanahitaji maelezo. Lakini kwamba tusubiri kuiamua mpaka ikifika wizara hiyo, mimi sina tatizo lakini nimesimama kuuliza kuhusu utaratibu wa sehemu moja tu Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba mradi unaitwa *e-government* lakini umejumuisha na mkonga wa taifa vinakwenda pamoja. Nikasema mwaka juzi umetajwa katika wizara sijui kama nne au tano, maana yake ilikuwa Wizara ya Fedha inayoshikilia fedha, Wizara ya Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora imesema kwamba ndio inayosimamia utekelezaji wa *e-government*, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano tukaambiwa ndio inayosimamia mkonga wa taifa, ilipokuja Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi tukaambiwa watu wa vitambulisho ndio wanaosimamia uendelezaji wa mradi wenyewe.

Kwa hivyo, imekuwa haina mwenyewe ndio maana nikasema inahusu serikali kwa ujumla wake, tulihoji hapa kwa sababu katika kitabu cha hotuba ya waziri kataja kwamba sasa ndio kakabidhiwa yeye. Kama nilivyosema nilipokuwa mjumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria tulikwenda tukakagua na waliokwenda kutukaguza ni watu wa wizara yake. Kwa hivyo, mimi sina tatizo Mhe. Mwenyekiti, na *ruling* yako. Nilikuwa naomba muongozo wako tu kwamba tutakapofika kwenye fedha za maendeleo za wizara hii hii, kuna kiji-*component* cha *e-government*, basi naomba tuiamuwe sasa hivi, tukifika huko uje uniruhusu nije niulize kwamba je, fungu hili tunaliruhusu wakati huo mfumo wa kuezesha hiyo *e-government* ku-*takeoff* hatujaupatia maelezo, nitakuja kuomba maelezo tukifika hapa. Ukisha kulielewa hili Mhe. Mwenyekiti, nasema tuendelee, ahsante.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ninachokiogopa kuweka *precedent* kuibuka hoja wakati jambo ambalo limeibuliwa halihusiani na wizara ile, hii inawezekana ikawa *precedent* ambayo inaweza ikatupeleka pahala ambapo hatutegemei.

Kwa hivyo, kama kuna maelezo zaidi baadae wakati wa kifungu cha maendeleo tutakusikiliza kama kawaida, lakini *ruling* ninayoitoa tusubiri Wizara ya Fedha. Haya tuendelee.

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 0401 | Idara ya Mipango, Sera na Utafiti | 162,956,000 |
| Kifungu 0402 | Chuo cha Utawala wa Umma | 600,000,000 |
| Kifungu 0501 | Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu | 525,565,000 |
| Kifungu 0601 | Idara ya Mafunzo na Maendeleo ya Watumishi | 111,698,000 |
| Kifungu 0701 | Idara ya Mipango ya Rasilimali Watu | 177,696,000 |

Kifungu 0901

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:**Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kuniona hivi sasa. Vile vile nimshukuru Mhe. Waziri au mwakilishi mzoefu wa Baraza lako hili Mhe. Haji Omar Kheir kwa lugha nzuri aliyokuwa kaitumia hii leo na tunaambiwa vile vile maneno mazuri ni sadaka. Tunashuhudia hata wengine leo akiwaita mwanafunzi, wengine walimu na wengine kaka tunamshukuru sana na ufafanuzi aliotupa.

Mhe. Mwenyekiti, lile suala la daktari lilichukua karibu nusu mwaka hivi sasa na hii leo akanijibu kuwa watakalia kitako, lakini wananchi wa Jimbo la Muyuni wanasema wanamuonea huruma kwa muda mrefu kishasema karibu miezi sita au nusu mwaka. Kwa hivyo, ningemuomba tu leo akatoa uamuzi ili yule daktari akaanza kazi kesho rasmi, hakuna tatizo lolote, daktari kishafanyakazi karibu miaka 30. Nakuomba mheshimiwa kwa heshima na taadhima utoe kauli hivi sasa ili yule daktari kesho aanze kuripoti kazi. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora:** Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru Mhe. Jaku Hashim Ayoub, lakini kama alikuwa amenifuatilia vizuri, mimi sina tatizo hata kidogo, ningependa

kabisa daktari wetu aanze kazi kesho. Lakini kuna taratibu ambazo zinatufanya tusiweze kwa sababu nimezitoa *scenario* mbili ambazo zinawezekana.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwa mujibu wa sheria ya marekebisho ya sheria ya utumishi wa umma, nimepewa mamlaka ya kutangaza kada hadidu, *rare proffesional* na masharti yake ni kwamba nikishaona katika taasisi yoyote ya serikali inahitaji watu wa aina hiyo, natakiwa nitangaze kwenye gazeti rasmi au nitengeneze *legal notes* kwa ajili ya kutangaza. *Legal notes* iliopo sasa hivi inatambua kuwa kada ya afya ipo kwenye *rare professional*, kuanzia ngazi ya diploma, mtumishi wetu hana sifa hizo. Sasa nilimuambia *scenario* mbili.

Ya kwanza ama bodi ya madaktari ikae ihalalishe nafasi aliyonayo iwe inalingana na diploma, kama tulivyofanya kwa wanafunzi waliotoka Chuo cha Karume Ufundi ama mimi mwenyewe niende sasa baada ya kushauriana na Wizara ya Afya na wataalamu nirekebishe ile *legal note* badala ya kuweka kuanzia ngazi ya diploma, sasa niweke na *qualification* nyengine ambayo inalingana na hiyo diploma.

Sasa kazi hiyo nataka nimuhakikishie Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwamba haitachukua muda mrefu, kwa sababu jambo lenyewe ninaruhusiwa mimi kisheria, kiasi cha kutengeneza ile *legal note* na tukafanya hayo baada ya kushauriana na wizara yake. Kama lingekuwa ni suala tu la kufanya bila ya kufuata tarataibu hizo za sheria, namuhakikishia Mhe. Jaku Hashim na watu wa Muyuni kesho ningefanya hiyo kazi, lakini kwa sababu tutahitaji hivyo, wakiniambia Wizara ya Afya kwamba bodi inaweza kukaa na ikafanya maamuzi haraka, nikiona kuwa hakuna *posibility* hiyo basi mimi mwenyewe nitakapofika ofisini kuanzia kesho au keshokutwa nitalifanyia kazi hili jambo na Mhe. Jaku Hashi atafurahi.

Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Jaku Hashim asiniambie kitu lakini nimuahidi angalau wiki ijayo hilo jambo linaweza likakamilika na wananchi wa Muyuni wataondokana na kadhia hii. Nataka nimpongeze Mhe. Jaku Hashim kwa sababu amekuwa anawatetea sana wananchi, kama nilivyosema agizo ni la Rais, lakini sasa Rais hata kama anatuagiza tuangalie tunaloagizwa hatuwezi kuvunja sheria katika utekelezaji wake. Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Jaku

Hashim akubaliane na mawazo yangu kwamba nilikuwa *busy* na bajeti hii na *Inshaallah* bajeti hii itamaliza leo na nitakaporudi ofisini kesho na keshokutwa nitalishughulikia hili jambo na wako wengi wa namna hii. Ndio maana nikasema nikae na Wizara ya Afya, lakini maalum kwa ombi hili la Mhe. Jaku Hashim basi hili jambo nitalifanya haraka iwezekanavyo.

**Mhe. Jaku Hashi Ayoub:** Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, mimi ningemuomba sana tena sana, mimi ni *mas-ullah* kwa wale wananchi wa Jimbo la Muyuni na itabidi kuwajibika mbele ya safari ninakokwenda *'kullukum raii wakullukum mas-uul alaa raiyyatihi'*, kila mmoja ataulizwa kwa alichokichunga.

Mimi namuomba, kuanzia leo yule daktari nitamuajiri mpaka atakapokuwa tayari, aniruhusu hivyo tu, kama serikali imeshindwa kumuajiri yule daktari basi mimi nitatoa pesa zangu kwa kila mwezi kumlipa mpaka serikali itakapokuwa tayari, aniruhusu hapo tu. Watu wanakufa kule.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Jaku Hashim mfuatilie Mhe. Waziri kwa karibu sana ili jambo hili aliendeshe kwa mujibu wa taratibu za kisheria. Maana akitoa kauli bila ya kufuata hizo taratibu, basi atakuwa anaanza kuvunja taratibu za kisheria. Hajakataa yeye, kwa hivyo fuatilia kwa karibu na kwa sababu ya shughuli nyingi ziliopo, lakini hili kama alivyoahidi haraka iwezekanavyo kwa kupitia hizo taratibu za kisheria. Nadhani tuendelee na wewe ufuatilie kwa karibu.

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 0901 | Idara ya Utawala na Rasilimaliwatu | 886,548,000 |
| Kifungu 1002 | Idara ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano | 362,751,000 |
| | **Jumla ya Fungu** | **300,642,000,000** |

**UTARATIBU**

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Mwenyekiti, miwani yangu leo nimeisahau lakini naona hii mamlaka ya kupambana na rushwa umeitaja vile.

**Mhe. Mwenyekiti:** Kuna fungu jengine tutakuja. Kwa hivyo, tunaelekea huko, hatujasahau kupitisha fungu lake. Tunakushukuru kwa kutukumbusha.

**Jumla ya Fungu** **300,642,000,000**

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**FUNGU - 50 MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU WA UCHUMI**

Kifungu 0201 Utawala Unguja

**Mhe. Mwenyekiti:** Ndio hapa ulikuwa unapahitaji Mhe. Hamza Hassan, tafadhali.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Nilikuwa nasubiri unikumbushe.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza namshukuru sana Mhe. Waziri leo katika ufafanuzi wake yuko *very cool*, namshukuru sana kwa hili. Katika eneo hili kabla ya hapa Mhe. Mwenyekiti, na mimi ni Mtumbatu, lakini Mhe. Mtando yeye sio Mtumbatu wa chini ni Mtumbatu wa kati. Maana yake Mhe. Haji Omar yeye ni Mtumbatu wa juu, Mhe. Mtando yeye Mtumbatu wa kati Mkwajuni na mimi Mtumbatu wa Chaani. Hivyo mimi ni Mtumbatu wa chini. Mhe. Mwanasheria Mkuu na hili pia weka sawa katika msamiati wako.

Mhe. Mwenyekiti, katika eneo hili la Taasisi ya Kupambana na Rushwa, kwanza niishukuru sana serikali kwa sababu haya maoni yote tunayoyatoa hapa ya ubadhirifu na mengineyo hapa hasa ndio eneo lake. Kwa hivyo, napongeza kwa hilo kwa upande wa serikali. Mimi hoja yangu ilikuwa moja tu katika eneo hili.

Mhe. Mwenyekiti, tunaishukuru serikali kwamba tulipiga kelele na tukashauri kuwa imeundwa hii taasisi lakini haijapewa jingo. Sasa hivi wameshapatiwa eneo katika lile eneo ambalo wamepatiwa, niliwahi kushauri kwamba ule ukumbi ambao ulikuwa ukitumika na waasisi wetu, chombo cha kutunga sheria ulikuwa uwe-*revised* kwa ajili ya

kama kumbukumbu ya chombo cha kutunga sheria. Sasa hili Mhe. Waziri unajua mambo yalikuwa mengi na muda hakuwahi kulitolea ufafanuzi, labda tungesikia tu kwa upande wake alikuwa na maoni gani katika hili, ahsante Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora:** Mhe. Mwenyekiti, nataka tena nimshukuru Mhe. Hamza Hassan Juma kwa hoja yake hii, ni kweli sikupata nafasi kutokana na mambo kuwa mengi na muda, lakini mimi nataka nikubaliane naye kabisa kwa mawazo yake na mawazo haya pia yalishaambiwa na serikali kwa jumla kwamba maeneo yote yale ya kumbukumbu.

Kwa mfano lile lilikuwa ni Bunge la kwanza likifanyika pale na hivi sasa panatumika kwa shughuli za Manispaa na badala yake serikali imetupa sisi kupatumia kwa ajili ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar.

Nataka nimthibitishie kwamba kama ushauri wake alivyoutoa kwamba sisi tutatumia yale maeneo ambayo yametengenezwa au yamekatwa *partition* kwa ajili ya ofisi zetu, na ule ukumbi tutaendelea kuutunza ili kubakia na ile historia kama serikali na mawazo yake ambayo ametupa. Nataka nimthibitishie kwamba pale sisi tutakuwepo kwa muda, wakati sisi tunafanya juhudi ya ujenzi wa jengo letu basi tutahakikisha kwamba na taasisi zetu zote zinakuwepo huku na lile kama alivyoshauri na serikali ikishaamua kwamba libakie kama ni eneo la historia kwa ajili ya kumbukumbu ile ambayo ilikuwa ikifanyika hapo zamani.

Sasa maamuzi mengine ya kwamba tupewe rasmi Baraza la Wawakilishi hayo ni mambo ambayo yanazungumzika, kwa sababu sisi haja yetu tutakuwa tunataka kama Baraza la Wawakilishi kumiliki kwenye ile *property* ambazo zilikuwa zinauasili wa chombo kama chetu cha Baraza la Wawakilishi.

Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Hamza Hassan Juma kwamba jambo hili tutaheshimu mawazo yake na itabidi tupate maelekezo ya serikali na sisi ule ukumbi tutaendelea kuuheshimu. Mhe. Mwenyekiti, sisi tutautumia pia lakini sio *LEGICO*, ispokuwa tutakuwa tunatumia kwa taasisi yetu lakini akija mgeni au watu kutaka historia, basi

tutahakikisha kwamba watu tunawaelimisha kwamba jengo lile lilikuwa likitumika kwa nini.

Mhe. Mwenyekiti, kwa haya mambo mengine ya kiutawala namuomba Mhe. Mjumbe, mimi pamoja na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais tutashirikiana, ili kuona hilo jambo linakuwa endelevu. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Mwenyekiti, nashukuru tuendelee.

## TAARIFA

**Mhe. Mwenyekiti:** Nashukuru. Sasa kwa faida ya Waheshimiwa Wajumbe tu, hili wazo ambalo amelitoa Mhe. Hamza Hassan Juma ni matokeo ya *research* ambazo tumefanya katika maeneo mbali mbali na wiki iliyopita ikawa kuna semina ndogo juu ya ku-*compile* zile taarifa tulizopata katika maeneo mbali mbali.

Kwa hivyo, tumeelezwa nadhani ilikuwa ni kutoka Ghana wanacho kitengo ambacho wanaita *marketing*. Waheshimiwa Wajumbe katika suala la *marketing* ni pamoja na kuonesha, kuelezea historia za mambo yanayohusu mabunge. Sasa kihistoria tulianza kuwa na *LEGICO* ndio ilikuwa hapa na akazungumza Mhe. Hamza Hassan Juma.

Katika semina ile ulitoka ushauri kwamba maeneo yote haya tuwe nayo lakini taarifa hizi Waheshimiwa Wajumbe sote tukaae pamoja, ili tuone *the way forward* juu ya yale mapendekezo mbali mbali yaliyokuja.

Kwa hiyo, eneo lile la *Victoria Garden* jengo lake, kwenye eneo la ukumbi tulilokuwa tukiutumia zamani pamoja na hapa tulipo hivi sasa. Kwa kweli kuna mambo mengi yamekuja mapendekezo pamoja na maamuzi makubwa yaliyofanyika kwa nyakati mbali mbali. Kwa mfano, huu mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa uliamuliwa tukiwa pale, hoja ambayo ilitolewa na Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria wa hivi sasa.

Kutokana na hali hiyo basi vitu vya aina hiyo tuvitafutie utaratibu na pengine hata kutengeneza *brochures*, ili wakati wageni wanakuja na

kuwatembeza katika maeneo hayo na inawezekana ikawa ni sehemu ya kiutalii, pia wanapata *information* za mambo mbali mbali yaliyokuwepo huko nyuma. Waheshimiwa Wajumbe, hii hoja aliyoileta hapa Mhe. Mjumbe inahusiana na kile ambacho tulikifanyia *research*.

Vile vile Waheshimiwa Wajumbe nataka nikwambieni kwamba serikali inanidai yale mambo ambayo tumeyafanyia kazi, kwa ajili ya kuboresha ile Sheria ya Utawala wa Baraza basi ninadaiwa sasa mimi na serikali kwamba tufanye haraka. Kwa hivyo, nataka nikupeni hiyo taarifa tu, mujue kwamba tunafanyakazi kweli kweli, ndio ile nilipokuwa pale kwenye kiti nikasema jana tumefanyakazi mpaka saa 5 za usiku, kwa ajili ya kufanikisha mambo mbali mbali yale ambayo Waheshimiwa Wajumbe mnayaelekeza na kuyaagiza yafanyike, Kwa hivyo hata na mimi naingia kazini. *(Makofi).*

Nashukuru kwa taarifa hiyo, nilitaka muijue hiyo, tuendelee.

**FUNGU 50 – MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU UCHUMI**

| | |
|---|---|
| Kifungu 0201 Utawala Unguja | 810,000,000/= |
| **Jumla ya Fungu** | **810,000,000/=** |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe kabla ya kwenda kwenye fungu la maendeleo tumalize matumizi kwenye kitabu kile cha pili, yaani lile buku kubwa Waheshimiwa Wajumbe.

**FUNGU 47 – KAMISHENI YA UTUMISHI**

**UTARATIBU**

**Mhe. Mbarouk Wadi Mussa:** Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa naangalia kwenye (b) vifungu vya fungu hili vinavyooneshwa hapa chini matumizi yake yatasimamiwa na Katibu Mkuu au ni Katibu wa Kamisheni ya Utumishi, na hapa nataka ufafanuzi kidogo.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Waziri, tupate ufafanuzi wa hapo ili isijekuwa kila mmoja anang'ang'ania kazi yangu mimi. *(Makofi).*

**Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora:** Mhe. Mwenyekiti, Katibu wa Kamisheni ni Katibu, lakini *status* yake ni sawa sawa na Katibu Mkuu wa Wizara, yaani *status* ya Katibu wa Tume alivyo Katibu Mkuu ndivyo alivyo Katibu wa Kamisheni, lakini usahihi anatamkwa Katibu wa Kamisheni.

**Mhe. Mwenyekiti:** Kwa hivyo, anayesimamia sio Katibu Mkuu wa Wizara, isipokuwa ni Katibu wa Kamisheni.

**Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora:** Mhe. Mwenyekiti, Katibu wa Kamisheni *status* yake ni sawa sawa na Katibu Mkuu kwa mujibu wa sheria.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Waziri, sasa hapa tuweke vipi?

**Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora:** Mhe. Mwenyekiti, tuweke Katibu wa Kamisheni ya Utumishi wa Umma.

**Mhe. Mwenyekiti:** Kwa hivyo, ile Mkuu tuiondoe.

**Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora:** Mhe. Mwenyekiti, ile Mkuu tuiondoe.

**Mhe. Mwenyekiti:** Sasa haya ondoa Mkuu. Mhe. Mbarouk Wadi Mussa tunakushukuru.

## FUNGU 47 – KAMISHENI YA UTUMISHI

**Mhe. Salmin Awadh Salmin:** Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Wakati nilipokuwa nikichangia hotuba hii ya Mhe. Waziri nilitumia kifungu cha Kanuni cha 96(6)(b) kwa kuondosha shilingi mia moja katika fungu hili la Kamisheni ya Utumishi kama sikupata majibu juu ya hoja yangu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba unipe muda kidogo katika siku ambayo Mhe. Waziri yuko *fit* basi ni leo, yaani yuko *fit* sana kwa sababu amejaribu kujibu hoja zetu kwa utulivu, yaani ametulia hana jazba. Kwa hivyo, nimuombe aendelee Mhe. Waziri kuwa katika *moody* hiyo hasa katika vyombo hivi vya Bunge, kwa sababu mna *pressure* nyingi humu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, wakati Mhe. Waziri akijibu hoja ameeleza mambo mengi lakini moja kati ya mambo ambayo ameyaeleza wakati alipokuwa akijibu alihusisha wadhifa wangu wa chama kama ni Mnadhimu wa Chama na hiyo hii iliopo mbele yetu. Kwa hivyo, ninachotaka kusema Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba Chama cha Mapinduzi kina miongozo yake, kuna Katiba, Sheria pamoja na Muongozo wa Chama na sisi wanachama tunawajibika au tunalazimika kufuata. Kwa kweli suala la uwajibikaji ni sera ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Kwa hivyo, sisi sote ni wanachama wa Chama cha Mapinduzi iwe waziri au Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi anatakiwa atekeleze sera ya uwajibikaji ya Chama cha Mapinduzi na pia kinapiga vita sana wizi na rushwa. Mhe. Mwenyekiti, nilichokuwa nikikifanya ni kutekeleza sera ya Chama cha Mapinduzi kuhimiza uwajibikaji na mimi nitaendelea kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, niwaombe sana Waheshimiwa Mawaziri wetu hususan wale wa Chama cha Mapinduzi kwamba wawajibike. Kwa kweli wasije wakafikiria au wakafika pahala wakaona Chama cha Mapinduzi kitawalinda kwa kutowajibika, Chama cha Mapinduzi kisitumike kama kichaka cha kufichia maovu. *(Makofi)*

Baada ya maelezo yangu Mhe. Mwenyekiti, sasa niendelee kwa kumnukuu Mhe. Waziri pale aliposema kwamba, ‘Watumbatu na Wamakunduchi wana uungwana unaofanana’, ni kweli Mhe. Mwenyekiti na mimi nataka kuutumia uungwana huo unaofanana.

Kwa kweli kule Makunduchi kuna kijiji kinaitwa Nganani nafikiri tunakijua. Kijiji kile chimbuko lake, yaani wakaazi wake ni kutoka Tumbatu na wavuvi wametokea Tumbatu kwa bahati wakaharibikiwa pale katika maeneo ya bahari ya Nganani wakaweka nanga pale

wakateremka wakakaa pale Nganani, kwa hivyo hawakuondoka tena na leo wanazaliana. Kwa hivyo, nakubaliana na kauli ya Mhe. Waziri kwamba uungwana wa Watumbatu na Wamakunduchi unafanana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikijenga hoja ya kutaka kuondosha shilingi mia katika fungu hili ni kwa sababu ya uwajibikaji wa Kamisheni ya Utumishi.

Sisi zamani kule kwetu tulipokuwa wadogo, mzee wako anapokwambia ukatwange au ukachote maji, basi kama hukutwanga au hukuchota maji, maana yake siku ile hupewi chakula au kama kitachukuliwa kibichi ufunikiwe pale na ukiuliza chakula chako kiko wapi? Utaambiwa kile pale, ukifunua kibichi kwa sababu hukutwanga au hukuchota maji na hiyo inakuwa ndio adhabu yako. Sasa na mimi nilivyokusudia niipe adhabu hii Kamisheni kwa kutowajibika katika suala hili la chombo kikubwa kama hichi. *(Makofi).*

Wakati Mhe. Waziri alipokuwa akinijibu alisema kwamba muundo umeidhinishwa, lakini akijua kwamba hakuna muundo ulioidhinishwa huo tuliokusudia sisi, isipokuwa kilichoidhinishwa ni miundo ya utumishi kwa kada katika utumishi wa Baraza la Wawakilishi. Lakini ule muundo wa ofisi bado haujaidhinishwa mpaka leo ambao hiyo ndio tunayoizungumzia hapa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikieleza nimwambie tu anipe sababu ya kwamba muundo huu hadi leo ni kwa nini haujaidhinishwa na Kamisheni ya Utumishi, ambao ni wajibu wao. Vile vile kuna kitu ambacho alieleza Mhe. Waziri kwenye maelezo yake kwamba Kamisheni ya Utumishi haimalizii kwa mujibu wa sheria kuidhinisha moja kwa moja *unless* baadae ipeleke kwa Mhe. Rais, alieleza kitu kama hicho kwa mujibu wa sheria yake ya utumishi.

Sasa unaporekebisha muundo (*structure*), maana yake unahitaji fedha, kwa hivyo Mhe. Rais lazima alikubali hili na aliidhinisha. Kwa hivyo, mimi nilitaka Mhe. Waziri anipe ufafanuzi na wala sina tabu na jambo hili, isipokuwa natumia ule uungwana Wakimakunduchi na Wakitumbatu. Je, huu muundo umeshafika mezani kwa Mhe. Rais ili aukubali au aukatae?

Mhe. Mwenyekiti, juzi kuna mwananchi wangu mmoja alinilalamikia juu ya kesi yake kwamba haijapelekwa mahakamani, alipokwenda kwa *RPC* wa Mkoa akaambiwa kwamba *file* lako ameliita Kamishna wa Polisi. Mimi nikamwambia basi twende kwa Kamishna na tulikwenda kwa Kamishna, basi tukamueleza *file* la huyu mama la kwenda Mahakamani umeliita wewe kutoka kwa *RPC* sasa tumekuja kulikwamua huku. Kwa hivyo, alichokifanya Kamishna ni kunyanyua simu na kumpigia *RPC* na kumueleza hilo *file* liko mkononi hapa nakusudia kukuletea leo. Kwa kweli lugha hizi mara nyingi za kiutawala kwamba tuko hivi pengine utekelezaji halisi haupo.

Kutokana na hali hiyo, ninamuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, atupe uhakika kama suala hili limesimama kwa Mhe. Rais juu ya uidhinishaji na wao wenyewe Kamisheni wameshaidhinisha, basi kupitia Baraza hili tumuombe Mhe. Rais akubali kuidhinisha ili hawa wafanyakazi wetu waweze kupata haki zao kwa mujibu wa sheria na mimi akisha kuniambia hapo sina tatizo, kwamba *file* lipo kwa Mhe. Rais tunasubiri majibu ya Mhe. Rais, basi kutumia kikao hichi cha Baraza la Wawakilishi tumuombe Mhe. Rais alikubali hili ili wafanyakazi wetu wapate *rights* zao.

Mhe. Mwenyekiti, najua Mhe. Rais hana matatizo tena analipenda Baraza la Wawakilishi na anawapenda wafanyakazi wa Baraza la Wawakishi na tukimuomba tu atuidhinishie, basi jambo hili ataliidhinisha na kwa sababu ni katika mipango yake. Kwa mfano, juzi nilisoma *hansard* na moja ya mikakati yake Mhe. Rais ni kuboresha maslahi ya wafanyakazi katika ngazi tofauti. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti namuomba Mhe. Waziri anipe ufafanuzi juu ya jambo hilo. *(Makofi)*

## UTARATIBU

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Mhe. Mwenyekiti, kusema kweli hoja ambayo anayoizungumza Mhe. Salmin Awadh Salmin na hata hivyo anavyosisitiza kwanza ni ya msingi sana na ikipata maelezo naamini kila mtu atafurahi na mimi naamini kwamba maelezo hayo yapo.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, wakati hoja hii akiichangia Mhe. Makame Mshimba Mbarouk mimi binafsi niliwahi kunyanyuka kuomba suala la

utaratibu, kwamba kwa mujibu wa Kanuni yetu ya 48 kifungu cha 7 mjumbe haruhusiwi au hawezi kuzusha jambo ambalo limeshajadiliwa katika ama kikao hichi au kikao kilichopita.

Kwa hivyo, baada ya kumueleza suala hili la maslahi, miundo na kupata uamuzi kuhusiana na suala hili kwa watumishi wa Baraza la Wawakilishi ni kweli tumelizungumza muda mrefu.

Lakini siku ambayo tulipokuwa tukijadili bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Hamza Hassan Juma aliliibua kwenye fungu la uratibu na serikali na wewe mwenyewe nakumbuka ulikuwa ni mwenyekiti na ukamwambia kwa nini basi usisubiri kwenye fungu la Baraza la Wawakilishi, lakini yeye ni mtaalamu alijua kwa nini amelileta kwenye uratibu kwamba pale ndipo serikali inaratibu shughuli zote hizi.

Kutokana na hali hiyo, serikali ikatakiwa kuchukua ahadi ya kulimaliza, kulifuatilia pamoja na kulipatia ufumbuzi suala hili na serikali maana yake kama kuna mtu mkubwa katika mawaziri basi ni Mnadhimu wa Serikali na ikachukua ahadi hiyo. Mimi nikawakumbusha kwamba kutokana na ahadi hii mwenyewe Mhe. Spika suala hili aliitisha kikao kwa ajili ya kulijadili kufuatia ahadi ile ya serikali.

Sasa jambo hili leo tukilizungumza tena hapa wakati ile ahadi iliyochukuliwa na serikali inaendelea kutekelezwa ni kinyume na Kanuni yetu ya 48 fasili ya 7. Mhe. Mwenyekiti, akatoa uamuzi kumwambia Mhe. Makame Mshimba Mbarouk kwamba suala hili kweli kwa mujibu wa Kanuni zetu hatupaswi tena kulizusha tena ndani ya kikao hichi, kwa sababu tayari limeshachukuliwa ahadi na ahadi ile imo katika kutekelezwa.

Mhe. Mwenyekiti, tukiangalia Kanuni yetu ya 58 fasili ya 5 Mwenyekiti akishatoa uamuzi kuhusu suala lile, basi hatuwezi tena tukaanza kulirejea. Kwa hivyo, Mhe. Salmin Awadh Salmin aliendelea na akalizungumza lakini unaweza kusema kwa mujibu wa Kanuni hoja ile haikuwa sahihi kuzungumzwa kwa sababu umeshatoka uamuzi wa Mwenyekiti kwamba suala hili kwa mujibu wa Kanuni ya 48 fasili ya

7 hatutakiwi kulizungumza au kulijadili ama kulizusha tena katika kikao hichi.

Kwa maana hiyo, Mhe. Mwenyekiti, labda utupe muongozo katika hili lakini mimi nadhani kwamba na wala si kwa sababu ya kwamba hatutaki majibu yatoke au hayapo, isipokuwa ni kwa mujibu wa utaratibu.

Kwa hivyo, na mimi nasema Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu ya Kanuni hizo hizo ndio maana umekaa hapo huna joho, lakini ungeweza kuteremka na joho na hili rungu dada yetu anakuja mara kwa mara analifunika na kulifunua kwa sababu ya utaratibu, lakini lingeweza kukaa limefunuliwa na tukaendelea na shughuli zetu. Sasa hiyo ndio katika kulinda hizo Kanuni na labda utuongoze katika hili. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Salmin Awadh Salmin, umepata maelezo hayo na sijui kama utataka na mimi niseme mengine kidogo.

**Mhe. Salmin Awadh Salmin:** Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mwanasheria amezungumzia Kanuni ya 48 kifungu cha 7 na mimi naomba nikinukuu kwanza.

Kanuni ya 48 kifungu cha 7 kinaeleza hivi:-

"48(7) Mjumbe yeyote hatoruhusiwa kufufua jambo lolote ambalo Baraza lilikwisha kuliamua '*Mhe. Mwenyekiti, nadhani namna ya kuamua unajua ni kujenga hoja kwamba waliokubali na waliokataa juu ya hoja hiyo'* ama katika mkutano uliopo au ule uliotangulia, isipokuwa kwa kufuata masharti ya Kanuni ya 49 kifungu cha 3"

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuisoma Kanuni ya 49 kifungu kidogo cha 3.

Kanuni ya 49 kifungu kidogo cha 3 inaeleza hivi:-

> "49(3) Taarifa ya hoja ambayo kwa maoni ya Spika ina madhumuni ya kujaribu kutaka lifikiriwe tena jambo ambalo lilikwisha kuamuliwa na Baraza katika kipindi cha zaidi ya miezi kumi na mbili iliyopita kabla ya kikao kinachoendelea litakubaliwa".

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kulitaka Baraza lako kutaka kuamua juu ya kuendelea na hoja hii au laa, kwa sababu hoja iliopo mbele yetu ni hoja ya Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ndio hoja iliopo mbele yetu.

Sasa kama kuna wajumbe waliochangia hotuba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa wakati ule, basi ni hoja ambayo ilikuwa mbele ya wakati ule lakini hoja tuliyonayo sasa ni hoja ya Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora na ndio tunayoijadili na ndio kwenye taasisi hii ya Kamisheni ya Umma.

Mhe. Mwenyekiti, kama kuna mtu alizungumzia habari ya taasisi katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, nadhani ilikuwa Mhe. Mwanasheria amjengee hoja kwamba hii hoja haiko mbele yako, pia kanuni hii inakataza kuzungumzia hoja ambayo iko mbele ya kikao kile.

Kwa hivyo, kwa wakati ule kama ilikuwa Mhe. Makame Mshimba Mbarouk alikuwa anazungumzia hoja ambayo haiko mbele yake kwa mujibu wa Kanuni hii ndipo alipokuwa anatakiwa ajenge hoja. Lakini leo tunazungumzia hoja ya Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ndio hoja iliopo mbele yetu. Mhe. Mwenyekiti, nadhani sifanyi makosa kuzungumzia juu ya hoja iliopo mbele yetu hivi sasa. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, Mhe. Mwenyekiti naomba uniachie niendelee kujenga hoja na kwa sababu ndio hoja iliopo mbele yetu na wala hakuna hoja isiyokuwa na majibu na Mhe. Mwanasheria Mkuu asijaribu kupindisha mambo kila swali lina majibu. Kwa hivyo, Mhe. Mwanasheria Mkuu asijaribu kutumia vifungu vya sheria kutaka

kutubabaisha hapa. Kwa kweli hapa kila kitu kinakwenda kwa mujibu wa taratibu. Mhe. Mwenyekiti, hoja iliopo mbele yetu ni ya Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora na ndio tunayoijadili hapa. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, nakuomba sana uniruhusu niendelee kwa sababu ndio hoja iliopo mbele yangu, kama kuna mjumbe alijenga hoja ya Kamisheni ya Utumishi katika hoja ambayo haihusu, basi huyo ndiye alikuwa na haki ya kuzuiliwa kuendelea na hoja. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Mwanasheria Mkuu, kaa kitako kidogo. Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora, unayo maelezo kidogo.

**Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa kutoa ufafanuzi, pia nimshukuru Mhe. Salmin Awadh Salmin kwa kutetea hoja yake.

Kwa kweli kuna hoja mbili ambazo zimewasilishwa, kama nilivyosema katika majumuisho yangu na Mhe. Salmin Awadh Salmin kama nimempata vizuri, anazungumzia hoja ya *structure* ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikitoa ufafanuzi nilisema kwamba kuna maombi ya aina mbili ambayo yalipelekwa Kamisheni ya Utumishi wa Umma na Tume ya Utumishi. Kwa bahati nzuri Kamisheni kila ombi inapolipokea hufanya hima ya kuweza kujibu aliyempelekea ombi na tunatumia *system* hiyo na ndio maana ya utawala bora, yaani ukishapokea maombi au barua unatakiwa umrejeshee yule ambaye amekuletea angalau kumwambia kwamba ombi umelipokea na huo ndio utaratibu.

Kwa hivyo, suala zima la *scheme of service* ya Baraza hilo ndio nimesema limekwisha na wala halina matatizo, isipokuwa *scheme of service* iliyorejeshwa isioambatana na mishahara na taratibu za mishahara yaani *salary structure* marekebisho hayo yanataratibu zake kwamba Kamisheni ikishapelekewa inafanya *consultation* na Wizara ya Fedha na Wizara ya Utumishi, yaani Ofisi Kuu ya Utumishi na

hatimaye wanarudi na wakishakupata maamuzi, hayo maamuzi yanapelekwa kwa Mhe. Rais. Hilo nafikiri hana tatizo nalo kama nimemuelewa. Tatizo lake ni juu ya muundo wa Baraza lenyewe, yaani zile nafasi za uongozi za Baraza la Wawakilishi au ule muundo wa ile *structure* ya Baraza la Wawakilishi kwamba kuna Katibu kuna na Wakurugenzi.

Kwa mujibu wa maamuzi yaliyofanyika siku za nyuma na Tume halali ya Utumishi wa Baraza la Wawakilishi, kwa watu au viongozi waliokuwa wanajulikana kama ni Wakurugenzi hilo halina tatizo, hao wataendelea kuwepo kuwa ni Wakurugenzi na Ofisi ya Utumishi na Kamisheni inawatambua kwa mujibu wa sheria. Kwa sababu sheria inasema kwa yale maamuzi ambayo yalifanywa siku za nyuma na chombo halali kisheria, sheria hii inatambua maamuzi hayo.

Lakini katika muundo wa sasa wa Baraza la Wawakilishi ameongezeka Mkurugenzi mwengine mmoja. Sasa huyu kwa sababu hakufanyiwa maamuzi na ile Tume inabidi sasa huyu azingatiwe upya. Hata hivyo Mkurugenzi huyu Ofisi Kuu ya Utumishi imemtambua na baadhi ya zile stahili zake nyengine anastahiki kulipwa. Lakini ile *structure* yenyewe ya jinsi gani tunataka uongozi wa nafasi za Baraza iwe, hiyo Kamashini wamepokea. Kiliitishwa kikao wakashirikishwa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwenda kujadiliana kwa sababu waliombwa na wao wawepo na wanaendelea kulifanyia kazi.

Kwa sababu Kamisheni kama nilivyosema siyo yule Katibu ambaye Mhe. Mtando ametaka tumuweke wazi hapa ni Katibu Mkuu au ni Katibu. Kamisheni ni ile Kamisheni ni wale Makamishna. Sasa wale kufanya kazi kwao hutokana na vikao. Mimi nataka niseme kwamba si muundo wa taasisi moja ya Baraza la Wawakilishi kama nilivyosema, iko miundo ya taasisi nyingi ambazo zimeshafikishwa pale kwenye Kamisheni hiyo wanaendelea kuifanyia kazi ili wapate maamuzi ya kumpelekea Mhe. Rais. Lakini jengine ni kutokana na mapendekezo yetu mapya ambayo tumejadili sana kule shamba, pengine kutahitahitajika vile vile kuzingatia upya juu ya hayo mapendekezo. Sasa tusende huko kwa sababu huko pengine itakuwa mbali sana.

Lakini kwa *spirit* ya serika na Baraza la Wawakilishi Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, nalazimika kusema kwamba tumekubaliana hilo jambo halina tatizo, tukae katika kuona tunafanyaje ili tuweze kulipatia ufumbuzi. Huyo Mhe. Rais ambaye atapelekewa ameshatoa ahadi ya kusema kwamba likifika yeye ataliamua.

Sasa kazi yangu mimi ni kuwahimiza Kamisheni walifanyie haraka kulikalia, kwa maana ya kukaa kwenye vikao vinavyohusika wakaidhinisha rasmi halafu baadaye hili jambo likaweza kupelekwa kwa Mhe. Rais na Mhe. Rais aweze kuidhinisha.

Sasa nataka nimuhakikishie Mhe. Salmin tumefikia pahala pazuri katika jambo hili. Nataka Mhe. Salmin aniamini nilisema jambo hili kwamba ni la kisera na ni la kisheria na mimi ndio *policy maker* wa Wizara hii. Alifanya vizuri kuzuia mshahara wangu kwa sababu akijua kwamba alizuia fungu la Kamisheni sawa, naomba radhi alizuia fungu hili lakini nimuombe Mhe. Salmin akizuia hili fungu maana yake hawa Makamishna hawataweza kufanya kazi.

Mimi nimuombe kwa heshima zote kabisa kwamba aturuhusu tuendelee, *commitment* iliyofanywa kati ya viongozi wakuu wa mihimili miwili mbele ya shahid Mhe. Spika, sijui kama mlinielewa pale nilipokaza mguu kwa Mhe. Spika na Mhe. Makamo wa Pili wa Rais, nilikuwa nawakumbusha jambo ambalo jana tumeliamua.*(Makofi)*

Kwa hivyo Mhe. Salmin Awadh Salmin nataka uniamini kwamba mimi kama *policy maker* nitahakikisha hili jambo lipatiwa ufumbuzi na Mhe. Rais analipata kwa mujibu wa taratibu na analifanyia maamuzi sahihi kabisa yale ambayo tutakuwa tumekubaliana pale tulipokuwa tumeshauriana. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala hili sio kwamba maelezo hayapo, maelezo yapo lakini mimi nilidhani kwamba ile kazi tuliyokabidhiana pengine ile *massage* imeshafika kwa wahusika. Lakini kwa sababu nimetakiwa nitoe maelezo hayo hapa naomba nimthibitishie Mhe. Salmin Awadh kwamba makubaliano nimeshayasikia jana chini ya usimamizi wa viongozi wa mihimili miwili. Mhe. Rais, Mhe. Spika, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais na mimi ambaye nasimamia, na ndio maana

nikaendelea kukaza mguu kwa hili jambo sasa nikitoka hapa nakaza buti, kazi mbele na sio kurudi nyuma.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Salmin Awadh Salmin, yapokee hayo maneo, hicho kikao nilikiomba mimi ambacho maelezo anayoyasema Mhe. Waziri, kwa hivyo tulimalize hili jambo ili tuendelee.

**Mhe. Salmin Awadh Salmin:** Mimi kama utangulizi wangu nilivyosema kwamba leo Mhe. Waziri ni siku yake, siku ya Jumatano leo, kwa hivyo siku yako leo uko kwenye *moody* nzuri sana. Lakini kwa kuwa Mhe. Mwenyekiti, hapa tunaozungumzia ni muundo wa chombo ambacho unakiongozi wewe. Chimbuko hili limetokana na Kamati ya Uongozi kila wakati tumekuwa tukipokea mabarua juu ya muundo. Kikao cha mwisho wewe shahidi Mhe. Omar, ambaye ni Mjumbe wa Kamati ya Uongozi aliiambia ofisi kwamba jambo hili msituletee tena, malalamiko haya msituletee tena, tunataka tukayaamue huko chini na wewe ukiwa shahidi.

Kwa bahati nzuri wewe leo Mhe. Waziri wa Utumishi amekutaja ni miongoni mwa uliokwenda kwa Mhe. Rais na wewe ndio *head* wa chombo hiki, hivyo nataka utoe kauli hapa kwamba jambo hilo alilozungumza Mhe. Waziri wa Utumishi wa Umma, ni sahihi na halina tatizo na litatekelezwa. Ukishakutoa fatwa hiyo sisi hatuna wasi wasi. Ahsante *(Makofi).*

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe hichi chombo kinasimamiwa na mimi. Tumefanya vikao vingi kweli na niliahidi katika Kamati ya Uongozi kwamba itakapofika pahala mambo nayaona hayakati sawa nitakwenda kwa mwenzangu, kama vile nilivyokwenda kwa ajili, tena na wewe mheshimiwa ulishiriki kwa ajili ya mambo yanayowahusu Wajumbe. Wajumbe sisi hatuwezi kufanya kazi zetu vizuri sana bila ya kuwa na watendaji wetu wakawa wanatusaidia vizuri ili waweze kufanya hivyo basi ni lazima maslahi yao yaangaliwe.

Nilianza kuitisha kikao hichi shambani, nilikukaribisha na wewe na Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti akiwa vile vile na Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi ya Viongozi Wakuu, Mhe. Waziri Mohammed Aboud, Mhe. Mwanasheria Mkuu tulikuwa

pamoja, tukaitisha kikao hicho kwa madhumuni ya kuona *the way forward* juu ya jambo hili ambalo ni muhimu. Jana sikuwepo kitini wakati wa michango inaendelea lakini nikapata habari kwa sababu nilikuwa nafuatilia kwa karibu sana juu ya suala hili, nikaona hapana inavyoonekana muongozo tulioutoa pale shambani. Tukamuachia Mhe. Waziri wa Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais kwamba yale ambayo yatakuwa katika mikono yake atayatekeleza lakini yale ambayo yanahitaji maamuzi ya Mhe. Rais ameyataja hapa akamuone.

Bahati nzuri Mhe. Rais alikuwa safarini akanipigia simu huko huko kwa kutekeleza yale tuliyoondokea pale. Mimi nilipoona kwamba sijapata jibu kutoka kwa Mhe. Waziri nikaona hapana, nikamfuata *Air Port*, anaingia tu nikamnong'oneza hilo jambo. Kwa sababu najua tuna dhamana tumechukua na tunakusudia kutengeneza mambo yanayohusu watumishi wetu wa Baraza. Kikao kikaitishwa kama alivyosema Mhe. Waziri wa Utumishi wa Umma, tumeifanya kazi hiyo mpaka karibu saa 5 za usiku ndio ile niliyosema na haikuwa hiyo tu kwa sababu nilimueleza mapema Mhe. Rais, kwamba kuna jambo linakuja kuhusu ile Sheria ya Utawala wa Baraza. Akasema ninakudai uniletee hiyo, haraka sana.

Kwa hivyo nataka muelewe kwamba kweli kikao hicho kilikuwepo na Mhe. Rais anasubiri aweke mkono kuidhinisha haya mambo yote. Anasubiri na sheria ya Utawala wa Baraza na mimi nilimueleza mapema kwa sababu sikutaka tuwe tunaficha jambo. Mambo yetu yawe *public* yaeleweke, hatukuwa tunafunika funika serikali, ziara zote zile nilimueleza kwa sababu na yeye ni sehemu ya chombo hichi na tukakubaliana kwamba sawa fanya hiyo kazi na jana akanambia fanya haraka hilo jambo ulilete.

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu alieleza kwenye kikao lakini kule kule shambani, kwamba tujitahidi isije ikafika Oktoba huko, ikawa hili jambo bado. Ninakaza buti tuone kwamba mambo yote hayo yatakwenda vizuri pamoja na hili ambalo Mhe. Rais anatusubiri sisi sasa. Yeye yupo tayari zaidi pengine kuliko sisi. Kwa hivyo nathibitisha kwamba haya mambo yametokezea na hiyo kazi tunaifanya na nikuombe Mhe. Mjumbe pamoja

Waheshimiwa Wajumbe wote tukubaliane tuendelee juu ya jambo hili na kazi inafanyika.

**Mhe. Salmin Awadh Salmin:** Ahsante sana kwa maelezo yako na kwa kweli naamini wajumbe wengi yamewaridhisha sana. Kwa hivyo narudisha sasa shilingi mia katika fungu 47 ili tuwaruhusu Kamisheni wakaendelee kufanya kazi zao kwa uadilifu na kwa imani kabisa na kwa kutekeleza maelekezo ya Mhe. Rais. Ahsante. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Nina hakika Mhe. Waziri shilingi mia zake anazipokea.

*(Baraza lilirudia)*

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe kazi imebakia kidogo kumaliza lakini muda uliobaki hautuwezeshi kumalika kazi hiyo.

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Spika, kwa kuwa muda uliombele yetu hautoshelezi kumaliza kazi iliyombele yetu. Hivyo naliomba Baraza lako liweke kanuni ya muda kando ili tuweze kumaliza shughuli iliyo mbele yetu. Naomba kutoa hoja.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe leo hatutofika saa 4:00 tutaondoka mapema.Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wanaokubaliana hoja wanyanyue mikono, wanaokataa hoja, waliokubali wameshinda.

*(Hoja ilitolewa Iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Hapa Baraza lilirudia)*

## KAMATI YA MATUMIZI

**Mhe. Ismail Jussa Ladhu:**Mhe. Mwenyekiti, nina nukta ndogo sana lakini kabla ya kuizungumza nukta hiyo nadhani nitakuwa sitendi haki kwangu kwa Wajumbe wa Baraza hili na kwa wananchi wote ambao

wanakitegemea chombo hichi ikiwa sitotanguliza kwanza pongezi na shukurani zangu na zetu sote za dhati kwako.

Mhe. Mwenyekiti, siku zote tunapokumimia sifa huwa tunafanya hivyo kwa sababu umekuwa ni muhimili muhimu wa muhimili huu. Tunashukuru sana kwamba unakijengea heshma chombo chetu na unakilindia hadhi na haiba na heshma yake. Lakini vile vile nataka nimpongeze Mhe. Salmin Awadh kwa kuisimamia hoja yake vizuri. Kasema na hii ni kwa ajili ya kuweka *record* tu kwamba hapa tukifanya kazi hasa katika mfumo huu tulionao wa muunda wa Umoja wa Kitaifa wa Serikalini yetu, hatutizami sana vyama.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niliilaza bajet ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais hapa. Ni kwa sababu katika mambo haya hatutizami nani anayeongoza wala tunaongozwa na chama gani. Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, nije katika nukta yangu ndogo tu.

Mhe. Mwenyekiti, nimesikiliza kwa makini mijadala yote. Nilipokuwa nikichangia pia niligusia nukta inayohusu Kamisheni ya Utumishi wa Umma na suala zima la muundo wa utumishi wa Baraza. Lakini mimi sikwenda kule ambapo wenzangu walikwenda. Mimi nilizungumza na nikakinukuu kifungu cha 77(1) cha Katiba ya Zanzibar, hichi kinasema hivi:

> "77(1) Kutakuwa na Ofisi ya Baraza la Wawakilishi itakayoongozwa na Katibu wa Baraza la Wawakilishi na itakuwa na nafasi za madaraka kama itakavyoidhinishwa na Tume ya Utumishi ya Baraza la Wawakilishi"

Mhe. Mwenyekiti, nilisema hili kwa sababu kimsingi napata tabu kidogo tangu siku tulipokuwepo kule *Zanzibar Beach Resort* aliponyanyuka Katibu wa Kamisheni ya Utumishi wa Umma kusema kwamba hata Idara za Baraza la Wawakilishi na Wakurugenzi wake zinapaswa zikaidhinishwe na Rais. Ilinitatiza sana mimi kwa sababu huu ni muhimili peke yake.

Sasa hapa pametoka ufafanuzi na wala sitaki kulirudisha nyuma Baraza, wala sikusudii kuibua mjadala mpya, wala kuomba kuzuia

fungu. Ninachoomba tu hili suala mimi nadhani Mhe. Mwenyekiti, tukubali kwamba katika marekebisho ya 10 katika suala la kuingizwa kwa Kamisheni ya Utumishi wa Umma kumekuwa na mkanganyiko baina ya kifungu hichi na kile kifungu kilichoingizwa katika Kamisheni ya Utumishi wa Umma, sote tulikubali Mhe. Mwenyekiti, na sisi ni binadamu. Kwa hivyo nimesimama hapa Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu nililichangia hili kuiomba serikali itafute njia ya kufanya marekebisho juu ya hili, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na Serikali kwa jumla wakae.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa navitazama vifungu vyengine vya Tume zote za Utumishi zile ofisi zao zinazohudumiwa hazikupewa mamlaka kama haya ambayo imepewa Ofisi ya Baraza la Wawakilishi. Ukitizama Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 117 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kinazungumzia Tume ya Utumishi serikalini. Hichi kinazungumzia Tume ya Utumishi serikalini, hichi kinasema tu,

> "117 Kutakuwa na Tume ya Utumishi serikalini hichi kinasema tu kutakuwa na Tume ya Utumishi ya Serikali kama itakavyooelezwa na sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi,"

Ikaishia hapo. Haina Ofisi inayoambatana nayo ikapewa madaraka kama ilivyopewa Ofisi ya Baraza la Wawakilishi na Katibu wake.

Ukija katika ibara ya 102. Tume ya Utumishi ya Mahakama inasema:

> "102 Kutakuwa na Tume ya Utumishi ya Mahakama ambayo muundo kazi na uwezo wake utakuwa kama ulivyoelezwa na sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi."

Ikaishia hapo. Ukija Mhe. Mwenyekiti, katika idara maalum ibara ya 122 inasema:

> "ibara ya 122 Kutakuwa na Tume ya Utumishi Idara Maalum ambayo uwezo wake, nguvu zake, kazi zake na kanuni za mwenendo wake zitakuwa kama zitavyoainishwa katika sheria

itakayotungwa na Baraza la Wawakilishi kwa ajili hiyo."

Mhe. Mwenyekiti, kwenye Baraza la Wawakilishi tu na nadhani kwa sababu uzito, ukubwa na umuhimu wa chombo hiki ndio kifungu cha 77 (1) Tume ya Utumishi ya Baraza la Wawakilishi na jukumu la kuidhinisha nafasi na Ofisi za madaraka katika Baraza la Wawakilishi zilizokuwa chini Katibu wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 116 kinachoainisha Kamisheni ya Utumishi wa Umma. Sawa kimesema kwamba kutakuwa na Kamisheni ya Utumishi wa Umma ambayo itakuwa ni chombo cha juu kabisa kwa Tume zote za Utumishi ya Mamlaka ya kusimamia na kuratibu mambo yote ya Utumishi wa Umma wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kule kwenye 77(1) kumetoa mamlaka kwa Ofisi ya Baraza la Wawakilishi kuanzisha Ofisi kama zitakavyoidhinishwa na Tume ya Utumishi ya Baraza la Wawakilishi. Mhe. Mwenyekiti, *point* yangu ni kwamba zile Tume za Utumishi nyengine zote hazikupewa wala hazikuunganishwa kimadaraka na ile Ofisi inayohudumiwa na Tume ya Utumishi ile kama ambavyo Ofisi ya Baraza la Wawakilishi imeunganisha na Tume ya Utumishi ya Baraza la Wawakilishi.

Tatizo langu ni kwamba kifungu cha 116 cha Katiba tulikitafsiri ndio maana kila wakati kinaleta matatizo na mtafaruku baina ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wanapolinda hadhi yao ya kutumia kifungu cha 77(1) na kile cha serikali. Kwa hivyo nilikuwa nasema nimesimama hapa kwa sababu nimechangia hili katika mchango wangu. Naiomba serikali hebu hili ikalikalie tena ikalifanyie kazi. Kama kuna utatanishi katika vifungu hivi turekebishe ili hadhi na heshma ya chombo cha Baraza la Wawakilishi kama muhimili wa dola muhimu sana ambayo mara nyingi ndio wanaotunga sheria na zinazoongoza mihimili mengine yote, ipate kuenziwa na kuheshimiwa kama ilivyokusudiwa na wananchi wa Zanzibar ambao ndio wadhamini *sponsor* wa Katiba zao. Naomba hilo tu Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mimi nafikiri ameomba jambo ambalo tunalifanyia kazi na katika mazungumzo hayo hayo ya jana masuala

yanayohusu marekebisho mbali mbali yatakuja kufuatana na sheria hiyo, tutakayoipendekeza kwamba serikali imetutaka tuharakishe jambo hilo ili tufikie pahala tulimalize.

Kwa hivyo michango ya aina hii na mambo mengine yote yatakayokuja yanaweza yakafikia kurekebishwa kufuatana na sheria hiyo wakati wake ukifika. Kwa hivyo nikuombe Mhe. Ismail Jussa Ladhu tukae pamoja na hili jambo kimsingi kama vile tulivyokubaliana pale shamba tutakuwa na semina ya kupeana taarifa juu ya yote yale tuliyoyafanyia *research* ili *input* ya *reseach* hiyo ndiyo itakayoingia kwenye hiyo sheria ya utawala wa Baraza kwamba maeneo mengi ambayo yanahusu kufanya marekebisho tutafanya hivyo.

Mheshimwa kwa kweli tumeombwa jambo hili tuliharakishe kuondoa mizozo ambayo au tofauti ambazo zimekuwepo kwa kipindi kidogo. Kwa hivyo tukubaliane hivyo kwamba hili ni jambo letu na kazi hiyo ilifanywa na sisi wenyewe hapa. Tutaiendeleza wenyewe kwa ujumla wetu wala sio *back benchers* peke yao, lakini pia na serikali tutakwenda kwa pamoja ili tuhakikishe kwamba jambo hili limefikishwa pahala pake na kwenda vizuri zaidi baada ya marekebisho hayo. Basi niombe kwamba jambo hili tusubiri wakati wake na tupate kuendelea, nadhani tuendelee.

## FUNGU 47 - KAMISHENI YA UTUMISHI

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 0201 | Utawala Unguja | 818,000,000 |
| **Jumla ya Fungu** | | **818,000,000** |

*(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)*

## FUNGU 48 - TUME YA UTUMISHI

Kifungu 0201

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante Mhe. Mwenyekitik, nilipokuwa nikichangia kuhusu kitengo cha Mwanasheria wa *DPP* Mhe. mwalimu Haji Omar Kheri kwa mara yangu ya mwanzo kukusikia kwamba ni

mwalimu, sina habari kama ni mwalimu wa skuli au ustadhi. Alinijibu kwamba suala hili analishughulikia kuhusu kiwango cha mishahara. Sasa kushughulikia hivyo anaweza kunambia kwamba lini litamalizika suala hili.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Waziri wa Utumishi wa Umma na Utawala Bora, umelipata vizuri suala hili.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:** Nimelielewa na Mhe. Jaku Hashim Ayoub, nafikiri angenisikiliza vizuri nilisema kwamba hili jambo tumelishughulikia na wamefaidika watumishi wa *DPP* kupata kile ambacho walikiomba. Moja kati ya Ofisi ambazo zimefaidika na kuwatengeneza wataalamu wake ni pamoja na Ofisi ya *DPP* na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na ndio maana hata wajumbe kwenye hoja za nyuma walivyokuwa wakiwadai madai wafanyakazi wa Mahkama za Mwanzo wakilinganisha kufaidika kwa ofisi hizo. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, hili jambo lishamalizika kwa maana pale Ofisi ya *DPP* na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu mambo yapo bomba.

| | |
|---|---|
| Kifungu 0201 Utawala Unguja | 667,000,000 |
| **Jumla ya Fungu** | **667,000,000** |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

## FUNGU 44 OFISI YA RAIS UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA

Kifungu 0401

**Mhe. Ismail Jussa Ladhu:** Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nilizungumzia suala la mradi wa *e-Government* unaoambatana na mradi wa mkonga wa taifa. Tulipokuwa tunapitisha vifungu vya matumizi ya kawaida nilikuja na hoja ya Kamati Teule ambayo tumeshakubaliana kwamba tuisimamishe mpaka tufike katika Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Lakini nilitaka muongozo wako ukanambia nizuie mpaka itakapofika katika linalohusika, sasa hapa ndio pahala pake Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, katika fungu hili la Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kwenye shughuli za maendeleo *sub-vote* 0401 kijifungu 740021 huduma za kiserikali kwa njia ya mtandao e-*Government* pameombwa shilingi 450,000,000/= ambazo zote ni *government contribution* kwa maana zinalipiwa kutoka mfuko wa Hazina wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, fungu hili la shilingi 450,000,000/= nikilioanisha na kitabu cha hotuba ya Mhe. waziri katika ukurasa wa 38 hadi 40 ambapo anazungumzia Idara ya Teknolojia, Habari na Mawasiliano, ndipo ambapo linapatikana katika ukurasa wa 40 kwenye *paragraph* ya 87.

Mhe. Mwenyekiti ukitizama maelezo ni machache kwa sababu idara hii ni mpya lakini neno ninalojirejea kila pahala ni la kiswahili lile la *e-Government,* ni serikali mtandao. Sasa hoja yangu ni kwamba ikiwa katika hotuba hii hii, suala la mkonga wa taifa ambalo lilihusishwa mno na ufanisi wa mradi mzima wa *e-Government* kwamba ule ufanisi wake, ile *speed* ya mtandao itayopelekea huduma hizi zikafanyika vizuri basi ingepelekea kufanikiwa suala lile.

Sasa huko kwenye mkonga wa taifa, Waziri mwenyewe katwambia kutokana na matatizo ya kuchelewa katika ukurasa ule nadhani wa 11, kutokana na kuchelewa kuanza kwa matumizi ya huduma za mkonge wa mawasiliano ya *ICT* hakuna makusanyo. Sasa limehamishiwa Wizara ya Fedha, lile tumesema tutaliundia Kamati Teule na nikauliza pale muongozo wako kwamba ikiwa hali ni hiyo najua *e-Government* unaweza ukatumia hata mtandao unaotolewa na *ZANLINK* au ukatolea *ZANZINET,* wote ni watoaji wa huduma za mitandao.

Lakini nilikuwa ninajiuliza kwamba hivyo ikiwa tayari kuna matumizi ya fedha ambayo hatujaridhika, wajumbe tumeyaweka *pending* ni halali kupitisha shilingi 450,000,000/=, tena kwa mradi wa *e-Government* ambao msingi wake uwezeshaji wake unategemewa kufanikiwa kwa mradi ambao mpaka sasa hivi hatuna uhakika nao, ndio maana nikataka muongozo wake Mhe. Waziri nione kwamba ikiwa tunaweka *pending* mpaka tumchunguze basi na hili ninafikiri lingekaa *pending* mpaka tulijue hatma yake, kwa sababu kama nilivyosema Mhe. Mwenyekiti mradi ule baada ya kukamilika huko

Mazizini, sasa inaonekana umekabidhiwa, unaonekana ni sehemu ya hiyo *e-Government.*

Sasa fedha hizi ningepaswa kujua zinakwenda kufanya shughuli gani lakini pili je, kuna uhalali wa kuidhinisha fedha hizi ikiwa wajumbe wa Baraza lako bado tuna wasi wasi na ile milioni kumi na tisa dola zaidi ya bilioni thalathini ya pesa za Tanzania. Malipo mengine mbali mbali ambayo yamefanywa tangu mwaka juzi ambayo mpaka leo matumizi yake hatuyajua Mhe. Mwenyekiti, naomba sana maelezo.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora:** Mhe. Mwenyekiti kwanza nisema nimshukuru Mhe. Jussa kwa maelezo yake hayo lakini niseme kwamba dola milioni kumi na tisa ni za mradi ule wa uanzishwaji wa utandikaji wa mkonga wa taifa na ku-*install* ile *system* ya *e-Government* pale kwenye kituo chetu kikuu cha Mazizini. Kwa hivyo ni vitu viwili tofauti na matumizi yake haya ni tofauti.

Nilisema kwamba kutokana na kuchelewa kwa kuanza na huku hasa kulisababishwa na kuchelewa kwa ku-*sign contract* kati ya serikali na *ZANTEL* ambayo ndio iliyokuwa ilipe hizi bilioni moja milioni mia nne arubaini, kulisababisha sisi tukose kukusanya haya malipo kwa sababu hakuna biashara ambayo ilifanyika. Lakini *contract* imeshasainiwa na serikali, na *contract* hii imesainiwa kati ya Serikali na *ZANTELl* kwa ajili ya kufanya kazi nyengine ambazo *ZANTEL* wako tayari kuweza kuzikamilisha. Na sisi tukaona ni busara kwamba tusiwe wakusanya mapato, makusanyo tuyarejeshe Wizara ya Fedha lakini kwa sababu hatukuwahi kuifanya kazi hiyo sisi tusijihusishe na ukusanyaji wa mapato yanayotokana na faida itakayopatikana na matumizi ya mkonga wa taifa ambayo tutalipwa na hii kampuni ya *ZANTEL* kupitia shughuli mbali mbali ambazo watazifanya.

Faida nyengine ambayo tutaipata ni kuunganisha na Ofisi zote za Serikali au za umma kama tutaona katika vitabu mbali mbali, wengine wameanza kutoa maelezo kwamba wametenga fedha kwa ajili ya kujitayarisha na huo uungwanishwaji wa hiyo *system ya e-government.* Sasa pesa hizi ambazo sisi tumezitenga mwaka huu tunataka kuzitumia katika maeneo yafuatayo.

Kwanza kuimarisha kwa huduma za umeme pale katika kituo chetu pale cha serikali, mtandao pale tuna tatizo ya *law votage* ya umeme. Kwa hivyo tunataka kuhakikisha umeme unakuwa sawa ili kile kituo kiweze kufanya kazi zake vizuri.

Lakini jengine tunataka kulipa leseni ya matumizi ya program ambazo tutazifanya. Jengine ni kwa ajili ya kujenga vituo mbali mbali vidogo vidogo vile vya huduma ya serikali mtandao katika maeneo tofauti tofauti. Sasa Mheshimiwa nilikuwa nasema ni vizuri Mhe. Ismail akaziruhusu hizi fedha kwa sababu nia yetu ni kutaka kile kitu kifanyike na labda nitoe taarifa moja muhimu sana kwa Baraza lako Tukufu, kuwa hivi karibuni tu tunatarajia kuwapata wenzetu kutoka Singapore ambao wamewasaidia sana wenzetu wa Rwanda katika kufanikisha masuala haya ya mtandao katika nchi yao na wataalamu hao wamekubali kuja kwetu kushirikiana na sisi kwa kutusaidia ili kufikia lile lengo ambalo tumelifikia.

Sasa natambua *concern* Mhe. Ismail lakini mimi nimuombe kwamba sisi aturuhusu na Baraza lako liridhie, kwa maana Kamati ya Matumizi liidhinishe hizi shilingi milioni mia nne hamsini ili zituwezeshe kwenda kufanya kazi wa yale mambo ambayo tunayahisi yanaweza yakatusaidia katika uendeshaji wa shughuli hizi za *e-Government*.

Mhe. Mwenyekiti nilikuwa na maelezo hayo. Ahsante.

**Mhe. Ismail Jussa Ladhu:** Mhe. Mwenyekiti, ninashukuru kwa maelezo hayo ya Mhe.Waziri. Najua Mhe. Mwenyekiti, tangu jana mpaka leo palikuwa na mafunzo makubwa ya istillahi za lugha katika mjadala wa Wizara hii, umepata bahati kubwa sana mjadala wa Wizara hii. Tulifundishwa hapa kuna harufu, unuko, uvundo. Zote istillahi zilikuja katika bajeti ya Wizara hii.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, unajua Wahenga walitwambia kwamba, “Ukitafunwa na nyoka ukiona ung’ong’o unakimbia”. Kwa sababu harufu nzima ya e-*Government* na mkonga wa taifa ambazo zinatofautiana na Mhe. Waziri aliposema kwamba haihusiani, kwa sababu yeye mwenyewe kakiri kwamba ile milioni 19 dola ilikuwa ni kuweka *fiber optic,* yaani huo mkonga wa taifa na kuweka kile kituo cha *e-Government.* Kwa hivyo inahusiana.

Sasa ukiihusisha hii ndio ile sijui ama inaingia kiwango cha unuko au uvundo, lakini ndio ile hofu inayokuja.

Mhe. Mwenyekiti sina tatizo kwa sababu sitaki nizuie fungu bure bure, sina tatizo kwenye kifungu najua yote itakuja kutegemea yale maamuzi yetu ambayo tunayasubiri ya kwenda kuchunguza mradi mzima ikifika Wizara kama haijatutosheleza na maelezo. Lakini niombe basi Mhe. Mwenyekiti kama nilivyosema katika mchango wangu mwengine kwamba nilipotoa hoja ile ile ya Kamati Teule nilikinukuu kifungu cha 23 cha *Public Finance Act* ya mwaka 2005 ambacho kimsingi Mhe. Mwenyekiti, kingekuwa kinatekelezwa, hili zogo na mabishano na hoja nyingi katika miradi ya maendeleo katika Baraza lako lingepungua sana, ingelikuwa serikali kila *contract* inayohusu *development project* inaileta mbele ya Baraza na masharti ya (a),(b),(c), yaliyowekwa hapa yanawekwa juu ya meza.

Kwa hivyo niombe Mhe. Mwenyekiti, kwa hili tunaanza, hivyo zile *contract* ambazo zimo katika masuala haya katutajia za kulipa leseni na vitu vyengine ndio vitakavyosaidia kuweka uwazi katika kuzilinda na kuhakikisha matumizi bora ya fedha za walipa kodi maskini na wanyonge wa nchi hii. Mhe. Mwenyekiti naruhusu tuendelee lakini naomba kuanzia sasa, serikali izingatie na sisi tutakuwa wakali, tutaitumia *Public Finance Act* ya mwaka 2005 kutilia nguvu masharti ya kifungu cha 25 cha sheria. Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo, nasema tuendelee.

**Mhe. Mwenyekiti:** Nilichelea kutoa muongozo mapema ili tujue nini hasa fedha hii inahitajika ifanyiwe na kwa kuwa jambo hili la *e-Government* linahitajika kutoa fedha hizi, maana yake tunasimamisha isiendelee. Kwa hivyo ninakushukuru kwa kuliona hilo na kwa hivyo tunaendelea.

| | |
|---|---|
| Kifungu 0401 Idara ya Mipango Sera na Utafiti | 700,000,000 |
| **Jumla ya Fungu** | **700,000,000** |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 50 MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA WAHUJUMU UCHUMI**

| | |
|---|---|
| Kifungu 0201 Utawala Unguja | 480,000,000 |
| **Jumla ya Fungu** | **480,000,000** |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

*(Baraza lilirudia)*

**Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora:** Mhe. Spika, ilivyokuwa kamati ya matumizi imejadili na kupitisha makadirio ya fedha ya wizara yangu bila ya mabadiliko, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali makadirio hayo.

**Mhe. Waziri wa Afya:** Mhe. Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe nikushukuruni sana lakini nitoe shukurani pia kwa Mhe.Waziri kwa jitihada kubwa na ninafikiri ni vizuri basi Mawaziri au Serikali kwa ujumla ikawa inatoa majibu kwa utulivu namna kama hii ili tufikie pahala Wawakilishi wa wananchi kwa faida ya wananchi waelewe na wananchi kule wapokee yale tunayowafanyia katika chombo chetu.

Nichukue nafasi hii pia kumshukuru Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa kutoa kauli hapa leo ili kuhakikisha kwamba mambo yanayokwama basi yakwamke. Kwa hivyo yamekwamka nakushukuru sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, tunashukuru pia watendaji wa Ofisi hii kwa kumsaidia sana Mhe. Waziri pale kiasi cha kwamba tukafikia pahala saa hizi 2.05 tunamaliza shughuli hii.

Baada ya hayo basi Waheshimiwa Wajumbe ninaahirisha kikao hiki hadi kesho tarehe 4/07/2013 saa 3.00 barabara za asubuhi, Waheshimiwa wajumbe saa 3.00 barabara za asubuhi. (*Makofi).*

*(Saa 2.05 usiku Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 04/07/2013 saa 3.00 asubuhi)*